# Nipashe

Jumanne Septemba 24, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580031

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Vigingi saba vinavyomkabili mkuu mpya mkoa Morogoro

UKURASA 2




UKURASA 13

# DPP afunguka masharti watakaokiri kuhujumu

• **Abainisha** njia za kufuata hadi msamaha, wadau wapokea kwa hisia, watoa ushauri...*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**OFISA USALAMA POSTA MATATANI**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanamshikilia Ofisa Usalama wa Shirika la Posta Tanzania, George...

UKURASA WA 5

**WATUHUMIWA KESI BOMBA LA MAFUTA WAACHIWA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewafutia mashtaka na kuwaachia huru, washtakiwa watano waliokuwa wanakabiliwa na tuhuma za kujiunganishia...

UKURASA WA 5

**HABARI NJEMA WAOMBAJI MIKOPO ELIMU YA JUU**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imewatangazia wanafunzi wanaoomba mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020, kuwa kwa sasa...

## Kicheko matumizi mabomba ya ndani

UKURASA 3







Mabaki ya ndege ndogo ya Shirika la Auric Air, iliyopata ajali katika uwanja mdogo wa ndege eneo la Seronera ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti jana asubuhi na kusababisha vifo vya watu wawili akiwamo rubani wake, Nelson Mabeyo (Picha ndogo). **NA MPIGAPICHA WETU**

## Ajali ya ndege ndogo yaua mtoto wa mkuu wa majeshi

UKURASA 2


**MICHEZO** **DANTE AITWA YANGA KUONGEZA NGUVU** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# DPP afunguka masharti watakaookiri kuhujumu

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, ametaja mambo mawili muhimu katika utaratibu wa kuachiwa huru kwa mahabusi wa kesi za uhujumu uchumi ambao ukomo wake ni siku nne zijazo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, DPP Mganga aliyataja masharti hayo kuwa yanajumuisha mtuhumiwa mwenyewe kukiri kosa pasipo kumhusisha wakili na kuandika barua rasmi ya kuonyesha dhamira yake hiyo.

Juzi, Rais Magufuli wakati akiwaapisha viongozi wa serikali aliowateua Ijumaa, alishauri watuhumiwa wa makosa hayo walio tayari kuomba msamaha na kukiri makosa yao na wako tayari kurejesha hasara ya fedha zinazowahusu, wapewe fursa hiyo kabla ya Jumamosi ijayo.

DPP Mganga akielezea hatua za utekelezaji wake, ni kwamba mtuhumiwa mwenyewe aliyeko mahabusu, anatakiwa aandike barua kupitia kwa mkuu wa gereza akikiri kosa na kuomba kutubu haraka iwezekanavyo na wao watachukua hatua.

"Jambo hili linatakiwa kufanywa na mtuhumiwa mwenyewe aliyeko gerezani na siyo wakili kwani kukiri kosa na kuomba toba ni jambo zito linalohitaji utashi binafsi na si kuwakilishwa," DPP Mganga alisisitiza.

"Ni mtuhumiwa mwenyewe ndiye anayetakiwa kuandika barua siyo wakili. Unajua wakili anaweza kubadilika na hata mtuhumiwa kumkana kuwa sijamtuma afanye alichokifanya kwa niaba yangu.

"Ndiyo maana mara zote watuhumiwa wanaomba msamaha na kukiri kuandika barua wenyewe kwa mkono wao kupitia kwa mkuu wa gereza," alifafanua.

Katika kauli yake hiyo ya juzi Ikulu, Rais Magufuli alipendekeza DPP kuwasikiliza watuhumiwa hao ndani ya wiki moja kuanzia jana ili kutoa fursa kwa wenye dhamira ya kutumia nafasi hiyo kutoka mahabusu.

Akifafanua sababu za kufikia uamuzi huo, Rais Magufuli alisema: "Huwa naumia sana kuona watu wapo mahabusu au wafungwa kwa miaka mitatu hadi minne, lakini kwa kuwa sheria zipo, huwa nakaa kimya.

"Mtu anapowekwa mahabusu na anakaa miaka mitatu inaumiza, nisingependa kuongeza na kuona watu wanatoa machozi. Ningekuwa na uwezo, siku moja nione hakuna mfungwa, mahabusi.

"Kuna watu wapo mahabusu kwa zaidi ya miaka, lakini wapo ambao wanataka kutubu kwa makosa waliyoyafanya. Kama wapo watu wa namna hii, ninashauri DPP mkawasikilize kuanzia kesho (jana) hadi Jumamosi ya wiki ijayo, kama wapo walioshtakiwa kwa kesi za uhujumu uchumi na wapo tayari kurudisha fedha wakatoke ndani.

"Nenda DPP kasimamie hilo, upange

INAENDELEA UK. 8



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiangalia sehemu ya mabaki ya hoteli ya Coco Beach, jijini humo jana, baada ya kuteketea kwa moto, juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Ajali ya ndege ndogo yaua mtoto wa Mkuu wa Majeshi

**Rahma Kisilwa na Jovin Lamwel,**

TUDARCo

RUBANI Nelson Mabeyo ambaye ni mtoto wa Mkuu wa Majeshi na rubani mwanafunzi, Nelson Orutu, wamefariki dunia katika ajali ya ndege ndogo iliyotokea eneo la Seronera ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Ndege hiyo aina ya C208B EX yenye namba za usajili 5H-AAM, ilianguka jana katika eneo la kurukia ikielekea kiwanja cha ndege cha Grumeti nje kidogo ya hifadhi hiyo wakati inakwenda kuchukua abiria. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Thomas Ngulika, ajali hiyo ilitokea jana saa 1:35 asubuhi.

"Ndege hiyo imeanguka mara tu baada ya kuruka ikiwa imebeba watu wawili akiwamo rubani wa ndege na rubani mwanafunzi na wote walifariki (dunia).

"Wizara imemtuma mkaguzi wetu wa ajali za ndege kuelekea eneo la tukio ili kutuletea taarifa kamili," ilielezwa katika taarifa hiyo ya wizara.

Taarifa kutoka Serengeti zilidai kuwa jana saa 2:35 asubuhi, chopa ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ilitua kwenye uwanja wa huo kwa ajili ya kuchukua mwili ambao ulihifadhiwa katika zahanati ya Soronera.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu, alisema helikopta hiyo ilipelekwa kwa ajili kuchukua mwili wa mmoja wa marubani waliopoteza maisha kutokana na ajali hiyo.

Kiongozi wa msafara kutoka JWTZ, Meja Makimboka, alisema wataalamu wa jeshi watafika eneo la ajali kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

"Pamoja na wataalamu wa anga, jeshi pia linaleta wataalamu wake kwa ajili ya uchunguzi, sisi tunachukua mwili tu kwa sasa," alisema.

Taarifa ya awali ilitolewa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Mawasiliano wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Paschal Shelutete, ilieleza: "Ndege hiyo ya Kampuni ya Auric imeanguka leo (jana) asubuhi ikiwa imebeba watu wawili, wakati inaruka kwa bahati mbaya ilianguka na kusababisha vifo vya Watanzania wawili."

Shelutete alidai katika taarifa yake hiyo kuwa chanzo cha ajali hiyo hakijajulikana kwa kuwa ilipata hitilafu ambayo haijajulikana na inasubiri uchunguzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA).

TCAA ilithibitisha ajali hiyo na kueleza kuwa ndege iliondoka jijini Dar es Salaam juzi kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Terminal I.

"Baada ya kuhakikiwa na kuonekana ipo sawa, iliruhusiwa kuruka na kwenda Gurument kwa ajili ya kuwachukua wageni na kuwapeleka Uwanja wa

INAENDELEA UK. 8

# Vigingi saba RC mpya Morogoro

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli juzi alimwapisha Lootha Sanare kuwa Mkuu mpya wa Mkoa wa Morogoro, akichukua nafasi ya Dk. Stephen Kebwe ambaye uteuzi wake ulitenguliwa Ijumaa kutokana na kile kilichoelezwa kuwa utendaji mbovu katika kusimamia majukumu yake.

Kabla ya kupewa jukumu la kuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Sanare alikuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha.

Katika kuiongoza Morogoro, Sanare anapaswa kujipanga kuvikabili vigingi saba ili kutoingia katika orodha ya wakuu wa mikoa waliotumbuliwa kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yao.

## MATUMIZI MABAYA YA FEDHA

Katika hotuba yake ya juzi Ikulu jijini Dar es Salaam wakati akiwaapisha viongozi wa serikali aliwaoteua Ijumaa, Rais Magufuli aliweka wazi kuwa Mkoa wa Morogoro umewasumbua kwa kiasi kikubwa katika kuongoza kutokana na mambo mengi kusimama.

Rais Magufuli alisema halmashauri za mkoa huo zimekuwa na matumizi ya ovyo ya fedha, jambo lililosababisha baadhi ya wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kugombana.

Alisema alishawahi kumtuma Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, mkoani humo na alibaini changamoto lukuki.

Rais Magufuli alisema miradi ya maendeleo katika mkoa huo haimaliziki licha ya serikali kupeleka fedha, akitolea mfano wa Sh. bilioni 1.3 zilizopelekwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati lakini fedha hizo zilikaa kwa mwezi mmoja bila kutumika.

## UWAJIBIKAJI

Rais Magufuli alisema watendaji wa Mkoa wa Morogoro wamekuwa hawafanyi vizuri katika kutimiza majukumu yao., lakini mkuu wa mkoa hakuchukua hatua dhidi yao.

Sanare anapaswa kuhakikisha watendaji walio chini yake; wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri wanafanya vizuri katika utendaji wa kazi.

"Haiwezekani watendaji walio chini yako hawafanyi vizuri halafu unajiita RC (Mkuu wa Mkoa) ndiyo maana nikampeleka huyu aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Arusha, ninajua nampeleka mahali penye changamoto nyingi," Rais Magufuli alisema.

## MIGOGORO YA ARDHI

Morogoro ni miongoni mwa mikoa yenye migogoro mingi ya ardhi inayosababisha wafugaji na wakulima kuuana wakigombea maeneo kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Sanare anapaswa kujipanga kuhakikisha anatatua changamoto hiyo ya muda mrefu ili kulinda kibarua chake kwa kuwa hata Rais Magufuli aligusia suala hilo kwenye hotuba yake ya juzi.

"Wewe (Sanare) kwa kuwa umetoka Arusha na unawajua vizuri wafugaji, nimekupeleka Morogoro ili ukatatue changamoto za wakulima na wafugaji, usimwonee mtu," Rais Magufuli aliagiza.

## UWEKEZAJI

Mkoa wa Morogoro una maeneo mengi ya uwekezaji hasa kwenye sekta ya kilimo, lakini umekuwa ukisuasua katika uwekezaji,

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

## THRDC yazungumzia wajumbe Tume ya Haki za Binadamu

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), umesema uwapo wa wajumbe waliotoka serikalini pekee kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kutaifanya ijione kuwa ni sehemu ya serikali na kushindwa kusimamia matukio ya uvunjaji wa haki za binadamu.

Akizungumza jana na Nipashe, Mratibu wa THRDC, Onesmo Ole Ngurumwa, alisema walishiriki kwenye mchakato wa kupendekeza majina na jina la mwakilishi wa asasi za kiraia lilikuwapo, lakini uteuzi haukuwa na uwakilishi.

"Nilishiriki kupendekeza majina yaliyotoka kila sekta ikiwamo asasi zisizo za kiserikali, lakini tumeona walioteuliwa hakuna mchanganyiko kwa kuwa wote wametoka serikalini na kuifanya Tume kuonekana kama kitengo cha serikali kinachotekeleza majukumu ya serikali," alisema na kuongeza:

"Iwapo kutakuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu unafanywa na serikali ni vigumu kwa wajumbe wa aina hiyo kufanya uamuzi kwa kuwa nao watajiona ni kitengo cha serikali wakati haitakiwi kuwa hivyo."

Kwa mujibu wa Ole Ngurumwa ni vyema kukawa na mchanganyiko wa wajumbe wa tume hiyo ili kuleta uwiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

Novemba mwaka jana, THRDC ilizungumza na waandishi wa habari kueleza kuwa kukosekana kwa uongozi wa tume hiyo kumesababisha masuala mengi ya haki za binadamu kutochukuliwa hatua.

Alisema kikatiba na kisheria tume imepewa mamlaka ya aina mbili ya kutumikia umma na kuwa kama mashauri mkuu wa serikali na mihimili mingine pale masuala ya haki za binadamu yanahusika nchini.

Mengine yapo kwenye ibara ya 130 ya Katiba, yakijumuisha kuheshimu haki za binadamu kwa mujibu wa sheria, kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu, kufanya uchunguzi juu ya ukiukwaji haki za binadamu na kutoa mapendekezo.

# Shangwe agizo la JPM mabomba ya ndani

**Na Henry Mwangode**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) limeunga mkono agizo la Rais John Magufuli la kuwapo na ulazima wa kutumia mabomba yanayotengenezwa nchini katika miradi ya serikali.

Akizungumza jana na Nipashe kwa simu, Mtalaamu wa Sera wa CTI, Frank Daffa, alisema wazalishaji wa mabomba wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu tamko la aina hiyo.

Alisema tamko la Rais limewapa hamasa wazalishaji wa bidhaa hizo kuwekeza zaidi na kuzalisha kwa wingi kwa sababu wamepata uhakika wa soko.

"Tunaamini tamko hili litatoa 'support' (msaada) mkubwa. Tunaamini litalinda uwekezaji kwenye sekta hiyo ambao umeshafanyika tayari maana tulikuwa tunasubiri kwa muda kauli kama hii. Kwetu sisi hii imetupa mwanga wa soko la uhakika," alisema Daffa.

Wiki iliyopita, Rais Magufuli wakati akizindua kiwanda cha kutengeneza mabomba cha Pipe Industry Ltd jijini Dar es Salaam, alitoa agizo kwa kutaka miradi yote inayofadhiliwa na serikali kwa asilimia 100 ni lazima itumie mabomba yanayotengenezwa na viwanda vya ndani ili kuvilinda na kupunguza matumizi makubwa ya fedha za serikali katika kuagiza nje.

Katika hotuba yake, Rais Magufuli aliuliza kwa nini mabomba yanayotengenezwa na viwanda vya hapa nchini hayatumiwi kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali licha ya uhitaji uliopo.

"Nataka mabomba ya ndani yapewe kipaumbele, ikiwezekana wekeni kipengele kwenye mikataba na makandarasi kwamba kama hatatumia mabomba ya ndani basi kiwe kigezo cha kutopata tenda," alisema.



Rais Magufuli (pichani) alieleza kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya kulinda viwanda vya ndani, kukua, kupata faida hatimaye kulipa kodi na kuajiri Watanzania wengi.

Alisema kutotumia mabomba yanayozalishwa nchini wakati kuna tani za bidhaa hiyo zinazotengenezwa nchini ni kukosa busara.

Aidha, Rais Magufuli aliwataka wamiliki wa viwanda vya ndani, hasa vya mabomba, kufanya utafiti na kufahamu kwa nini mabomba ya ndani hayapendwi na makandarasi.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Nassor Seif, alisema awamu ya kwanza ya mradi huo umegharimu Sh. bilioni 120.

Kiwanda hicho kwa mujibu wa mkurugenzi huyo kitatengeneza mabomba aina ya PVC tani 25,000, tani 40,000 aina ya HDPE na tani 500 ya GRP.

"Kiwanda hiki kimetoa ajira 215 za moja kwa moja na tunategemea kitakaponalizika kwa awamu ya pili tutaweza kuajili watu 500," alisema Seif.



# Ofisa Usalama Posta matatani tuhuma za mihadarati

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wanamshikilia Ofisa Usalama wa Shirika la Posta Tanzania, George Mwamgabe, kwa tuhuma za kuhusika na usafirishaji wa dawa za kulevya aina ya mirungi kilo 214 kwa kutumia shirika hilo.

Kaimu Kamishna Jenerali wa mamlaka hiyo, James Kaji, alisema jana kuwa, ofisa wa Shirika la Posta, alisema mtuhumiwa huyo awali alitoweka kutokana na mahojiano yaliyokuwa yakiendelea dhidi yake.

"Kwa sasa amekamatwa kwa ushirikiano wa mamlaka ya dawa za kulevya na Jeshi la Polisi, yupo mikononi mwa mamlaka yetu.

"Katika kipindi cha mwezi huu, mamlaka imefanikiwa kukamata dawa za kulevya aina ya heroine katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza pamoja na zaidi ya kilo 215 za vifurushi vya dawa za kulevya aina ya mirungi zilizokuwa zikisafirishwa kwa njia ya posta kutoka Arusha kwenda nchini Uingereza," alisema.

Alisema uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa mkemia mkuu wa serikali ulithibitisha majani ya mirungi yana kemikali aina ya Cathinone ambayo inapatikana kwenye mmea huo.

"Taarifa za awali zilibaini kuwepo kwa kasi kubwa ya usafirishwaji wa dawa za kulevya aina ya mirungi kutoka nchini kwenda nchi za Ulaya hasa Uingereza, Canada na Ufaransa kwa njia ya Posta ambapo awali vifurushi hivyo vilikuwa vikisafirishwa kupitia Posta ya Dar es Salaam na sasa vimekamatwa vikisafirishwa kupitia Posta jijini Arusha.

Alisema mbali ya mtuhumiwa huyo, mamlaka hiyo pia inawashikilia watuhumiwa wengine watano ambao nao wanadaiwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya heroine.

Mamlaka hiyo imetoa rai kwa wote wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya kuacha mara moja na kutafuta kazi halali za kufanya kwa kuwa mkono wa sheria utawafikia popote walipo.

## Maagizo JPM Coco Beach pasua kichwa

**Na Romana Mallya**

MAAGIZO ya Rais John Magufuli kwa watendaji wake yamekuwa pasua kichwa, baada ya kuagiza utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa ufukwe wa Coco Beach ndani ya mwezi mmoja mara mbili na kuonekana utekelezaji wake ni ndivyo sivyo, Manispaa imepata kigugumizi kuzungumzia hilo.

Wiki moja iliyopita, Rais Magufuli alionyesha kukerwa na baadhi ya viongozi ambao hawasimamii na kuchukua maamuzi utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwamo uendelezaji wa ufukwe wa Coco.

Baada ya kauli hiyo siku iliyofuata viongozi wa Manispaa ya Kinondoni waliibukia Coco na kutangaza kufunga kupisha ujenzi.

Juzi, Rais Magufuli wakati akiwaapisha baadhi ya viongozi aliowateua Ikulu jijini Dar es Salaam miongoni mwa mambo aliyoyazunguzia ni ujenzi wa ufukwe huo na kushangaa mkandarasi kukabidhiwa Sh. bilioni 14 kwa ajili ya kujenga ghorofa moja.

Rais Magufuli alisema eneo ambalo mkandarasi amekabidhiwa kwa ajili ya ujenzi huo ndipo patajengwa mradi wa ujenzi wa

INAENDELEA UK.8



Kaimu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzia na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, James Kaji (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kukamata zaidi ya kilo moja na nusu ya dawa za kulevya aina ya Heroin katika mikoa wa Dar es Salaam na Mwanza. Kushoto ni Kamishna wa Operesheni, Luteni Kanali Fredrick Milanzi na Kaimu Kamishna wa Huduma za Sheria wa mamlaka hiyo, Edwin Kakolaki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

# Wingu zito dhamana kwa vigogo Simba

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kutoa au kusimama kusikiliza maombi ya dhamana ya vigogo wa zamani wa Simba, akiwamo aliyekuwa Rais wa klabu hiyo, Evance Aveva, itajulikana Septemba 27, mwaka huu.

Mahakama hiyo inatarajia kutoa uamuzi baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) jana kuwasilisha kusudio la kukata rufani Mahakama Kuu kwamba hajaridhika na uamuzi wa mahakama hiyo kuwaondolea mashtaka ya kutakatisha Dola za Marekani 300,000.

Akiwasilisha hoja za kusudio hilo Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, alidai kuwa upande wa Jamhuri unapinga uamuzi wa mahakama hiyo kuwaondolea mashtaka ya kutakatisha fedha Aveva na Makamu wake Godfrey Nyange maarufu kama Kaburu ikiwamo kuwapa masharti ya dhamana.

Washtakiwa hao wanaokabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi mahakamani na wiki iliyopita, waliondolewa mashtaka ya utakatishaji, hivyo kupewa masharti ya dhamana ambayo hata hivyo walishindwa kuyatimiza.

Kesi hiyo jana ililetwa mahakamani hapo kwa ajili ya upande wa mashtaka kuwasilisha hoja zao juu ya kusudio lao la kukata rufani mbele ya Hakimu Simba.

Akiwasilisha hoja hizo, Wakili Simon alidai kuwa anaomba kusimamishwa kwa usikilizwaji wa kesi hiyo na hatua nyinginezo ikiwamo kutoa dhamana.

Wakili huyo alidai kusudio la rufani linasimama kama rufani, hivyo rufani ya DPP tayari iko mahakama ya juu huku akitolea mfano wa uamuzi mbalimbali uliokwishatolewa na Mahakama Kuu.

Wakili wa utetezi, Nehemia Nkoko, akijibu hoja hizo, alipinga ombi la DPP na kudai kuwa mahakama hiyo ina uwezo wa kuendelea kutoa dhamana kwa washtakiwa hao huku ikisubiri uamuzi wa Mahakama Kuu.

Nkoko alidai kuwa mahakama hiyo inaweza kusimamisha kesi hiyo pale tu DPP atakapowasilisha rasmi rufani yake Mahakama Kuu kwa mujibu wa taratibu za Mahakama ya Rufani. Kutokana na hoja hizo, Hakimu Simba alisema atatoa uamuzi Septemba 27 mwaka huu.

Katika kesi hiyo, washitakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashitaka tisa na wiki iliyopita mahakama iliyaondoa mawili ya utakatishaji fedha kwa kuwa upande wa mashitaka ulishindwa kuyathibitisha.

Masharti ya dhamana waliyopewa ni kuwa na wadhamini wawili kila mmoja atakayetia saini bondi ya Sh. milioni 30 na vitàmbulisho.

Hata hivyo, washtakiwa hao pamoja na mwenzao Zacharia Hansppope walikutwa na kesi ya kujibu katika mashtaka saba ambayo ni kughushi, kula njama, matumizi mabaya ya madaraka, kutoa nyaraka za uongo na kutoa maelezo ya uongo ambayo upande wa mashtaka umethibitisha.

# Watuhumiwa kesi bomba la mafuta waachiwa huru

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewafutia mashtaka na kuwaachia huru, washtakiwa watano waliokuwa wanakabiliwa na tuhuma za kujiunganishia isivyo halali bomba la mafuta, mali ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, wakati kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Awali upande wa Jamhuri ulidai kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) anaomba kuwaondolewa washtakiwa mashtaka yao kwa sababu hana nia ya kuendelea na kesi hiyo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Simon Wankyo, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa lakini DPP hana nia ya kuendelea na kesi dhidi ya mshtakiwa hao.

Washtakiwa hao wamefutiwa mashtaka hayo chini ya kifungu namba 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), sura ya 20, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Hakimu Simba alisema kupitia kifungu hicho mahakama imewafutia mashtaka washtakiwa hao watano na imewaachia huru.

Washtakiwa waliofutiwa kesi ni Audai Ismail (43) ambaye ni mkazi wa Kibaha, Chibony Emmanuel, Roman Abdon, Amina Shaban na Zubery Ally.

Hakimu Simba alisema kupitia kifungu hicho namba 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), DPP anao uwezo wa kuwakamata na kuwafungulia mashtaka, washtakiwa hao.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanadaiwa kati ya mwaka 2015 hadi Januari 8, 2018 katika eneo la Tungi Muungano wilayani Kigamboni, walijiunganishia bomba la mafuta ya dizeli lenye upana wa inchi moja kutoka katika bomba lenye upana wa inchi 24 bila kuwa na kibali.

Katika shtaka la pili washtakiwa walidaiwa kuharibu miundombinu na kwamba siku hiyo ya tukio, walitoboa bomba la hilo ambalo lilikuwa likitumika kusafirisha mafuta mali ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Katika shtaka la tatu, washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kuharibu bomba la mafuta mazito (crude oil) lenye upana wa inchi 28, ambalo lilikuwa likitumika kusafirisha mafuta ghafi, mali ya TPA.

# Habari njema waombaji mikopo elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imewatangazia wanafunzi wanaoomba mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/2020, kuwa kwa sasa inaendelea na kazi ya uhakiki wa maombi yaliyowasilishwa ambayo itakamilika mwishoni mwa wiki hii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo, Abdul-Razaq Badru (pichani), baada ya kukamilika kwa kazi ya uhakiki, Bodi itatoa fursa ya siku nne kuanzia Jumatatu, Septemba 30 hadi Alhamisi, Oktoba 3, 2019 kwa waombaji mikopo ambao maombi yao yatakuwa yamebainika kuwa na upungufu kufanya marekebisho.



"Taarifa hii inatolewa kufuatia bodi kupokea maoni na maswali kupitia barua pepe na simu kuhusu hatua iliyofikiwa katika uhakiki na uchambuzi wa maombi ya mikopo ya elimu ya juu yaliyowasilishwa kwenye bodi," ilisema taarifa hiyo.

Iliwataka waombaji mikopo wote kutembelea tovuti ya bodi (www.heslb.go.tz) au kuingia katika akaunti zao walizoombea mkopo kupitia mfumo wa uombaji mkopo (www.olas.heslb.go.tz) kuanzia Septemba 30, 2019.

Ilisema tovuti ya bodi itawapa mwongozo wa kufanya marekebisho kwa njia ya mtandao na baada ya kuingia, watapata ujumbe iwapo maombi yao yamekamilika au yanahitaji marekebisho.

Taarifa hiyo ilisema imejipanga kuhakikisha kazi yote ya uhakiki na uchambuzi wa maombi yote ya mikopo inakamilika ifikapo Oktoba 6, mwaka huu.

Aidha, ilisema wanafunzi wahitaji watapangiwa mikopo, watapata taarifa na fedha za mikopo zitatumwa vyuoni kabla ya vyuo kufunguliwa katika wiki ya kwanza ya mwezi Novemba.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuomba radhi kunaweza kuwa tija kesi uhujumu

**HATUA** ya Rais John Magufuli kuwashauri watuhumiwa wa kesi za kuhujumu uchumi na kutakatisha fedha walioko mahabusu kuomba radhi na kurejesha mali wanazodhani hazikupatikana kiuhalali, ni sawa na kuwaambia Watanzania hao njooni tuyamalize.

Ni nia njema ya Rais ya kusikiliza kilio cha familia nyingi zinazomsihi kuwaangalia jamaa zao walioko mahabusu magerezani, lakini pia kama binadamu ni kuwa na huruma kwa watu hao ambao wanastahili kusikilizwa ya moyoni.

Tunaipongeza hatua ya kumtuma Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasikiliza ili kama wanakubaliana na ushauri wa serikali waombe radhi na kurudisha mali wanazoamini kuwa zilikuwa na walakini katika kuzipata.

Mapendekezo hayo ya Rais yana nia njema na yanakusudia kutoa haki ya wahusika kuzungumza yale ambayo wanatamani kuyasema ambayo kupitia mahakamani wasingeweza kupata fursa hiyo.

Tunawashauri kuwasiliana na DPP kueleza ya moyoni na ukweli wa mambo ili kujinusuru na mlolongo wa mashtaka ambao kwa kuitikia wito huo, wanakuwa wamejinasua nao.

Ni ukweli kwamba kuna washtakiwa na wafungwa ambao wako mahabusu magerezani na ambao kesi zao au rufani zao hazijasikilizwa.

Kuchukua hatua hiyo ni wazi kuwa kutasaidia kupunguza idadi ya watu wanaookaa mahabusu kusubiri mashtaka yao kutajwa na wengine wanaongoja rufani zao kusikilizwa.

Inawezekana pia wapo wengine mahakamani ambao kesi zao hazijasikilizwa na polisi wanaendelea kusaka ushahidi, hivyo ni vyema kuwapunguza kwa utaratibu huo wa kuomba radhi, kukiri makosa na kurejesha mali.

Tunaipongeza serikali kwa sababu inafahamika kuwa ni gharama kubwa kuwatunza wafungwa na mahabusi magerezani na kama ilivyofanyika ni njia mojawapo ya kupunguza msongamano.

Tunatoa wito kwa wanaohusika na kesi hizo ambao wanakubaliana na ushauri huo kama hawatajali kuomba radhi, kukiri kuwa kweli wanahusika na kulipa mali walizochukua kwa njia zisizokuwa halali.

Aidha, wamepewa muda wa kuzungumza na DPP na kueleza ya moyoni, hivyo ni vyema pia wakatumia mwanya huo kueleza programu ya namna ya kuzirejesha mali hizo ili waendelee kuishi na kufanya shughuli zao.

Jambo la kutia moyo ni kuwa DPP jana alianza kutekeleza mapendekezo ya Rais, kwa kutangaza utaratibu ambao wahusika watapaswa kuufuata.

Kwa upande mwingine tunaona kuwa suala la kurejesha mali zikiwamo fedha ni muhimu kwa kuwa zinaweza kutumiwa katika utekelezaji wa miradi ya kuwasaidia wananchi na maendeleo kwa ujumla badala ya kubakizwa kwenye mikono ya wapelelezi na waendesha mashtaka kama ushahidi.

Kumbukeni hakuna jambo lisilosameheka, kikubwa ni kueleza ukweli na kufanya jambo ambalo litaleta tija kwa watuhumiwa na familia zao pamoja na Watanzania ambao watanufaika na kurejeshwa mali hizo.

Tunapongeza serikali kulifanya jambo hilo kuwa la ana kwa ana kati ya DPP na washtakiwa. Tunaamini hiyo ni njia rahisi ya kuwafanya wahusika kuwa huru tofauti na pengine hatua kama kuwaambia wakiri makosa yao mbele ya jopo au kadamnasi.

Kwa wahusika walioko mahabusu magerezani tunawashauri kulichukulia jambo hilo kwa wepesi badala ya kuumia moyo na kuona kuwa pengine hawakustahili kufanyiwa hivyo.

Tunaamini kuwa hawana haja ya kuona uchungu kwa kuwa ni hatua inayolenga kuwaondolea fikra za maumivu ya kuendelea kusota mahabusu kwa muda mrefu zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanunuzi wa pamba wawezeshwe kuwalipa wakulima kwa wakati

Na Raphael Kibiriti

**KUNA** mengi ambayo Tanzania inaweza kuyabainisha kama sehemu ya majaliwa iliyokirimiwa na Mwenyezi Mungu, miongoni mwake ni maliasili mbalimbali.

Imejaliwa kwa mfano misitu, wanyama, bahari, maziwa, mito, milima kama Kilimanjaro, madini ya aina tofauti na maliasili zingine zinazojenga ustawi wa nchi.

Lakini ukiachana na hilo la maliasili, inajivunia kwa kiwango kikubwa kumpata Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, mwasisi ambaye alikuwa na sifa nyingi, ikiwamo ya kuwa mtetezi wa watu, hasa wanyonge.

Na katika hili la kutetea wanyonge kwa mfano alikuwa anajali sana maslahi ya wakulima ambao ndio walio wengi nchini hadi nyakati hizi.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, zaidi ya asilimia 66 ya Watanzania ni wakulima, wengi takribani asilimia 70 wakiishi vijijini.

Utetezi wake kwa wakulima unathibitishwa na moja ya hotuba zake ambapo alipinga suala la vyama vya ushirika kwa wakati huo, kununua mazao ya wakulima bila ya kuwalipa fedha zao taslimu, kwa maana ya kuwakopa na akaiita hatua hiyo kuwa ni ya kinyonyaji.

Msimamo wake ulijikita katika ukweli kwamba kilimo ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi ya wakulima, wengi wao wakiwa wadogowadogo na kwa hiyo wanakitegemea kwa minajili ya kupata kipato cha kuendeleza maisha yao.

Sasa kuwakopa kimsingi ni kukwamisha maendeleo yao yanayotegemea fedha za mauzo ya mazao kugharimia miradi kama ya ujenzi wa nyumba, ununuzi wa vyombo vya usafiri, lakini pia kwa ajili ya kupanua na kuendeleza kilimo chao.

Muungwana amerejea msimamo huo wa Mwalimu, akihusianisha na kinachoendelea sasa kwenye kadhia ya ununuzi wa zao la pamba nchini.

Bado katika maeneo mengi yanayolima zao hilo, kuna wakulima ambao wamekopwa pamba yao, kwa muda sasa na hawajalipwa fedha zao na kampuni za ununuzi. Muungwana ana taarifa kwamba wanunuzi 'wamekubaliwa' sasa wasombe pamba ya wakulima kutoka kwenye maghala ya Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) bila ya sharti la kuilipia kwanza, kama msimamo ulivyokuwa umewekwa awali.

Kilio hiki cha wakulima kutolipwa fedha zao ndicho kilichobainika pia kwenye ziara ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mkoani Geita ya kukagua viwanda vya pamba na kuzungumza na wananchi.

Ikumbukwe kwamba hawa ni wakulima ambao wamepeleka pamba yao kwenye maghala ya AMCOS, lakini kuna wakulima ambao bado wana pamba yao majumbani kwao, wakisubiri fedha ipatikane ndipo waiuze.

Pamoja na ahadi ya serikali kupitia kwa Majaliwa kwamba hakuna mkulima ambaye hatalipwa fedha zake iwapo atauza kupitia AMCOS, Muungwana anakumbusha kuwa wakati ni mali.

Anasema hivyo kwa sababu msimu wa kilimo cha pamba ndio huo, kwani katika maeneo mengine kuanzia mwishoni mwa mwezi wa Oktoba, huwa ni wa kuanza kilimo cha zao hilo.

Na mwezi Oktoba unaingia wiki ijayo, sasa kama kuna wakulima hawajalipwa fedha zao mpaka sasa, kama kuna wakulima hawajauza pamba yao hadi sasa, watajiandaaje kwa msimu ujao wakati kilimo chao kinategemea fedha na fedha zao bado hawajalipwa?

Katikati ya maswali haya mnunuzi mmoja wa zao hilo amenukuliwa akisema kwamba wanalazimika kulipa fedha za wakulima kidogokidogo kwa sababu ya changamoto wanazokutana nazo kutoka benki.

Kwamba pamoja na serikali kuruhusu wachukue fedha kutoka kwenye taasisi hizo, wanakuta benki wakati mwingine zina fedha kidogo kuliko kiasi wanachohitaji na ndiyo maana nao wanapeleka fedha kidogokidogo za kuwalipa wakulima.

Kama ilivyo kwa Baba wa Taifa, Muungwana anaikubali serikali ya awamu hii linapokuja suala la kutetea wanyonge, yakiwemo maslahi ya wakulima.

Ni muhimu basi ikahakikisha wanunuzi wanapata fedha za kutosha ili waweze kuwalipa wakulima fedha zao na hivyo kuwawezesha wajiandae vyema kwa msimu ujao wa kilimo cha pamba.

# Wakazi Kilimanjaro tuiache tabia hii

***Mhariri***

*Habari za majukumu ya ujenzi wa Taifa,*

*NIMEJITOKEZA leo kwenye nafasi hii inayotupa fursa wananchi pamoja na mambo mengine ya kueleza kero na changamoto mbalimbali zinazotukabili kwenye maeneo yetu, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo mbele.*

*Kwa fursa hii, ninapenda kuzungumzia hatua isiyo ya kiungwana au kistaarabu inayofanywa na baadhi yetu sisi wazaliwa wa mkoa wa Kilimanjaro ambayo hata katika misahafu kwa wanaoamini haikubaliki.*

*Tayari watoto wetu, ambao ni wanafunzi waliokuwa wanasoma shule za msingi wamemaliza mitihani yao ya kitaifa katika ngazi hiyo ya elimu, na kwa hali hiyo kwa sasa wako majumbani wakisubiri matokeo yao kwa ajili ya kujiunga na masomo ya sekondari.*

*Sasa wakati wa kipindi hiki wanachosubiri majibu, kuna utamaduni wa wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na hasa sisi Wachaga ya kuchukua watoto hao ili waje watufanyie kazi zetu na hasa zile za kusimamia biashara mbalimbali kwa maana ya kuuza.*

*Kimbembe huwa kinatokea wakati majibu ya mtihani huo yanapokuwa yametoka na kijana akawa amefaulu na kwa hali hiyo akahitajika sasa arudi nyumbani kwao tayari kwa ajili ya maandalizi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwa masomo ya sekondari. Mara nyingi 'matajiri wao' ama wenye biashara ambao wanakuwa wamewachukua watoto hao huwa wakati mwingine hawako tayari kuwaachia, wakitaka waendelee kuwauzia biashara zao.*

*Ndipo visa vya kwamba kuna mapungufu ya fedha kutoka kwenye biashara zao ama kuna mapungufu ya mitaji yaliyojitokeza baada ya kijana huyo kuwa ameanza kuisimamia biashara husika kabla hajaja.*

*Ndipo unakuta kijana wa watu anafanyiwa visa vya hapa na pale kwa lengo la kumkwamisha asiende kuendelea na masomo yake au hata kama anaondoka basi asiweze kulipwa haki yake ya mshahara aliyokuwa akiidai.*

*Ninatoa wito kwetu sisi wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na hasa sisi Wachaga tumwogope Mungu, kwa maana tuachane na aina hii ya dhuluma ambayo baadhi ya wenzetu wamekuwa wakiifanya kwa muda mrefu sasa.*

*Ieleweke kuwa vijana hao huruhusiwa na wazazi ama walezi wao ili waje wajitafutie kipato cha kuwawezesha kujikimu katika kipindi wanachosubiri matokeo yao na tusitumie mwanya huo kuwadhulumu watoto hawa.*

***Deogratius Massawe-Rombo***

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU
mhariri@nipashe.co.tz

# Mabweni yana mchango kuepusha mimba hizi




Mabweni yanatakiwa kujengwa kwa ajili ya kuwaokoa wanafunzi kama hawa dhidi ya mimba za utotoni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

**KUTEMBEA** umbali mrefu kufuata elimu na pia baadhi ya wanafunzi kupanga nyumba za mitaani ni miongoni mwa sababu, ambazo hutajwa kuchangia kuwapo tatizo la mimba kwa wanafunzi hasa wa sekondari.

Kutokana na hali hiyo, serikali ilishaziagiza halmashauri kote nchini kuwa na mpango mkakati wa kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya bajeti ya ujenzi wa mabweni ya watoto wa kike ili kuwaepusha na tatizo hilo.

Uhaba wa shule za sekondari katika baadhi ya kata na ukosefu wa mabweni vinadaiwa kuwafanya wanafunzi kukumbana na vishawishi na wakati mwingine kuwa huru kujiamulia mambo yao.

Kuwa huru na kujiamulia mambo yao wenyewe husababisha baadhi yao kupachikwa mimba na hata wakati mwingine kukumbwa na magonjwa ya zinaa, ambayo ni hatari kwa afya zao.

Hatua ya serikali kuziagiza halmashauri kuwa na mikakati ya ujenzi wa mabweni, ni kujali na kutambua kwamba bila mabweni hali inaweza kuendelea kuwa mbaya kwa wanafunzi wa kike.

Kimsingi ukosefu wa mabweni unazikumba sekondari nyingi za kata nchini, na kwa kutambua changamoto hiyo, baadhi ya wazazi hapa nchini wameanza mikakati ya ujenzi wa mabweni hayo ili kumnusuru mtoto wa kike.

Wakazi wa Musoma Vijijini ni miongoni mwa wazazi waliochukua hatua ili kunusuru mtoto wa kike dhidi ya mimba kwa kujitolea kujenga mabweni na kuongeza sekondari za vijiji ili watoto wao wasome katika shule za karibu.

**Katika kufanikisha ujenzi wa sekondari za vijiji na mabweni, wamekuwa wakichangia nguvu zao kwa kusomba mawe, maji, mchango na hata kuuza mifugo ili kuhakikisha lengo kuwaokoa watoto wa kike linatimia.**

Kata za Ifulifu na Nyakatende, Nyegina na Nyamrandirira ambazo ni mfano mmojawapo, sasa wakazi wake wanajenga sekondari za vijiji baada ya zile za kata, lengo likiwa ni kuwapunguzia watoto wao kutembea umbali mrefu.

Wakati kukiwa na ujenzi wa sekondari za vijiji, kwenye maeneo mengine ya Musoma Vijijini kuna ujenzi wa mabweni, huku lengo likiwa ni hilo la kuwaondolea changamoto wanafunzi wa kike.

Wakazi wa Musoma Vijijini hawakusubiri halmashauri yao kutenga fedha, bali wamehamasishwa na wadau wa elimu akiwamo mbunge wao, Profesa Sospeter Muhongo na kuitikia wito.

Katika kufanikisha ujenzi wa sekondari za vijiji na mabweni, wamekuwa wakichangia nguvu zao kwa kusomba mawe, maji, mchango na hata kuuza mifugo ili kuhakikisha lengo kuwaokoa watoto wa kike linatimia.

Wanatambua kuwa mimba za watoto shuleni ni jambo la aibu ndio maana wazazi wameamua kuchukua hatua ya kujenga mabweni na hata kuongeza sekondari za vijiji ili kuhakikisha wanafunzi wa kike wanakuwa salama.

Mjadala huu unaamini kwamba suala la kujenga mabweni halipaswi kuwa la hiyari, wazazi ambao bado hawajaona umuhimu huo washurutishwe ili waige mfano kwa wenzao wa Musoma Vijijini, ambao wameamua kufanya kweli.

Hatua waliochukua ikikamilika itawaepusha watoto wao dhidi ya vishawishi vya watu mbalimbali wakiwamo madereva wa bodaboda wanaodaiwa kutumia changamoto za umbali wa shule na mabweni kujinufaisha.

Ujenzi wa sekondari za vijiji unaweza kusaidia wanafunzi kusoma karibu na nyumbani kwao.

Aidha, ujenzi wa mabweni utasaidia wanafunzi kuachana na mtindo wa kupanga kwenye nyumba za mitaani.

Mazingira hayo mawili ya kupanga uraiani na kutembea umbali mrefu kwenda shule, kimsingi si salama kwa mtoto wa kike, hasa kutokana na ukweli kwamba ni rahisi kukutana na vishawishi vingi.

Wakati serikali ikihimiza ujenzi wa mabweni, wazazi na walezi wa Musoma Vijijini, wao wameamua kupiga hatua moja zaidi ambayo mbali na ujenzi wa mabweni wanaona kuna haja ya kuwa na sekondari za vijiji.

Mjadala huu unaamini kwamba mfano huo unafaa kuigwa kwani hatua zinazochukuliwa zinaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kumwokoa mtoto wa kike kwenye mtego wa kupata mimba bila kutarajia.

Wataalamu wa afya wanasema mimba za utotoni husababisha matatizo ya muda mrefu ya kiafya na kijamii na hata wakati mwingine vifo vinavyohusiana na uzazi.

Hivyo uwekezaji zaidi katika elimu kwa mtoto wa kike ni muhimu ili kutokomeza matatizo hayo na hatua mojawapo ni hiyo waliochukua wakazi wa Musoma Vijijini mkoani Mara.

Wanatambua kwamba elimu ni haki za mtoto wa kike, kwa kuwa mtoto wa kike asiye na elimu itamwia vigumu kupata ajira na kujijengea maisha bora na familia yake.

# DPP afunguka masharti

INATOKA UK. 2

nao namna ya kuzirudisha fedha walizotakatisha, lakini haya ni mapendekezo, sijaingilia mahakama, ninapendekeza kama kiongozi. Na wasipofanya hivyo ndani ya siku saba, endeleeni kuwabana."

**WADAU WANENA**

SIKU moja baada ya Rais Magufuli kumwagiza DPP kuwasikiliza watuhumiwa wa makosa ya uhujumu uchumi ikiwezekana wasamehewe, wadau wamepongeza na wengine kutoa ushauri wa kisheria.

Wakitoa maoni yao kwa nyakati tofauti, wadau mbalimbali walimpongeza Rais Magufuli kuwa ameonyesha namna msamaha unavyotakiwa kutolewa kwa aliyekiri kosa.

Sheikh Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema kitendo cha Rais Magufuli kumtaka DPP kuwasikiliza watuhumiwa wa uhujumu uchumi na ikiwezekana kuwasamehe, ni jambo zuri ambalo limelenga kuonyesha namna msamaha unavyotakiwa kuwa.

"Hili ni jambo nzuri Rais Magufuli ameonyesha uzalendo, ameonyesha kujali wananchi wake, ameonyesha upendo mkubwa kwa wale anaowaongoza.

"Watu wanapokiri makosa yao wanastahili msamaha, ukifanya kosa na kutubu Mungu anakusamehe, hata kibinadamu mtu anapofanya kosa na kukiri kosa anastahili msamaha, anachofanya Rais Magufuli kwa tafsiri nyingine ni kwamba anafanya jambo la kijasiri na kiimani," alisema.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRD), Onesmo Olengurumwa, alisema maagizo hayo yanaweza kuwa na utata ama kutokua kwa sababu inategemea itakavyokwenda.

"Maagizo haya yana changamoto yake kwa watu wanaojua sheria kwa sababu DPP ana uwezo wa kufuta kesi yoyote ambayo haina ushahidi. Maagizo haya ni kama amemtaka DPP aende kuongea na watuhumiwa ili walipe fedha walizotakatisha au wafanye majadiliano kitu ambacho tukirudi kwenye sheria ni changamoto.

"Kama mtu alikiri kosa na kesi ipo mahakamani DPP hawezi kufuta kesi hiyo. Nini basi kifanyike, turudi kwenye mfumo wa makosa ya jinai na kutoruhusu kukamata watu ambao bado uchunguzi wa kosa haujakamilika ili ukimkamata uwe na ushahidi wa kujitosheleza," alisema.

Olengurumwa alisema asilimia 60 ya kesi ya uhujumu uchumi mara nyingi zinakuja kuonekana hazina ushahidi wakati watuhumiwa tayari wakiwa wamekaa miaka mitano mahabusu.

"Uchunguzi unafanyika miaka mitatu au minne, tunashauri hawa watu wasikamatwe kwanza wafanye uchunguzi angalau ukifika asilimia 50 ndipo wakamatwe ili kesi ziendelee," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema kosa la uhujumu uchumi ni la jinai siyo la madai ambalo linaweza kuomba msamaha.

Henga alishauri wakati wa utekelezaji wa maagizo ya Rais Magufuli DDP ahakikishe kesi za uhujumu uchumi zinakwenda haraka na mshtakiwa akikutwa na hatia mahakama itachukua hatua ya mhusika kulipa faini au kwenda jela.



Washtakiwa Evans Aveva na Geofrey Nyange (Kaburu) na Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Simba, Zacharia Hans Poppe, wakitoka katika Mahakama ya Kisutu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili kuahirishwa hadi Septemba 27 mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maagizo JPM Coco pasua kichwa

INATOKA UK.4

daraja jipya la Selander, litakaloanzia ufukwe wa Coco Beach (Oysterbay) kwenda Hospitali ya Aga Khan.

Hata hivyo, jana Nipashe ilipomtafuta Mkurugenzi wa Manispaa, Aron Kagurumjuli, ili kujua nini kinachoendelea baada ya maagizo ya Rais, alijibu kwa kifupi: "Siwezi kuyajadili maagizo ya Rais."

Juzi, Rais Magufuli alisema mkandarasi alipopewa zabuni ya kujenga eneo hilo ndiye aliyeshindwa kujenga soko la Mwanjelwa mkoani Mbeya.

"Sasa sijui wakishajenga hiyo ghorofa lao, halafu ujenzi wa barabara nne utakapoanza sijui watalibomoa hilo jengo lao?" Zitapita wapi?" Unapojenga wachuuzi wa eneo lile watakwenda wapi?" Wata survive (kuishi) namna gani?" Alihoji Rais na kuongeza:

"Inaumiza sana tunapopewa madaraka halafu tunajisahau, Coco Beach haiwezi kujengwa kwa Sh. bilioni 14, unajenga lighorofa la nini?" Nendeni beach (fukwe) zingine mkaone zinavyojengwa."

Akizindua kiwanda cha kutengeneza mabomba Vingunguti jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Rais Magufuli alionyesha kukerwa na baadhi ya viongozi ambao hawasimamii na kuchukua maamuzi utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwamo uendelezaji wa ufukwe huo.

Alisema baadhi ya miradi inayocheleweshwa ni kiwanda cha machinjio Vingunguti na ufukwe wa Coco.

Baada ya kauli hiyo, kesho yake, Meya wa Kinondoni, Benjamin Sitta, akiwa na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Kagurumjuli, walifika kwenye ufukwe huo na kutangaza rasmi kuwa Coco kunafungwa kwa muda kupisha ujenzi uliolenga kupaendeleza ili uwe wa kisasa.

Sitta aliwaeleza wanahabari kuwa ufukwe huo umefungwa kwa muda kupisha ujenzi ambao utachukua miezi sita kuanzia sasa na utagharimu Sh. bilioni 13.6.

"Tutafunga mpaka kule wanakouza mihogo, wanaouza mihogo wameshapewa notisi ili watafute sehemu nyingine, tutafunga eneo hili lote kwa mabati ili makandarasi wafanye kazi bila kuleta matatizo, mkiona ufukwe umefungwa ni kwa maslahi mapana manispaa na mkoa wetu," alisema.

Alisema awali waliomba Sh. bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi huo lakini baada ya mazungumzo na mkandarasi imeshuka hadi Sh. bilioni 13.6.

"Ninaishukuru timu ya wataalamu na makandarasi wameonyesha uzalendo, tutahakikisha tunapata ufukwe wa kimataifa ili watu wakija kupumzika wapate madhari kama ya Afrika Kusini au Uingereza na kwingine," alisema.

Alisema mradi huo ni wa pili ambao Manispaa inautekeleza sambamba na ujenzi wa soko la Tandale ambapo taratibu za kisheria zote zimefuatwa.

Kagurumjuli, alisema kwa upande wa manunuzi hawakuruka hata kipengele kimoja, hivyo kwenye eneo hilo wapo salama.

Alisema mkandarasi anayeliendeleza eneo hilo ataifanya shughuli hiyo kwa miezi sita na kuikabidhi.

# Vigingi saba RC

INATOKA UK. 2

Viwanda vingi vilivyokuwapo miaka ya 1980 na 1990 vimekufa na vingine vinasuasua.

Katika hotuba yake ya juzi, Rais Magufuli alisema hata wawekezaji wa Kiwanda cha Tumbaku wanataka kukimbia na kukifunga kiwanda hicho. Sanare anapaswa kujipanga kuhakikisha changamoto zinazokwamisha uwekezaji zinatatuliwa.

**SEKTA YA AFYA**

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, Dk. Kebwe alishindwa kusimamia ujenzi wa vituo vya afya katika Mkoa wa Morogoro.

Sanare anapaswa kujipanga kuhakikisha anatekeleza mpango wa serikali wa kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na hospitali ya wilaya kila wilaya.

"Nataka pia ukatatue migogoro ya halmashauri, baadhi ya wakurugenzi wanachangisha fedha kwa ajili ya kupeleka makao makuu ndiyo maana baadhi ya miradi haiendi. Unapeleka Sh. bilioni tatu za kujenga Hospitali ya Wilaya zinakaa miezi hata jengo halijajengwa," Rais alisema.

**AJALI**

Morogoro ni miongoni mwa mikoa yenye ajali nyingi za barabarani. Wakati Watanzania wakiendelea kuomboleza vifo vya zaidi ya watu 100 kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea Agosti 10, mwaka huu, Sanare anapaswa kuhakikisha anashirikiana vyema na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kukabiliana na ajali za barabarani.

**DARAJA KILOMBERO**

Sanare pia anapaswa kutatua changamoto za kukatika kwa mawasiliano ya barabara kipindi cha masika kati ya Mkoa wa Morogoro na Dodoma kutokana na maji kufurika kwenye Daraja la Kilombero.

# Ajali ya ndege ndogo yaua

INATOKA UK. 2

Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA)," ilielezwa katika taarifa ya TCAA.

Msimamizi wa Ndege ya Auric, Peter Kimaro, alisema baada ya ndege hiyo kuruhusiwa, ilipaa lakini haikunyooka na badala yake ilikunja kona kisha kuanguka na kusababisha vifo vya watu wawili waliokuwamo ndani yake.

Akizungumza na gazeti hili kwa simu jana mchana, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Vallery Chamlungu, alisema wametuma wataalamu kufanya uchunguzi eneo la tukio.

**AJALI 3 MIEZI 2**

Agosti mwaka huu, zilitokea ajali mbili za ndege ndogo; ya kwanza ikitokea katika Kijiji cha Mahompa, Kata ya Igigwa wilayani Sikonge mkoani Tabora.

Ndege hiyo yenye namba za usajili ZU-TAF, aina ya Sling Aircraft ilisababisha vifo vya rubani na msaidizi wake, wote raia wa Afrika Kusini. Siku nne baadaye, ndege ya Kampuni ya Tropical Air yenye namba za usajili 5H-NOW, ikitokea Mafia kwenda Dar es Saalam, ilianguka sekunde chache baada ya kuondoka Uwanja wa Ndege wa Mafia na kusababisha kujeruhiwa kwa watu wanne.

Abiria wengine wa ndege hiyo walitoka wakiwa salama, lakini ndege hiyo iliwaka moto baadaye na hadi sasa chanzo cha ajali hiyo hakijafahamika.

# Serikali yawashtukia watumishi ardhi

**Na Futuna Seleman, KIBAHA**

SERIKALI imekiri baadhi ya mashamba ya wananchi wa Mlandizi na Kibaha mkoani Pwani yalifutwa umiliki kimakosa kutokana na baadhi ya watendaji kushindwa kutimiza majukumu yao ipasavyo na kutoa taarifa zisizo sahihi juu ya mashamba hayo kwa mamlaka husika.

Kutokana na hali hiyo, serikali imesema kuwa taarifa zilizotolewa zilikuwa kinyume kwa kuwa yalikuwa yameendelezwa.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, Angelina Mabula, ndiye aliyebainisha ukweli huo katika ziara yake maalum kupitia maeneo ya mashamba 12 kujiridhisha, hivyo kubaini sita yaliendelezwa.

Miongoni mwa mashamba hayo ni la miti ya mitiki, lingine minazi, michungwa, huku manne hayajaendelezwa likiwamo la mwanamke mzee pamoja na la Disunyara ambalo aliliuza na ndani yake familia tatu zimekwishajenga.

"Tumeona ni vema kusikiliza kilio ili haki itendeke, tulichoona wananchi wameonewa mashamba mawili yana miti ya miembe, michungwa lingine mitiki na lingine liliendelezwa kwa maombi waliyokuwa nayo watumishi na mwingine aliomba mabadiliko ya matumizi ya eneo ingawa kosa lake lilikuwa ni kusalender (kukubali) kuomba matumizi mengine ya eneo lake, lakini utaratibu wote aliufuata lakini mtumishi wa serikali akaendelea kuomba utaratibu wa kulifuta," alisema Mabula.

"Ninachosema haki katika ufutaji wa mashamba haikutendeka, watu wamefanya kazi wakiwa ofisini hawakufika 'sight' kuona mwendelezo, wananchi walikuwa na haki ya kulalamika kupata haki zao... nami nimejiridhisha kuona uhalisia wa maeneo yao taratibu za kiofisi zitafanyika kama ambavyo utaratibu wa kufuta ulifanyika," aliongeza.

Katika maeneo yaliyokiuka utaratibu, Mabula alielekeza halmashauri kuendelea na utaratibu ambao upo na unaokubalika katika kuyapanga upya maeneo na kipaumbele wapewe walioweka makazi kwa sababu wengine walishavamia maeneo na wamejenga, hivyo serikali haiwezi kuwaondoa kwa kuwa kuna familia ambazo zitalazimika kujipanga upya.

"Waliovamia kwa vile washajenga utaratibu wa kawaida ufanyike walipie gharama za upimaji hilo ndio kubwa ambalo nasema serikali inasema kwa waliovunja sheria kwa kuwa kila kitu kinakwenda kwa utaratibu," alisema zaidi.

Alisema kitendo kilichofanywa na watumishi waliopewa dhamana na serikali kuwatumikia wananchi kinaitia hasara serikali kwani ardhi iliyothaminishwa na mali za wananchi fidia yake ni kubwa na serikali inaingia hasara kubwa kwa kuwa kote walipopita wameliona hilo.

"Serikali inahakikisha haki ya kila mtu inapatikana na inatendeka na hakuna dhuluma inafanyika kwa mtu aliyetumia jasho lake na akazingatia taratibu zote kisheria," alimalizia Mabula.

Baadhi ya wananchi Mlandizi mkoani Pwani walimshukuru Rais Magufuli kwa kusikiliza kilio cha wananchi wanyonge wakisema uamuzi wake umelenga kutetea haki za wanyonge kwa vile baadhi ya watumishi wasio waadilifu wanaonea wananchi.



Ofisa programu katika Idara ya Maarifa, Utafiti na Uchambuzi wa TGNP Mtandao, Maureen Mboka, akiwaelezea washiriki wa mafunzo ya kila Jumatano kuhusu maandalizi ya tamasha la kijinsia na jubilee ya miaka 25 ya mtandao huo, litakalofanyika kesho kwenye viwanja vya makao makuu ya TGNP, Mabibo Dar es Salaam. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Misikiti ilivyosaidia kupunguza mila potofu

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

UWAPO wa misikiti katika maeneo mbalimbali wilayani Kahama mkoani Shinyanga kumesaidia kwa kiasi kikubwa kubadilisha imani potofu katika jamii ikiwamo mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino.

Hayo yameelezwa jana na Sheikh Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Omary Damka, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa msikiti mpya wa Masjid Ikhilas uliopo eneo la Mbulu Misheni uliojengwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Istikama Islamia ya Oman.

Sheikh Damka alisema kuwapo kwa misikiti imesaidia kwa kiasi kikubwa kubadilisha tabia ya watu kwa kuwa mafundisho yanayotolewa yamesaidia kufikisha ujumbe ulioleta mabadiliko katika jamii.

Sheikh Damka alitoa wito kwa Waislamu wote wilayani Kahama kujitokeza kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili kupata nafasi ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Awali akiwataja maimamu watakaosimamia msikiti huo na majukumu yao, Mwenyekiti wa Mawakala wa Jumuiya ya Istikama tul Islamia, Ahmed Alnubi, aliwataka maimamu hao kufanya kazi kwa ushirikiano na kuitumikia jamii.

Kwa upande wao Waislamu waishio eneo la Mbulu Misheni waliishukuru jumuiya ya Istikama Islamia ya nchini Oman kwa ujenzi wa msikiti huo, hali itakayowasaidia kupunguza umbali mrefu wa kufuata huduma za ibada mbali na makazi yao.

# RC aeleza watumishi cha kufanya kabla ya kustaafu

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara amewataka watumishi wa serikali kutokuwa na woga wa kumiliki ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwamo kujenga makazi bora ya kuishi pamoja na uwekezaji wa miradi ya kiuchumi isipokuwa wasivunje sheria ya nchi.

Wito huo ulitolewa wilayani Masasi na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alipokuwa akizungumza na watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Masasi, madiwani, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na watendaji wa taasisi za kiserikali.

Byakanwa alisema kitendo cha kusubiri kustaafu ndipo kuanza kujenga makazi ya kuishi au kufanya uwekezaji wa aina yoyote kwa mtumishi sio sahihi bali uwekezaji lazima mtumishi afanye wakati bado yupo kazini.

Alisema wapo baadhi ya watumishi mkoani humo ambao wamekuwa wakichelewa kufanya shughuli za kiuchumi au kujenga nyumba bora za kuishi kwa kisingizio kuwa wao si wazawa wa eneo wanalofanyia kazi.

Alisema kusubiri kuhamishwa au kustaafu kazi ndipo kufanya shughuli za kimaendeleo ni kuchelewa kujiletea maendeleo kwa mtumishi.

Alisema kila mtumishi ana haki ya kumiliki ardhi kuanzisha miradi ya kimaendeleo ilmradi sheria ya nchi isivunjwe, hivyo watumishi waangalie fursa zilizopo kwenye maeneo yao na kuzitumia katika kujiletea maendeleo.

"Kuna watumishi hawataki kufanya uwekezaji au kujenga nyumba za kuishi kwenye wilaya wanazofanyia kazi eti kwa vile watahamishwa na pia sio wazawa wa maeneo haya hii sio sababu ya msingi tuwekeze sasa kabla ya kustaafu," alisema Byakanwa.

Alisema watumishi lazima watafakari kwa kina juu ya maisha yao ya baadaye kuanzia sasa wakati wapo kazini kwa kuwekeza vitega uchumi mbalimbali ambavyo pale wakiondoka kazini wasihangaike tena kupigania maisha yao.

Byakanwa alisema leo hii watumishi wanapata kipato kupitia mishahara yao, hivyo hicho wanachopata wafanyie mambo ya msingi ikiwamo kuanzisha biashara na kuwa na makazi bora ya kuishi.

Alisema Mkoa wa Mtwara una fursa nyingi za kimaendeleo kama watumishi wakizitumia vema wanaouwezo wa kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo na mkoa pia kunufaika.

# Sababu BoT kutoza benki tano faini ya bil. 1.8/-

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imezitoza faini ya Sh. bilioni 1.88 benki tano za biashara zilizokiuka kanuni za kuzuia utakatishaji wa fedha haramu.

Benki hizo na kiwango cha fedha zilizotozwa kila moja ni African Banking Corporation (T) Limited (145), Equity Bank (Tanzania) Limited (580), I&M Bank Limited (655), UBL Bank (T) Limited (325) na Habib African Bank Limited (174).

Taarifa iliyotolewa jana na BoT, ilieleza kuwa benki hizo zimekiuka kanuni namba 17, 22 na 28 za Kanuni za Kuzuia Utakatishwaji wa Fedha Haramu za mwaka 2012 kwa kushindwa kuhakiki taarifa za utambulisho wa wateja na kushindwa kuwasilisha taarifa ya miamala yenye kuleta mashaka katika Kitengo cha Kuzuia Fedha Haramu (FIU).

Aidha, pamoja na faini hizo, BoT imezipa miezi mitatu imezitaka toka tarehe faini zilipotozwa kutekeleza masharti yaliyoelekezwa kwao.

Taarifa hiyo iliyataja masharti hayo ni kupitia upya taarifa za wateja wao na kuhakikisha kwamba zinakidhi matakwa ya kisheria na kanuni zilizopo za uhakiki wa utambulisho wa wateja.

Mengine ni kuwasilisha taarifa ya miamala yenye kuleta mashaka ambayo ilitakiwa kuwasilishwa FIU, kufanya tathmini ya ubora wa mifumo ya ndani ya kibenki na kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa mifumo hiyo ipo madhubuti kwa lengo la kukinga mapungufu hayo hayajirudii tena.

Aidha, benki hizo zimetakiwa kuwachukulia hatua stahili za kinidhamu, wafanyakazi wote waliohusika kufanikisha ufunguaji wa akaunti za amana kinyume na kanuni za kumtambua mteja.

"Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuzikumbusha benki na taasisi za fedha kuhakikisha kuwa zinafuata sheria na kanuni zilizopo nyakati zote," alisema taarifa hiyo.




Watoto wanaoishi katika mazingira magumu wakicheza jirani na taa za kuongozea magari katika makutano ya Barabara ya Nelson Mandela na Bagamoyo, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: JOHN BADI**

## CRJE yafunguka tuhuma rushwa mshirika wake

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ujenzi ya CRJE ya China imesema tuhuma rushwa zinazohusu kampuni mshirika wake katika ujenzi wa barabara wilayani Temeke, SEGA Y Engineering and Construction Company Limited hazihusu kampuni hiyo.

"Kampuni ya CRJE haijihusishi kwa namna yoyote na vitendo vya rushwa na imesikitishwa sana na kitendo cha kampuni mshirika wake kuhusishwa na tuhuma hizo," taarifa hiyo ilisema na kusisitiza kwamba madai ya vibarua wa kampuni mshirika ni ya kweli na kwamba yanashughulikiwa.

Katika taarifa yake hiyo, kampuni hiyo ya Kichina ilisema Septemba 17, mwezi huu, wawakilishi wake pamoja na wale wa kampuni mshirika ya SEGA Y walikutana na viongozi wa serikali mkoa wa Dar es Salaam kujadili suala hilo na kufikia mwafaka wa kutekeleza madai yote ifikapo Oktoba.

Taarifa hiyo ilisema CRJE inafanya kazi na kampuni hiyo ya Kitanzania ili kuzipa uwezo kampuni za ndani kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara siku za baadaye, na kwamba kama mkandarasi mkuu wa ujenzi wa barabara za mtaani katika Wilaya ya Temeke inahusika na udhibiti wa mradi mzima pamoja na yadi ya vifaa na magari kwenye saiti ambayo SEGA inahusika.

"Jambo la kutekeleza madai ya msingi ya vibarua limeshaanza ikiwamo kulipa kiwango cha serikali cha Sh. 12,500 kwa siku kwa wale waliokuwa chini ya kiwango na pia mchakato wa kulipa mapunjo ya nyuma unaendelea," taarifa hiyo ilisema.

# Waziri ataka tawi BoT mkoani kwake

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu, ameiomba serikali iweke tawi la Benki Kuu (BoT) mkoani Geita kutokana na matumizi makubwa ya pesa yatokanayo na biashara ya madini ya dhahabu.

Amesema biashara ya madini imechagiza ukuaji wa uchumi hali iliyosababisha kuwa na uhaba wa fedha katika mkoa huo.

Mbunge huyo ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alitoa ombi hilo mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati alipopewa nafasi ya kuwasalimia wananchi wa jimbo lake la Geita Mjini kabla ya Waziri Mkuu kufungua maonyesho ya madini mkoani humo.

Alisema mji wa Geita kwa sasa tangu sheria za madini zilipobadilishwa kumekuwa na matumizi makubwa sana ya fedha kutokana na ununuzi wa madini ya dhahabu, hivyo wanahitaji tawi la BoT ili kurahisisha upatikanaji wa fedha hizo.

Alisema tatizo hilo limekuwa kero kwa muda mrefu si kwa wanunuzi pekee wa madini bali hata kwa wanunuzi wa zao la pamba.

"Waziri Mkuu, umeshuhudia kule wilayani Chato wanunuzi wa zao la pamba wameshindwa kuwalipa wakulima kutokana na uhaba fedha, benki tulizonazo zina uhaba wa fedha," alisisitiza Kanyasu.

Kanyasu alimweleza Majaliwa kuwa benki zilizopo katika mkoa huo zinapoagiza fedha kutoka tawi la BoT lililopo jijini Mwanza huchukua zaidi ya siku mbili hadi ziweze kuwafikia, hali hiyo inawachelewesha kimaendeleo.

"Ikikupendeza Waziri Mkuu tunaomba tupatiwe tawi la BOT kama ilivyo mkoani Shinyanga ili kurahisisha upatikanaji wa fedha," alisisitiza Kanyasu.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliiomba serikali ibadilishe mji huo wa Geita kuwa manispaa kutokana na kukamilisha taratibu zote zinazotakiwa.

Amesema kutokana na mabadiliko hayo kama yataridhiwa mzunguko wa pesa utakuwa mkubwa kuliko hivi sasa, hivyo wana Geita wanahitaji sana uwepo wa tawi la BoT ili kujiletea maendeleo kwa kasi ya serikali.

# Waaswa kupambana na mimba za utotoni

Na Cynthia Mwilolezi, SIMANJIRO

WANASIMANJIRO mkoani Manyara, wametakiwa kupambana na tatizo la mimba za utotoni, kwa kuwasomesha watoto wa kike na si kuwaozesha wakiwa wadogo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, Asia Ngalisoni, aliyasema hayo juzi, kwenye mahafali ya nane ya darasa la saba ya shule ya awali na msingi New Light ya mji mdogo wa Mirerani.

Ngalisoni alisema wananchi wa wilaya hiyo, wanatakiwa kupambana na tatizo hilo, kwani baadhi ya watoto wa kike wanaachishwa masomo na wazazi na walezi wao, ili kuozeshwa wakiwa wadogo kwa tamaa ya mali.

Alisema tatizo la mimba za utotoni linaweza kukomeshwa, kwa ushirikiano wa wazazi na walimu, kwani mtoto akikatishwa masomo watoe taarifa sehemu husika.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Silvanus Tairo, aliwataka wananchi hao kusomesha watoto wao, kwani kuna baadhi ya shule wanafunzi hawahitimu hata darasa la saba.

Tairo alitoa mfano wa Shule ya Msingi Lerumo, ilikuwa na wanafunzi 20 walioanza darasa la kwanza na mwaka jana waliandikisha kufanya mtihani wa darasa la saba walikuwa sita tu na ilipofika siku ya kufanya mtihani walipungua na kubaki watatu waliofanya mtihani huo.

Mkurugenzi wa shule hiyo Mchungaji Sommy Severua, alisema elimu ina nguvu mno kwani inaweza kusababisha mtoto wa maskini kuwa daktari bingwa.

"Mtoto wa mlalahoi anaweza kuwa bosi kutokana na ukubwa wa elimu aliyonayo, hivyo tunapaswa kuzingatia hilo kwa kuwapatia elimu watoto wetu," alisema Mchungaji Severua.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya New Light, Tumaini Mbise, alisema wanafanya vyema kitaaluma, kwani mwaka jana katika mtihani wa darasa la saba, walishika nafasi ya kwanza kiwilaya na nafasi ya sita kimkoa.

**"Mtoto wa mlalahoi anaweza kuwa bosi kutokana na ukubwa wa elimu aliyonayo, hivyo tunapaswa kuzingatia hilo kwa kuwapatia elimu watoto wetu," alisema Mchungaji Severua.**

# 500 waula Ngorongoro

Na Zanura Mollel, NGORONGORO

VIJANA zaidi ya 500 wamenufaika na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ngorongoro, baada ya kupata ajira zilizoboresha maisha yao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Matthew Siloma, wakati alipokuwa kwenye ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa hospitali hiyo pamoja na Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia ambaye ni Mbunge wa Jimbo hilo, William Ole Nasha.

Siloma alisema wilaya hiyo ina vijiji 65, kata 28 na tarafa tatu na wamekubaliana wananchi kuchangia ujenzi wa hospitali hiyo kwa kutoa Sh. 2,000,000 kwa kila kijiji na pia kuwapa ajira vijana wao.

"Kila kijiji kinatoa fedha hizo na tangu tuanze mpango huu wa kuchangia tayari tumepata Sh. milioni 12, hivyo tunaendelea kuhamasisha wananchi wamalizie michango hiyo kwa wakati ili hospitali yetu imalizike kwa muda uliopangwa na ituhudumie," alisema Siloma na kuongeza kuwa na pia vijana wapate kazi.

Aidha, alishukuru juhudi wa mbunge wao William Ole Nasha kwa kufanikisha upatikanaji wa miradi mbalimbali, jimboni humo na kuinua kiuchumi wananchi wake.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ole Nasha, alisema kwa miaka minne ya awamu ya tano, wilaya hiyo imenufaika na kupata miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa hospitali ya wilaya, barabara kwa kiwango cha lami pamoja na umeme.

Alisema katika mradi huo wa hospitali serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba, japo kunahitajika majengo 22.

Aliongeza kuwa serikali imeona vyema kuanza na majengo haya saba kwa hatua za awali. "Majengo yanayohitajika ni 22, lakini kwa sasa kupitia hizi fedha tulizopata zitakamilisha majengo saba, ambayo yatatoa huduma zote muhimu za matibabu ila imeahidi kuwa itaendelea kukamilisha kwa awamu hadi majengo yote 22 yakamilike," alisema Ole Nasha.

Aidha, alisema uwepo wa hospitali hiyo utasaidia upatikanaji wa huduma za afya kwa jamii, kwani hapo awali wagonjwa walikuwa wakisafiri kufuata matibabu nchi jirani ya Kenya na wakati mwingine kusafiri zaidi ya kilomita 400 kutibiwa mkoani Arusha.

"Si jambo la kujivunia kufuata matibabu nje ya nchi au zaidi ya kilometa 40, hatua za ujenzi zipo mwishoni, miradi mingi inakwama katika hatua za mwisho. Nitoe rai simamieni ipasavyo ili iweze kukamilika kwa wakati," alisema Ole Nasha.

Pia alipongeza kamati mbalimbali zinazosimamia miradi hiyo ikiwamo ya ujenzi wa shule mpya 13 na kuwasihi kukamilisha jukumu hilo kwa wakati.



Ofisa madini mkazi mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima (kulia), akizungumza na wawekezaji wa China wanaotarajiwa kuchimba madini ya Graphite Mji Mdogo wa Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waomba serikali kudhibiti viuatilifu

Na Woinde Shizza, ARUSHA

MTANDAO wa vikundi vya wakulima nchini (MVIWATA), umeiomba serikali kuingilia kati na kudhibiti uingizwaji holela wa viuatilifu duni ili kumaliza tatizo la kuzagaa dawa feki za kuua wadudu.

Viuatilifu hivyo vinavyoshindwa kuua wadudu waharibifu wa mimea ya wakulima na kusababisha hasara.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Mviwata, Mkoa wa Arusha, Mchungaji John Safari, katika mkutano mkuu wa saba wa wanachama wa Mviwata, uliofanyika jijini hapa.

Alisema kuwa wakulima wengi nchini wamekumbwa na adha ya mazao yao kushambuliwa na wadudu, kiasi cha kukosa mavuno kutokana na dawa zinazoingizwa nchini, kutokuwa na uwezo wa kuua wadudu waharibifu.

"Kwa hiyo tunaiomba serikali kupeleka wataalamu wa kilimo vijijini, ili kufanya utafiti wa baadhi ya wadudu wasiosikia dawa na kupata dawa zenye uwezo wa kuuangamiza, lakini pia watusaidie kudhibiti viuatilifu feki vinavyoingia kinyemela nchini," alisema Safari.

Alisema, changamoto kubwa kwa wakulima ni jinsi ya kupata dawa za kuua wadudu kwenye mazao yao, kwani kwa sasa wadudu wamekuwa sugu, hawasikii dawa na hujikuta dawa wanazonunua zinawapa hasara kila mwaka.

Mwenyekiti wa Mviwata Taifa, Abdul Gear, aliishauri serikali kutoa watafiti wa kutosha, ili kubaini uwezo wa wadudu wanaoshambulia mazao yao, hasa mahindi na kutafuta viuatilifu vyenye uwezo wa kuwaangamiza.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema serikali inatafuta njia za kutatua changamoto zinazowakabili wakulima, husussani wanachama wa Mviwata ili kuboresha kilimo.

"Lakini si kujipanga tu bali hata suala la upatikanaji wa mbolea na pembejeo zingine nalo serikali tunalipa kipaumbele, hivyo msiwe na mashaka na serikali yenu," alisema.

Akiongelea suala la viuatilifu alisema kumekuwapo na tatizo la uelewa juu ya matumizi ya dawa za kuua wadudu kwa wakulima na hivyo kuchangia kushindwa kuangamiza wadudu.

Aliwataka maofisa ugani na wataalamu mbalimbali wa kilimo, kuhakikisha wanawatembelea wakulima na kuwapatia elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu.

# Waomba wakalimani mahakamani, polisi

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

CHAMA cha watu wenye ulemavu wa kusikia (Chavita), mkoani Kilimanjaro, kimeiomba serikali kuajiri wakalimani katika vitengo nyeti kama polisi, magerezani na mahakamani ili kuwapa msaada wanaokosa kutokana na tatizo la mawasiliano.

Waliomba Wizara ya Mambo ya Ndani, kuangalia namna ya kuajiri wakalimani katika kila kitengo kutoa msaada wanapofika katika taasisi hizo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki katika kongamano la uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya alama kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama na Mratibu wa Chavita Wilaya ya Hai, Pulcaria Aloyce.

Alisema watu wenye ulemavu wa kusikia wanakabiliwa na changamoto wanapofikia katika taasisi hizo bila kuwapo kwa mkalimani wanakosa haki zao kwa kushindwa kujieleza na kupatikana kwa ushahidi sahihi.

"Tunaiomba serikali kuangalia namna ya kuajiri mkalimani wa lugha za alama katika vyombo vya ulinzi na usalama ili waweze kupata tafsiri mara wanapofika katika vituo hivyo," alisema Aloyce.

Aidha, alisema wakati wa utoaji wa ajira tunaomba wawakumbuke watu wenye ulemavu ili kupatikana mkalimani mmoja katika kila halmashauri ili kurahisisha mawasiliano," alisema Pulcaria.

Akifungua kongamano hilo Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliyewakilishwa na Ofisa Tarafa ya Kata ya Masama, Nsajigwa Ndagile, alisema watu wenye ulemavu ni binadamu kama walivyo wengine na wanahitajika kupewa huduma zote kama walivyo raia wengine wote wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa sasa tutaishauri serikali kuangalia namna ya kuweka ajira za wakalimani katika kila wilaya lakini kwa sasa tunawaomba mwendelee kutoa mafunzo ya alama ili watendaji wa idara mbali mbali wapate mafunzo ya kuwezesha kuwahudumia watu wenye ulemavu," alisema Ndagile.

Kwa upande wao baadhi ya washiriki Inspekta wa Jeshi la Polisi katika wilaya hiyo, Zacharia Shabo, alisema mafunzo hayo yataweza kuwasaidia baadhi ya askari kufahamu lugha za alama.

Ufahamu huo utasaidia kuwahudumia watu wenye ulemavu wanapofika katika kituo hicho.

"Ni kweli wapo baadhi ya walemavu ambao wakifika katika kituo cha polisi unaanza kubuni ili kuwapa huduma, lakini kwa baadhi ya askari wetu kupata mafunzo kunaweza kusaidia mawasiliano kuwa rahisi zaidi," alisema.

Naiman Akyoo ni Mkaguzi Msaidizi wa Magereza kutoka Gereza la Karanga, aliiambia Nipashe kuwa licha ya kazi yao kuwahifadhi na kuwarekebisha mienendo ya wahalifu, changamoto ya mawasiliano hiyo ipo na mafunzo hayo yataleta mabadiliko.

Aidha, Hakimu wa Mahakama ya Bomang'ombe, Regina Samwel, alisema watu wenye ulemavu wamekuwa wakifika kutoa ushahidi katika mahakama hiyo na kuwataka waandike hali ambayo imekuwa ngumu kwao.

"Ambacho tumebaini kuwa watu hawa hawapendi kuambiwa waandike. Kutokana na kukosekana kwa wakalimani tunateseka kuwaelewa na wakati mwingine tunatumia nguvu kubwa ili kubaini nini alichotamani kukisema lakini ikiwa tutapata mafunzo haya ya alama, yatatusaidia kufanya kazi kwa uhakika bila kubaki na mashaka," alisema hakimu Regina.



Katibu wa Hamasa wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Manispaa ya Moshi, Hussein Msacky, akikata keki wakati wa kongamano la 'Soweto Mpya', lililofanywa na wanachama wa umoja huo katika Kata ya Soweto, Manispaa ya Moshi juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wasomi watakiwa kuuinua ushirika

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

VIJANA wasomi wameshauriwa kujiunga na vyama vya ushirika na kuviongoza na kuachana na mitazamo hasi, kuwa vyama hivyo ni vya wazee.

Pia wameshauriwa kuwa wanachama wa ushirika kutawaongeza nguvu ya kitaalamu na kufanikisha jitihada ya kuimarisha ushirika nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Joyce Mbwambo, wakati walipotembelea baadhi ya vyama vya ushirika katika Wilaya ya Hai.

Mhadhiri huyo alikuwa ameongozana na wanafunzi 60 wa chuo hicho ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo.

Mbwambo alisema vyama vingi vya ushirika hususani vyama vya msingi, vimekuwa vikiongozwa na wazee, huku vijana wasomi wakiwa mitaani.

Alisema kuna haja sasa kwa vijana hao kuamka na kuona kuwa vyama hivyo ni moja ya fursa kwao katika kupeleka elimu waliyoipata vyuoni na kuvisaidia kujiendesha kibiashara na kujikwamua kiuchumi.

"Ipo fikra mbaya juu ya vyama hivi vya ushirika, vijana wasomi wanaona hawawezi kufanya kazi kwenye vyama hivi kwa madai kuwa hakuna hela, lakini baadhi ya wazee wanafikiria kuwa vijana watakuwa wezi kwenye vyama vyao. Haya ni mawazo hasi ambayo hayapaswi kuendelezwa katika harakati hizi za kuvifufua vyama vya ushirika nchini," alisema Joyce.

Husein Omary ambaye ni miongoni mwa wanafunzi waliokuwa kwenye ziara hiyo, alisema bado kunahitajika elimu ya kina juu ya namna ya uendeshaji wa vyama vya ushirika na kubuni miradi ambayo itaviwezesha kujiendesha kwa faida.

"Vyama vingi vya ushirika havina hali nzuri. Katika kipindi hiki ambacho serikali imedhamiria kufufua ushirika nchini, maofisa ushirika wanapaswa kutoka maofisini, kwenda kwenye vyama hivi na kutoa elimu. Ni kwa sababu vingi vinayumba kutokana na kukosekana kwa elimu na utaalamu wa kuviendesha," alisema Omary.

Akizungumza zaidi kuhusu taasisi hizo, Mashaka Laurent, alisema katika harakati za kuvifufua vyama vya ushirika, ipo haja kwa serikali, kuyatazama masoko ya mazao na usimamizi wa vyama hivyo, kwa kuwa vyama vingi vimekuwa vikiyumba, kutokana na usimamizi mbovu na kukosekana kwa masoko ya uhakika.

# K'njaro kuchanja watoto 224,000

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

TAKRIBANI watoto 223,772 walio na umri kati ya miezi tisa hadi chini ya miaka mitano wa maeneo yote ya mkoa wa Kilimanjaro, wanatarajiwa kupatiwa chanjo ya surua, rubella na polio.

Chanjo hiyo inatolewa ili kuwakinga na magonjwa hayo pamoja na kuzuia kupooza. Hayo yalibainishwa jana na Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Kilimanjaro, Peter Kihamia, wakati akitoa elimu kwa waandishi wa habari mkoani hapa kuhusiana na kampeni ya chanjo hiyo.

Alisema kuwa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeanzisha kampeni maalum ya kutoa chanjo hiyo kwa lengo likiwa ni kutokomeza magonjwa hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakiwashambulia watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Kihamia alisema kuwa, kampeni hiyo ya kutoa chanjo kwa mkoa wa Kilimanjaro inatarajiwa kuanza wiki hii Septemba 26 hadi 30 na kwamba vituo 312 vitatoa huduma hiyo, huku makadirio yakiwa ni kuwafikia watoto 223,772.

"Tunatambua yapo maeneo ambayo vituo vya afya vipo mbali hali ambayo inawalazimu wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma hii ya chanjo kwa sasa tumekuja na huduma ya mkoba ambayo wataalamu wetu watakuwa wakienda katika maeneo ambayo yapo mbali na kituo ili kutoa huduma ya chanjo," alisema Kihamia. Aliwaambia wanahabari kuwa faida kubwa ya chanjo hii kwa watoto ni kuwakinga na magonjwa ya surua, rubella na ugonjwa wa kupooza jambo alilosema kuwa katika kipindi cha miaka mitano hakuna mtoto katika mkoa wa Kilimanjaro ambaye amethibitika kuwa na magonjwa hayo.

Kihamia alisema kuwa mtoto ambaye hatapata huduma hiyo ya chanjo madhara yake ni kuwa hatarini kupata maambukizi ya magonjwa hayo ambayo huleta vifo, endapo atacheleweshwa kupatiwa matibabu lakini pia anaweza kupooza baadhi ya viungo.

Kwa upande wake, Ofisa Afya Mkoa wa Kilimanjaro, Jonas Mcharo, alisema kuwa huduma hiyo ya chanjo hutolewa bila malipo na kuwataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka watoto kupatiwa chanjo kwani kinga ni bora kuliko tiba.

Aidha, aliwataka wazazi wanapoona mtoto amepata ulemavu wa viungo vya mwili ghafla kumwahisha hospitalini kufanyiwa uchunguzi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 24, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 15



## Vipaji vinaposhindana na vipaumbele, kipi kitangulie?

Ukurasa 18



## JE, WAJUA?

Kazi unayofanya kiukweli inakuua polepole?



Ukurasa 14

ELIMU KUTOKA POLISI

## IGP Sirro apokea uwanja wa mafunzo ya askari



# DC Kahama awaibukia wazazi ujenzi miundombinu ya shule

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# IGP Sirro apokea uwanja wa mafunzo ya askari

MKUU wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP) Simon Sirro, amepokea uwanja wa mafunzo ya askari katika Shule ya Polisi Moshi kutoka kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, ambaye alikuwa mgeni rasmi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu.



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali, Jacob Kingu (kushoto), akipokewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP Simon Sirro baada ya kuwasili katika Shule ya Polisi Moshi alipohudhuria hafla ya kupokea uwanja wa mafunzo ya askari.



Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye (mwenye suti nyeusi), akiwasili katika ufunguzi wa uwanja wa mafunzo ya askari kwenye Shule ya Polisi Moshi. **PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI**



Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, IGP Simon Sirro (kushoto), akisalimiana na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas (kulia), pamoja na maofisa wengine wa jeshi hilo, baada ya kuwasili katika Shule ya Polisi Moshi kwenye hafla ya kupokea uwanja wa mafunzo ya askari uliojengwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**

marobarnabas@yahoo.com

# Chonde chonde waandishi wa Kiswahili

ENYI waandishi wa magazeti mwakipeleka'pi Kiswahili? Wakati nchi za SADC zimeamua Kiswahili kiwe lugha ya nne katika nchi za Jumuiya hiyo, pia yatumiwa na Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Lugha zingine zinazotumiwa na Jumuiya hizo ni Kiingereza, Kifaransa na Kireno.

Hivi karibuni nilipokea ujumbe kutoka kwa msomaji anayefuatilia safu hii ya 'Tujifunze Kiswahili' katika gazeti hili akieleza masikitiko yake:

"Bwana Maro. Ingawa unafanya jitihada kubwa sana ya kutufunza matumizi sahihi ya Kiswahili, bado jitihada yako inachafuliwa na wakaidi wachache waandikao habari za michezo. Utumiaji wa maneno yasiyoeleweka kama vile; 'kamili gado', 'kwea pipa', 'kama lote' na mengineyo unatupa shida sana wasomaji. Je, tuwaache wapotoshe lugha au tuache kununua magazeti yao? Kumbuka, akosaye asipoelekezwa hujiona yuko sahihi." (KISSIWA Z.K. 0713 768 335).

Nilimjibu kwa ufupi kuwa kosa ni la BAKITA kutowakemea! Naye akanijibu: "Asante sana. Lakini tukiiacha Bakita je, Bakiza, Takiluki na wizara zinazohusika zinafanya kazi gani? Angalia: Takiluki ni taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Zanzibar."

Nimeamua kutumia ujumbe huo kwani labda (neno linaloashiria kuwapo kwa uwezekano; huenda, pengine, yawezekana) waandishi wa magazeti ya michezo, wakisoma kwa zingatio (jambo la kufikiriwa kwa makini; tafakuri) wataelewa malalamiko ya wasomaji kwa jinsi wanavyokereka (kitendo cha mtu kuudhika kutokana na jambo alilofanyiwa).

Baadhi ya maneno yatumiwayo na waandishi wa habari za michezo ambayo hayamo kwenye lugha ya Kiswahili au yamo lakini hutumiwa tofauti na maudhui (wazo kuu linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) yake! Nayaorodhesha kwanza kabla ya kuyachambua, yaani kusoma maandishi na kuhakiki fani na maudhui yake.

'Buana:' Neno hili hutumiwa kila siku na magazeti ya michezo. Eti 'buana' hutumiwa badala ya neno halisi, yaani bwana! Mara nyingi gazeti moja likianza kutumia maneno ya ovyo, mengine huiga, labda kwa dhana kuwa ndio lugha halisi kumbe ni upotoshaji!

'Bua' 1) chuma anachotumia mhunzi kukolezea moto ili uwake vizuri. 2) Kigogo cha mmea wa nafaka kama vile mtama au mahindi kilichokauka na kubaki baada ya kuvunwa; paje. 3) Kitendo cha kufanikiwa katika jambo; sibu. Kwa hiyo 'buana' si Kiswahili ila limebuniwa na waandishi wa magazeti ya michezo badala ya 'bwana' ambalo ndilo neno sahihi!

"Mitambo imewashwa rasmi Ligi Kuu" ni kichwa cha habari ya gazeti la michezo lililokubuhu (kitendo cha mtu kukithiri katika jambo maalumu hasa lisilopendeza) kwa kutumia maneno tofauti na maudhui yake.

Unasoma kichwa cha habari kilichoandikwa kwa herufi kubwa: "TUNATESTI MITAMBO" kikifuatiwa na habari kuwa:

"HISTORIA kuandikwa. Ndio, leo Jumapili Yanga itafanya tamasha kubwa la kuhitimisha Wiki ya Mwananchi, ambalo halijawahi kufanyika tangu klabu hiyo ilipoasisiwa miaka zaidi ya 80, kubwa ikiwa ni kiu ya mashabiki kutaka kuona mitambo mipya ikiwashwa Taifa." Wachezaji watawashwaje!?

Ingeandikwa: "Kwa mara ya kwanza, leo Yanga itafanya tamasha kuhitimisha 'Wiki ya Wananchi' tangu ilipoasisiwa zaidi ya miaka 80 iliyopita, huku mashabiki wakiwa na hamu ya kuwaona wachezaji wapya."

'Mitambo' ni wingi wa 'mtambo.' Ni vifaa vyenye kutoa nguvu za kuendesha vitu vinavyofanya kazi mbalimbali. 2) Kitanda ambacho hutumiwa kufumia nguo. 3) Kamba inayotengenezwa kwa chane za miyaa na hutumiwa kuvutia mtego wa samaki. 4) Eneo lisilokuwa na miinuko lipatikanalo kwenye mito zaidi ya mmoja.

Pamoja na maana zote hizo, waandishi wa magazeti ya michezo huandika 'mitambo' wakimaanisha 'wachezaji!' Binadamu awezaje kulinganishwa na vyuma vitumiwavyo kutengeneza mitambo?

'Mziki' ni neno litumiwalo mara kwa mara na magazeti ya michezo. Maana halisi ya neno hili ni mpangilio wa sauti za vinanda zinazoimbika; mdundo unaotokana na mseto wa sauti na ala za muziki kama vile ngoma, tarumbeta pamoja na uimbaji.

Kichwa kidogo kiliandikwa hivi: "Mziki Ulivyo" ikifuatiwa na maelezo kuwa: "Mchezo wa leo dhidi ya Kariobangi Sharks unaweza kutoa nafasi kwa kila mchezaji kuanza, lakini Zahera amepanga kufanya sapraizi ya kuanza na wachezaji tisa wapya huku wawili tu wakiwa wale waliocheza msimu uliopita."

**Methali: Kazi ni kanzi**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096 0784 334 096 0784 334 096**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Vipaji vinaposhindana na vipaumbele, kipi kitangulie?

WASHIKADAU wa elimu nchini wameanza kutoa lawama kwa mipangilio na sera za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwa kutanguliza vipaumbele vya kisera katika kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini, badala ya kuangalia tu ufaulu wao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Albert Chalamila alitoa lawama hizo katika ufunguzi wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa vyuo vikuu ambayo yamepangwa kuendeshwa kwa siku tisa, yakisimamiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mdau huyo wa elimu na kiongozi mwandamizi wa ngazi ya mkoa alikuwa hana shaka nini kitangulie kati ya hayo.

Katika mjadala wa kawaida ni rahisi kusema kuwa Chalamila hajaelewa au hajatilia maanani sababu za bodi hiyo kutoa mikopo kuendana na vipaumbele vya taifa, kwani bodi haina vipaumbele nje ya kile kinachoamuliwa wizarani, ambacho kinaendana na sera zinazofuatwa katika awamu iliyopo, n.k.

Sasa ni wapi ambapo kosa limefanyika, endapo kama alivyosisitiza mkuu huyo wa mkoa, ni vipaji ndiyo msingi wa mwanafunzi kusonga mbele katika masomo na kufanya vizuri, siyo tu shule bali katika fani husika, kuwa ana kipaji cha kutinga hapo na kujiendeleza humo. Akisukumwa tu kwenye mkopo kipaji kinakufa.

Suala la kwanza katika hoja ya mkuu wa mkoa ni kutatua suala lenyewe, kama kipaji kinakufa kwa hitaji la mkopo ambalo halitilii maanani vipaumbele, ambapo kwa maelezo yake, vijana watakimbilia mikopo na kubadili fani ambazo walikuwa na shauku zao kuanzia utoto au ujana wa shule.

Hapo kuna suala la ziada linajitokeza, kama wote wenye vipaji husukumwa kuliko na mikopo au wengine watabaki katika fani wanayoitaka, wakose mikopo halafu wadumae kielimu.

Hapo kuna tatizo lingine, kama kuna maisha ya elimu ya juu nje ya mikopo, na pia kama vipaji vinaweza kuendelezwa hata kijana akielekea kwingine.

Majawabu yanayopatikana katika hoja ya mkuu huyo wa mkoa ni kuwa kipaji inabidi kiheshimiwe, na ni chanzo muhimu zaidi ya kile ambacho mwanafunzi anaweza kufanya kwa ustadi zaidi katika maisha, kuliko kile ambacho kimewekewa mkono 'nje nje.'

Unaweza usitake kuhoji kama hisia hiyo ni sahihi au la, kwani licha ya kuwa wapo wanaoweza kuihoji, inakidhi hitaji la hoja sahihi au ya kina katika mantiki, dhana ya Rene



Wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu wakiandamana kudai kuchelewa kwa mikopo yao kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi Elimu ya Juu (HESLB). **PICHA: MTANDAO**

> Kama ni mwerevu katika masomo matatu manne ni kweli ataondolewa kipaji chochote maalum akifuata moja ya masomo hayo ili apate mkopo?

Descartes ya 'clear and distinct ideas,' yaani wazo au hoja ambayo mpangilio wake uko bayana.

Ni hoja ambayo inatokana na kuangalia maisha au jamii kwa karibu, hivyo kuielewa hiyo kanuni.

Tatizo kubwa zaidi la kupambanua hoja ya mdau huyo wa elimu ni kubainisha nani anaweza kukosea, mdau aliyeangalia mustakabali wa kukuza na kuainisha vipaji katika masomo na mwisho kutazamia michango adhimu katika jamii kutokana na vipaji hivyo, na 'realpolitik' ya kutafuta mikopo.

Katika hisia hii ya pili, mtu anaweka kando maadili, anaangalia tu mahitaji halisi kwa upande wake, na bila ubishi ni hitaji la fedha kupata elimu ya juu bila tabu ndiyo itakayotangulia.

Kwa maana hiyo kijana atakuwa hajakosea kukiacha kipaji chake na kufuata eneo tofauti ambako mikopo inatolewa, lakini taifa nalo je?

Ndiyo hapo inaingia hoja ya Chalamila kuwa kwa mwelekeo huo, tunaua vipaji, ambako kimsingi ina maana ya kukwamisha maendeleo.

Ni mpangilio tofauti wa hoja ukilinganisha na ule wa utoaji mikopo ambao unalenga ufaulu na maeneo ambapo mikopo inatakiwa itolewe kulingana na vipaumbele vya wizara na kwa maana hiyo vya taifa.

Sasa kijana atakuwa anapoteza kipaji au anafaa huku na kule pia? Hivi kupata mkopo wa masomo ya juu ni rahisi sana, mtu atupe kipaji halafu aende tu kusoma, na hilo lisiwe na athari yoyote kwa kile anachosoma, yaani awe anajilazimisha tu katika fani hiyo, haitaki kabisa?

Ni rahisi kuona kuwa hoja ya mdau haiendi mbali hivyo, ila inagusa suala ambalo linaweza kudhihirishwa kwa takwimu, au kuonekana katika maisha ya kawaida kwa masuala yanayofanana na hilo, kwa mfano mchezaji abadilishwe namba aanze kupoteza raha, si kwa kukosa kufunga ila kutofurahia nafasi hiyo.

Dhana ya kipaji ni pana, na katika matumizi yake ya kawaida mtoto mwenye kipaji anaonekana tu kuwa akili inachemka, na siyo anaelekea wapi siku za baadaye, na katika kipindi hicho ndoto (alizotaja kwa mbali mkuu wa mkoa) ni kama maruweruwe tu, siyo fani iliyoingia kichwani.

Halafu katika sekondari ngazi zote mbili (ya kawaida na ya juu) wenye vipaji mara nyingi hushinda masomo yote, wafae kokote.

Ina maana kuwa kama kipaji kinachoongelewa ni kipana, yaani uwezo wa kufaulu na siyo shauku ya kazi fulani na kuwa na kipaji cha kihisia cha kazi hiyo, bado siyo rahisi kusema kama kijana mwenye uwezo wa kufaulu vizuri sana masomo matatu anatakiwa aende wapi kimsingi.

Kama ni mwerevu katika masomo matatu manne ni kweli ataondolewa kipaji chochote maalum akifuata moja ya masomo hayo ili apate mkopo?

Ni rahisi zaidi kuona kuwa kipaji chake (uwezo wa kusoma, kuelewa na kutoa majibu ya maswali kwenye eneo au fani inayohusika na masomo hayo yote) kitaelekezwa eneo fulani, hata kama ni kwa hitaji la kupata mkopo, na siyo ajabu, wakati umri unajongea na ari ya awali kupungua, atulie hapo.

Vipaji katika maisha huingiliana na kubadilishana, kwani kuwa na kipaji ni dhana pana inayoweza kuegemezwa katika fani lukuki, na mtu hawezi kusomea fani zote kwa pamoja, au moja baada ya nyingine.

Ila elimu kwa upangilio wake inaanza kwa upana kiasi fulani halafu inabanwa huku kina chake kikiongezeka, kiasi kwamba ukifikia ngazi ya juu kabisa kuna chembe tu ya fani inayokuandama uifanyie kazi hadi ukubalike kukaa meza moja na mabingwa, kuwa una uwezo wa 'kutibu' katika fani hiyo, yaani kurekebisha dhana au mtiririko wa dhana ambao hauendi sawa kwa njia moja au nyingine. Ni'doctorate-Uzamivu'

Endapo kijana ana kipaji katika eneo fulani na siyo tu shauku ya mpito akiwa shuleni, zipo njia nyingi tu za vipaji hivyo kujitokeza mbeleni endapo ataendelea na masomo, apanue akili na kuanza kuchangia kifani na kimaisha kwa jumla.

Punde yuko mtu atagundua uwezo wake katika eneo fulani halafu si ajabu ahamie huko, au kuwe na mchepuo katika fani aliyochagua kwa ajili ya mkopo, awe kama vile ana uwezo wa ziada.

ELIMU

NA SHABAN NJIA, KAHAMA

# DC Kahama awaibukia wazazi ujenzi miundombinu ya shule

- Ataka wajitoe badala ya kutegemea wahisani kwa vyote
- Wauze mifugo kuwapatia mahitaji ya shule watoto wao



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha (aliyesimama kushoto) akizungumza na wananchi pamoja na wanafunzi wa Kijiji na Kata ya Kilango, Halmashauri ya mji wa Kahama, wakati wa ufunguzi wa kambi 28 za kata hiyo na Iyenze kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu ili waweze kusoma na kuandika.

WAHENGA walinena Elimu ni ufunguo wa maisha, ufunguo ambao ni dira ya maisha kwa mwanafunzi pindi anapomaliza masomo yake na kuanza kujitegemea.

Na katika hali hiyo anakuwa ameondokana na dhana ya kuwa tegemezi kwa wazazi na jamii yake.

Hata hivyo, mwanafunzi ana fursa nzuri ya kufanya vema katika masomo na mitihani yake ya mwisho, endapo mazingira ya shule ni rafiki kwa kujifunzia.

Mazingira mazuri kimsingi yanajumuisha miundombinu kama vile viwanja vya michezo, vyoo bora na safi, majisafi na salama, madarasa, nyumba za walimu pamoja na walimu wa kutosha wa masomo yote.

Asilimia kubwa ya shule za msingi na sekondari hapa nchini bado zina changamoto ya ukosefu wa mazingira rafiki ya kujifunzia mwanafunzi, pamoja na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali.

Bado baadhi ya shule zinakabiliwa na uhaba wa vyoo bora, viwanja vya michezo, upungufu wa madarasa pamoja na visima vya majisafi na salama.

Mkoa wa Shinyanga una jumla ya shule za msingi 553 huku Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama ikiwa na shule za msingi 91 na wanafunzi 10,722.

Aidha, Halmashauri ya mji wa Kahama, katika wilaya hiyohiyo ina shule 72 zenye wanafunzi 18,490.

Kwa upande wa Halmashauri ya Shinyanga vijijini, ina jumla ya shule za msingi 128 zenye wanafunzi 12,534.

Manispaa ya Shinyanga ina shule za msingi 48 zenye wanafunzi 54,001.

Vilevile Wilaya ya Kishapu ina shule za msingi 114 na wanafunzi 95,770, huku Halmashauri ya Ushetu ikiwa na shule 100 zenye wanafunzi 15,292. Kimsingi, shule zote hizo zinakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa na vyoo.

Kwa kuziona changamoto hizo za upungufu wa vyumba vya madarasa na vyoo, Halmashauri ya mji wa Kahama imeamua kuzishughulikia kwa kuhusisha pia wadau mbalimbali.

Wadau hao ni pamoja na wazazi, washirika wa maendeleo (NGOS), lengo likiwa ni kuangalia namna ya kutatua changamoto hizo, hususani vyumba vya madarasa na vyoo.

Hata hivyo, serikali ya wilaya hiyo kupitia kwa Mkuu wa wilaya Anamringi Macha anawasisitiza wananchi kubeba majukumu yao kwa kushiriki moja kwa moja kwenye utatuzi wa changamoto zilizo ndani ya uwezo wao.

Macha anabainisha kwa mfano kwamba si halali kwa wananchi wa wilaya hiyo kuendelea kuwaomba wahisani wawajengee vyoo katika shule zao za msingi na sekondari, kwa sababu hili liko ndani ya uwezo wao.

> Ombi kama hili nalipiga marufuku kwa kweli katika wilaya yangu... Inafaa muombe kujengewa miundombinu kama vyumba vya madarasa na maabara




Choo cha zamani chenye matundu manne kilichokuwa kikitumiwa na wanafunzi 717 wa Shule ya Msingi Gilime (kulia), kushoto ni choo kilichojengwa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania.

"Ombi kama hili nalipiga marufuku kwa kweli katika wilaya yangu... Inafaa muombe kujengewa miundombinu kama vyumba vya madarasa na maabara," anasema na kuongeza:

"Msije mkanikaribisha kwenye ufunguzi wa vyoo katika shule zenu ambavyo vimejengwa na wahisani...nitakuja kufungua na kuweka jiwe la msingi kwenye vyoo ambavyo vimejengwa kwa nguvu zenu wananchi."

Macha anasisitiza, ni aibu kubwa kuendelea kutegemea mashirika ya wahisani kwa kila kitu na hasa ikichukuliwa kwamba nchi ambazo yanatoka zimeendelea, hivyo cha kuomba ni ujenzi wa miundombinu kama vyumba vya madarasa, maabara na vifaa vyake.

"Na kwa hili la vyoo, inabidi wananchi tujenge vya kisasa katika shule zetu badala ya kuendelea kuona watoto wetu wakitumia vilivyochakaa, kwani ndiyo chanzo cha wanafunzi kujisaidia vichakani na hatimaye magonjwa ya mlipuko," anasema na kuongeza:

"Inashangaza kwa mfano kwa nini shule ya msingi kama Gilime yenye zaidi ya wanafunzi 717 ina matundu ya vyoo manne tu, mawili yakitumiwa na wanafunzi na mawili yaliyobaki yakitumiwa na walimu wakati wazazi wana uwezo wa kukutana na kujenga vyoo."

### UBAGUZI WA ELIMU

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa wilaya amewataka wananchi kuacha tabia ya ubaguzi wa kusomesha watoto wa kiume tu, huku wakike wakibaki nyumbani kulea wadogo zao, hali inayosababisha wageuke kuwa mama wa nyumbani wakati umri wao unawataka wawe shule.

Anabainisha kuwa kitendo hiki cha ubaguzi ndicho chanzo cha mimba na ndoa za utotoni kwani mwisho wa siku kwa kumnyima mtoto wa kike fursa ya masomo, kinachobaki ni kumuozesha.

"Sitasita kumchukulia hatua za kisheria mzazi atakayebainika kubagua watoto wake kielimu ili wa kike awe na jukumu la ulezi wa wadogo zake... suala la elimu halina mtoto wa kiume, wakike hata mwenye ulemavu," anasema.

### MAHITAJI MUHIMU KWA WATOTO

Macha anazungumzia pia suala la wazazi katika wilaya hiyo kuwahudumia watoto wao kwa mahitaji ya shule kama vile sare za shule, viatu, daftari, kalamu na mengineyo yaliyo muhimu kwa masomo.

Anabainisha kwamba asilimia kubwa ya wananchi wa wilaya ya Kahama wana mifugo ambayo wanaweza kuiuza ili watoto wao wapate mahitaji muhimu ya shule, badala yake hawalifanyi hilo, baadhi wakitegemea kufanyiwa na wahisani.

"Na ndiyo maana katika hili nimeshawaagiza maofisa elimu kata wahakikishe wanafanya sensa ya wanafunzi wasiokuwa na viatu na sare kwa kila shule ili tufuatilie hali ya kiuchumi ya wazazi wao," anasema na kuongeza:

"Kwa wazazi ambao tutakuta kwa mfano wana ng'ombe zaidi ya 10, wakati watoto wao hawana mahitaji ya shule, basi tutawasimamia wauze baadhi ya mifugo yao ili kununua mahitaji ya shule ya watoto wao."

### MENEJA WORLD VISION TANZANIA

John Massenza ni Meneja wa World Vision Tanzania, Kanda ya Ziwa.

Anasema wao kama wahisani na wadau wa elimu wilayani humo, tayari mpaka sasa wameshajenga matundu ya vyoo 32 yenye thamani ya Sh. Milioni 90 katika shule nne za msingi zilizo kata za Kilago na Iyenze.

Anazitaja shule walizozijengea miundombinu hiyo kuwa ni shule ya msingi Gilime, matundu ya choo nane, Mtungulu matundu ya choo nane, Tulole matundu ya choo nane na hivyo hivyo kwa shule ya msingi Isalenge.

### KAMBI ZA KUJIFUNZIA

Naye meneja mradi kutoka shirika hilo la World Vision Tanzania, Machibya Mwalla anasema kwamba katika kupambana na wimbi la watoto wasiojua kusoma na kuandika wameanzisha kambi.

Mwalla anabainisha kwamba kambi hizo ni za kujifunzia kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu kwa shule za msingi.

Anasema jumla ya kambi hizo ni 28 na zipo katika vijiji sita ndani ya kata mbili za Iyenze na Kilago.

"Walimu wanaofundisha watoto hao wanatoka katika kata hizo, lakini tunawatumia pia walimu waliostaafu na mafunzo yanakuwa kwa kila siku za Jumamosi," anasema.



Darasa katika mojawapo ya kambi 28 zinazotumika kufundisha wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu siku ya Jumamosi ili waweze kusoma na kuandika.

> Sitasita kumchukulia hatua za kisheria mzazi atakayebainika kubagua watoto wake kielimu ili wa kike awe na jukumu la ulezi wa wadogo zake...

Anabainisha hatua hiyo ya kuanzisha kambi imekuja baada ya kuona asilimia kubwa ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi hawajui kusoma na kuandika.

"Tumeanza na kata hizi na baadaye, tutaanzisha kambi hizo katika kata zingine," anasema na kuongeza:

"Lengo la kambi hizi ni kuwafikia zaidi ya watoto 2000...kambi hizi zimekuwa zikisaidia kuongeza uelewa na ufaulu wa wanafunzi ambapo umepanda kutoka asilimia 50 hadi kufikia asilimia 91 kwa kipindi cha mwaka mmoja."

### MWALIMU MKUU

Naye Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Gilime, Alex Zakayo, anatoa wito wa ushirikiano toka kwa wazazi na hasa katika suala zima la kuchangia maendeleo ya shule yao kwa faida ya watoto wao na taifa kwa ujumla.

"Kama alivyosema mkuu wa wilaya, wazazi wachangie kwa hali na mali ujenzi wa miundombinu iliyo ndani ya uwezo wao, lakini pia kuwapa mahitaji muhimu ya shule watoto wao na si kutegemea kila kitu kufanywa na wahisani," anasema.

JIELIMISHE

# WHO yataka hatua za dharura zichukuliwe



Madaktari bingwa wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

MAMILIONI ya watu wanaathiriwa kila mwaka kutokana na huduma za afya zisizo salama kote duniani.

Hali hiyo inasababisha vifo vya watu milioni 2.6, kwenye nchi za kipato cha chini na zile za kipato cha wastani.

Asilimia kubwa ya vifo hivi vinaweza kuzuiwa. Athari za kijamii na kiuchumi zinazotokana na matatizo kwa mgonjwa, huchangia kupotea kwa matrilioni ya dola kote duniani.

Shirika la Afya Duniani (WHO) sasa linaangazia dunia nzima katika suala la usalama kwa mgonjwa na kuzindua kampeni kuhusu uzalendo kwa mgonjwa wakati wa maadhimisho ya kwanza ya siku ya mgonjwa yaliyofanyika Septemba 17.

"Hakuna mtu anayestahili kuathiriwa wakati akipata huduma za afya. Kote duniani takriban wagonjwa watano hufariki kila dakika kutokana na huduma za afya zisizo salama," anasema Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi Mkuu wa WHO.

Wagonjwa wanne kati ya 10 huumia wakati wakipata huduma za afya ambapo makosa mengi huhusu vipimo, kutoa dawa na matumizi ya dawa.

WHO inasema makosa kwenye dawa pekee, hugharimu takriban dola bilioni 42 kila mwaka. Huduma za upasuaji zisizo salama huleta matatizo kwa hadi asilimia 25 ya wagonjwa na kusababisha vifo vya watu milioni moja wakati au mara tu baada ya upasuaji.

Kuumia kwa wagonjwa wakati wa kutoa huduma za afya haikubaliki.

WHO inatoa wito wa hatua za dharura kwa nchi kote duniani kupunguza madhara kwa wagonjwa wakati wa kupata huduma za afya. Uwekezaji katika kuboresha usalama wa mgonjwa unaweza kuokoa fedha.

Gharama ya kuzuia ni ya chini kuliko ile ya kutoa matatizo baada ya kasoro kutokea. Kama mfano, Marekani pekee iliangazia katika kuboresha, hatua iliyochangia kuokoa dola bilioni 28 kwenye hospitali kati ya mwaka 2010 na 2015.

Septemba 17 ilibuniwa kama Siku ya Mgonjwa Duniani na mkutano wa 72 wa baraza la afya duniani mnamo Mei 2019.

**HABARI UN**

JE, WAJUA?

# Kwamba kazi unayofanya kiukweli inakuua polepole?



Wafanyakazi hupoteza maisha kutokana na majukumu mengi ya kazi. **PICHA: MTANDAO.**

JEFFREY Pfeffer anaposema kuwa: "kazi zinawaua watu na hakuna anayejali," hasemi kwa njia ya mafumbo.

Anasema kwa hakika kabisa kutokana na utafiti alioufanya kwa miongo kadhaa, nchini Marekani na duniani kwa ujumla.

Profesa Pfeffer kutoka Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Stanford na mwandishi msaidizi wa vitabu 15, kuhusu muundo wa kampuni na masuala ya uongozaji rasIlimali watu, ametoa hoja hiyo katika kitabu chake.

Katika kitabu hicho cha hivi karibuni kiitwacho: "Kufa kwa ajili ya Mshahara" anaonyesha jinsi mifumo ya kazi inavyoathiri na hata kusababisha kukatisha maisha ya watu.

Katika kitabu hicho anazungumzia tukio la Kenji Hamada, mwenye miaka 42 aliyekufa kwa mshtuko wa moyo akiwa kwenye dawati lake kazini, jijini Tokyo nchini Japan.

Kabla ya kifo chake, alifanya kazi kwa siku 40 mfululizo bila ya kupumzika, na mjane wake anasema Kenji alikuwa na msongo mkubwa wa mawazo.

Huu ni moja kati ya mifano iliyokuwa kwenye chapisho lake, ambapo mwandishi anaeleza madhara ya mfumo wa kazi ambao wakati mwingine "si wa kibinadamu" kutokana na majukumu makubwa ya kazi.

Kwa mujibu wa ushahidi uliowekwa na Pfeffer, nchini Marekani, asilimia 61 ya wafanyakazi wanaona kuwa msongo unawafanya waumwe, na asilimia 7 wanasema walilazwa hospitalini kutokana na sababu zinazohusiana na kazi.

Makadirio yake ni kwamba, msongo una uhusiano na vifo vya wafanyakazi 120,000 nchini Marekani. Kwa mtazamo wa kiuchumi, msongo unawagharimu waajiri zaidi ya dola za Marekani 300,000 kwa mwaka nchini humo.

Katika kitabu chake, anaeleza kuwa kuna mfumo wa ufanyaji kazi unaowaua watu.

Je wewe una ushahidi gani kuhusu hili na ni kwa jinsi gani mfumo wa kisasa wa ufanyaji kazi, unawaathiri waajiriwa?

Kuna ushahidi wa madhara ya kiafya. Saa nyingi za kufanya kazi, kupunguzwa kazi, kukosa bima ya afya, masuala ya kiuchumi, migogoro kwenye familia na maradhi.

Kazi sasa zimekuwa si za kibinadamu. Kwa upande mwingine, kampuni zimeacha kuwajibika kwa ajili ya wafanyakazi wao.

Lakini changamoto za kiuchumi zimeongezeka, hofu ya kukosa ajira pia inaongezeka.

Kwenye benki za uwekezaji kwa mfano, kuna namna ya ufanyaji kazi, ambapo mfanyakazi huenda nyumbani kwake kuoga na kurejea ofisini.

Katika mfumo huo, waajiriwa wengi huingia katika uraibu wa dawa, kwa sababu wanaishia kutumia Cocaine na dawa zingine ili wawe macho.

Mfanyakazi wa kiwanda, rubani wa ndege, mwendesha lori, wana idadi ya saa za kufanya kazi.

Lakini kuna kazi zingine hazina saa maalumu za kazi. nchini Marekani, sababu ya tano ya vifo ni ile ya sehemu ya kazi.

### NANI ANAWAJIBIKA KWA VIFO HIVI?

Waajiri na serikali zinawajibika kwa kutochukua hatua yoyote kuhusu suala hili.

Ni kazi kubwa kiasi inapaswa kufanyike kitu kwa ajili ya kukomesha hili, lakini haiwezekani kwa mtu mmojammoja.

Kutatua tatizo hili yapaswa kuwa na utaratibu ambao utatoka kwa mtindo wa sheria.

Mazingira mabaya ya kazi husababisha maradhi kama vile sukari na shinikizo la damu.

Kwa upande wa gharama, kampuni zinaweza kuleta hoja kuwa kufanya mabadiliko katika mfumo wa kazi kutaathiri kipato chao.

"Hii si kweli," anasema Profesa Pfeffer na kuongeza:

"Tunajua kuwa watu walio katika msongo wa mawazo wako katika nafasi kubwa ya kuacha kazi... tunajua kuwa wafanyakazi wasio sawa kisaikolojia hawawezi kuizalishia kampuni inavyopaswa."

Anatolea mfano kwa nchi za Marekani na Uingereza ambako zaidi ya asilimia 50 ya siku za kazi hupotea kwa sababu ya wafanyakazi kutokuwapo kutokana na msongo wa kazi.

Hivyo, kuna athari kubwa kwa mfanyakazi mgonjwa anayekwenda kazini na asifanye kazi kama anavyotakiwa. Hali hii huigharimu kampuni.

### WAFANYAKAZI KUJIJALI

Kwa upande wa wafanyakazi, Profesa ameandika kuwa watu wajijali. Lakini ameulizwa swali kuwa itakuwaje ikiwa mwajiriwa atadai kuboreshewa mazingira ya kazi na akaishia kufukuzwa? Je mazingira ya kazi yatabadilishwaje?

Profesa anasema, kwanza waajiriwa wanapaswa kujali afya zao. "Ikiwa unakwenda kazini, mahali ambapo huwezi kuoanisha maisha ya kazi yako na familia, unapaswa kuacha kazi hiyo," anasema.

Jambo jingine ni kwamba, watu wanapaswa kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa. **BBC**

RIPOTI

# Kama si sababu ya kitabibu, usijifungue kwa upasuaji

KUJIFUNGUA kwa njia ya upasuaji ni utaratibu ambao hufanyika kwa sababu za kitabibu na unaweza kuokoa maisha ya mama na mtoto wake.

Hata hivyo, upasuaji mwingi unafanyika pasipo umuhimu, jambo ambalo linaweza kuweka maisha hatarini, kwa namna zote mbili, kwa muda mrefu na hata mfupi.

Duniani kote, takwimu za upasuaji zimekuwa zikiongezeka bila faida za msingi za kiafya kwa mama na mtoto.

Katika kutambua umuhimu wa kulifuatilia suala hili kwa haraka, Shirika la Afya Duniani (WHO) limechapisha maelekezo mapya yanayolenga kupunguza upasuaji usio wa muhimu wakati wa kujifungua.

Wakati wanawake wengi wenye uhitaji wa kufanyiwa upasuaji pindi wanapojifungua wakiwa wanaikosa nafasi hiyo, wengine wengi wanajifungua kwa njia hiyo pasipo umuhimu wowote, kwasababu ambazo si za kitabibu.

Kujifungua kwa njia ya upasuaji kunaweza kuwa na athari za muda mfupi na mrefu kwa mama, mtoto na hata ujauzito wa siku za usoni.

Hatari hii ni kubwa zaidi kwa wanawake walioko katika maeneo ambayo huduma za afya ni duni.

Vilevile kujifungua kwa njia ya upasuaji ni aghali na uwepo wa upasuaji huu usio wa lazima, unachukua rasilimali kutoka katika sehemu nyingine zenye uhitaji.

Dk. Betran anasema, "Ni muhimu wanawake wanaohitaji kujifungua kwa njia ya upasuaji waipate huduma hii ya kuokoa maisha, lakini vilevile upasuaji usio wa lazima uepukwe ili maisha ya mama na mtoto yasiwekwe hatarini."

Kuna sababu kadhaa ambazo zinaongoza watu kutaka kufanyiwa upasuaji wakati wa kujifungua na sababu zinatofautiana kulingana na nchi na nchi.

Hata hivyo, WHO inasema katika taarifa yake kabla ya kuingilia kati kujaribu kupunguza hali hiyo, utafiti unatakiwa kufanyika ili kufahamu ni kwa nini hali hiyo imeongezeka.

Ushauri wa WHO unajumuisha mambo kadhaa ikiwamo mawazo ya hofu na imani ya wanawake na wataalamu wa tiba kuhusiana na upasuaji wakati wa kujifungua.

Pia umezingatia ugumu na ufinyu wa mifumo ya kiafya na uratibu wa huduma za afya.

Mapendekezo ni pamoja na elimu kwa wanawake na familia kwa ujumla, kuhusu kujifungua na kuchagua namna ya kujifungua.

Mafunzo ya kisaikolojia kwa wanawake ambao wanaogopa maumivu ya kujifungua kwa njia ya kawaida na uchovu.

Mapitio ya miongozo ya upasuaji na mrejesho wa mara kwa mara kwa matabibu na wanaofanya upasuaji. **HABARI UN**



Daktari akimchunguza mjamzito. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

**NA NIKOLAUS KASERA**

TAKUKURU YAELIMISHA

# Hatuviziani kwenye Uwajibikaji

WADAU wa uwajibikaji waliokutana jijini Dodoma hivi karibuni, wamekubaliana kushirikiana ili kuhakikisha kwamba ufujaji na uporaji wa rasilimali za taifa ambazo ni mali za Watanzania unakomeshwa.

Wadau hao ambao wanatoka kwenye azaki za kiraia wamekutanishwa pamoja na watendaji wa mikoa mbali mbali wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), pamoja na watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tamisemi kwenye kongamano.

Ni kongamano lililolenga kuleta ufanisi wa kiutendaji baina ya azaki hizo na watendaji toka kwenye vyombo vya serikali, kikao ambacho kimeratibiwa na Wajibu Institute of Public Accountability.

Utafiti uliofanyika umebaini kwamba Azaki za Kiraia na wizara inayohusika na Tawala za Mikoa zimekuwa zikitumia mbinu mbili tofauti kufanya ufuatiliaji wa mapato na matumizi jambo ambalo wakati mwingine linaleta ukakasi wa matokeo yanayopatikana.

Hivyo basi, asasi ya Wajibu ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Ludovick Utouh ilileta wadau zaidi ya 150 jijini Dodoma, kujadili kwa pamoja na kupata ufumbuzi kuhusu PETS na SAM, vyote ambavyo ni mifumo ya ufuatiliaji.

PETS (Public Expenditure Tracking Survey) ni mfumo wa uhakiki wa matumizi ya fedha za bajeti ya serikali wakati ambapo SAM (Social Accountability Monitoring) vile vile ni mfumo wa ufuatiliaji ya matumizi ili kuthibitisha iwapo malengo yametimia.

Akihutubia wadau, Utouh alisisitiza kwamba uwajibikaji ni wajibu wa wote na si suala la taasisi zilizoko kisheria kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Takukuru, Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) wala taasisi ya Wajibu.

Utouh ambaye kabla ya kuanzisha taasisi ya Wajibu alistaafu wadhifa wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) miaka mitano iliyopita, alitolea mifano miwili ambayo alihusika nayo kipindi chake cha utumishi ambayo ilikuwa "mifupa migumu" hadi awamu ya tano ilipoingia madarakani.

"La kwanza lilikuwa suala la watumishi hewa...nilifanya ukaguzi na kwa miaka mitano mfululizo tulibaini uwepo wa janga hili ila mfupa ulikuwa mgumu...itoshe tu kumshukuru Rais wa awamu ya tano John Pombe Joseph Magufuli kwamba hatimaye suala hili lilivaliwa njuga na watumishi hewa 19,000 ambao walikuwa wanalipwa mishahara kila mwezi wakaondolewa...hili ni jambo ambalo lilihitaji ujasiri na maamuzi magumu."

Utouh alisema azma yake alipoanzisha Wajibu ilikuwa kuwasha vuguvugu ambalo siku ya siku litakuwa mazoea ya Watanzania ya kuwajibika katika nyanja zote na:

"Ndiyo maana kongamano hili ambalo linalenga kushirikisha wadau na kuhakikisha kwamba sote tunaelewa kwamba ili Serikali itoe huduma za jamii za uhakika, uwajibikaji haukwepeki... ingekuwa vita nyie ndiye mngekuwa "foot soldiers" maaskari wa kwanza wa kukabili adui."

Akiwasilisha hotuba ya Mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Mkurugenzi wa Elimu Kwa Umma Joseph Mwaiswelo alisema kitendo cha Wajibu kuwaleta pamoja wadau wa azaki za kiraia pamoja na Takukuru ni cha kupongezwa kwa sababu lengo ni moja na hakuna sababu ya kuviziana.

Msisitizo kama huo ulitolewa na wasilisho la Ofisi ya Waziri Mkuu Tamisemi kupitia kwa Falessy Kibasa.

Kibassa alitoa mfano wa enzi zake akiwa Mkurugenzi wilaya ya Kongwa kwamba alishirikiana na azaki ya Sikika inayofanya ufuatiliaji kwenye eneo la afya.

"Haikuwa kazi rahisi maana huko nyuma waliwahi kutimuliwa wilayani humo... nilichofanya ni kuwapigia mkwara ili wajieleze... bahati nzuri walijieleza vizuri na zoezi lao likafanikiwa," anasema na kuongeza:

"Nilijifunza kitu kwamba ukienda kufanya ufuatiliaji jishushe, pia sharti ujieleze kwa ufasaha... nawashauri nyie si Takukuru wala Polisi na si Usalama Wa Taifa...kazi mnayofanya inatusaidia sisi kwenye kuhakiki, kwamba huduma za jamii zimepatikana sasa iweje tuwe maadui?"

Kibasa maarufu Mwalimu Kibasa alisema azaki za kiraia ni kiungo muhimu kwenye zoezi la uwajibikaji ila anatahadharisha:

"Wekeni lenu sawa. Haiwezekani nyie huko mliko ndio wabadhirifu, shughuli zenu zinaghubikwa na mianya ya rushwa huku mnajipambanua kuwatembelea watendaji na nia ya kufanya ufuatiliaji."

Azaki zilizohudhuria kongamano hilo zilitoka nchi nzima pamoja na visiwa vya Pemba na Unguja, asasi la Zaeco ambalo ndilo liko kisheria visiwani na makamanda wa Takukuru kutoka wilaya mbalimbali.

Inatarajiwa kwamba baada ya mafunzo na uwezeshaji uliotolewa, azaki hizo na watendaji mbalimbali watashirikiana ili Watanzania kwa ujumla wao, waweze kunufaika na rasilimali za taifa pasipo ufujaji na matumizi mabaya ya rasilimali hizo.

**TAKUKURU**




Moja ya vilabu vya kupinga rushwa shuleni. **PICHA: MTANDAO**




Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbun'go. **PICHA: MTANDAO**

> "Wekeni lenu sawa. Haiwezekani nyie huko mliko ndio wabadhirifu, shughuli zenu zinaghubikwa na mianya ya rushwa huku mnajipambanua kuwatembelea watendaji na nia ya kufanya ufuatiliaji.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

## KWA sasa wanafunzi wa shule ya msingi hadi kidato cha nne wanasoma bure baada ya serikali kufuta ada na michango shuleni. Kifanyike nini zaidi kuboresha elimu nchini? Wadau wanajadili



### DEVIS KATETI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

TUKIWA na dhamira ya dhati na kuwa na viongozi wenye kutembea juu ya kauli zao huku wakihakikisha kuwa kila senti kwenye rasilimali za nchi inatumika ipasavyo bila upotevu au kudondokea kwenye mifuko ya wajanja wachache, tunaweza kabisa kuwa na shule bora zenye vifaa na walimu bora na elimu bora ya bure inayogharimiwa na serikali.

Hiki ndicho kinachoonekana kwa sasa nchini na hasa baada ya serikali kufuta ada ili wanafunzi wengi wapate elimu hata wale wanaotoka kwenye familia maskini. Nchi imeshuhudia jinsi serikali ilivyoweka mfumo wa kukusanya kodi na sasa kila Mtanzania anatambua umuhimu huo ndio maana ikafikia kutoa elimu bure.

Fedha zinazokusanywa zinafanya kazi ya maendeleo ikiwamo ya kulipia gharama za elimu bure.

Jambo la msingi ni kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali za kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu, haijalishi ni ya kiwango gani, lakini ni bora mtoto aende shule kuliko kukaa nyumbani kwa sababu ya ukosefu wa ada.

Uboreshaji wa elimu umeanza kwa kuondoa ada na kisha mambo mengine yatafuata baadaye. Hivyo tuipe serikali nafasi ya kuendelea kuboresha elimu na siyo kuibeza kama ambavyo baadhi ya Watanzania wamekuwa wakifanya kana kwamba hawaoni lolote linaloendelea kwenye sekta ya elimu.

Wanasiasa wajiweke pembeni kwenye jambo hili na kuwaachia wataalam wafanye kazi yao ili hatimaye elimu yetu iwe bora na yenye ushindani katika soko la ajira.



### AMINATHA KYANDO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

KWA maoni yangu, kufutwa ada ni sehemu tu ya kupunguza changamoto kwenye elimu na inatakiwa kutafutwa mbinu zaidi za kuinua kiwango cha elimu nchini.

Maabara ziboreshwe, kuwe na vitabu vya kutosha na hasa kitabu kimoja cha kiada badala ya vingi kama ilivyo sasa, unakuta shule hii inatumia kitabu cha mtu fulani na nyingine hiki.

Yaani ni vurugu tupu, hakuna elimu bali ni kuchanganya wanafunzi tu. Zaidi sana ni kama watu wanafanya biashara kwenye elimu huku wakijua wazi kwamba kinachofanyika ni kudidimiza elimu.

Kwa maana hiyo bila kufanya mabadiliko na kubuni mbinu mbadala za kupunguza matatizo yanayoikabili elimu, ninaamini hatua ya kufuta ada haiwezi kuwa na manufaa, badala yake wanafunzi watasoma wengi, lakini watahitimu wakiwa hawana kitu.

Ada imefutwa lakini kero zinazolalamikiwa kuwa zinadumaza elimu zimeendelea kuwapo. Inawezekana kwa sasa hali imetulia kidogo, lakini suala la mitaala kubadilishwa bila kushirikisha wadau ambao ni walimu lilikuwa likilalamikiwa sana.

Yaani ni kwamba baadhi ya watu wameweka maslahi yao mbele kuliko kutoa elimu bora ambayo ingesaidia wanafunzi kwa maisha yao ya baadaye.

Pamoja na kwamba ada zimefutwa, lakini cha msingi kinachotakiwa kufanywa ni kuondoa kabisa kero hizo, ambazo ninaziona kama ndizo zinachangia kuifikisha nchi hapa ilipo, huku wakiwa hawana wasiwasi na madudu wanayofanya kwenye nafasi zao walizoshikilia.



### MARIAM MAKANGE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

MIMI kama mdau wa elimu ninasema kwamba kufuta ada hakupandishi kiwango cha elimu...wakitaka ufaulu uongezeke waboreshe mazingira kwa kuongeza mishahara kwa walimu, kujenga maabara, kuongeza madawati ya kutosha na mahitaji mengine ya muhimu shuleni ndipo ufaulu utapanda.

Mbona shule za binafsi ada ni kubwa lakini wanafunzi wanafaulu sana? Kwa hiyo mimi sidhani na siamini kama kufuta ada kuna uhusiano na uboreshaji wa elimu.

Sina maana kwamba ninadharau utaratibu wa elimu bure, ninachosema ni kuwa kuondolewa kwa ada siyo njia pekee ya kumaliza changamoto kwenye elimu.

Kwanza nieleweke kuwa sipingi ada kufutwa bali cha msingi ni kwamba ufutaji wa ada ungeenda sambamba na kutatua kero na changamoto zinazoikabili elimu ya Tanzania, hilo likifanyika tunaweza kushuhudia kiwango cha elimu kinainuka, lakini bila kufanya hivyo itakuwa ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu, kutokana na ukweli kwamba kuondoa ada hakutanui wigo wa kukuza elimu bali kinachoweza kupanua wigo huo ni kuwa na walimu bora katika kufundisha wanafunzi na kuboresha miuondombinu yote ya elimu ili iwe rafiki kwa elimu yetu na vilevile maslahi ya walimu yaboreshwe ili wafanye kazi yao kwa moyo wote.

Siyo kwamba kwa sasa walimu hawafundishi, ila kinachofanyika ni kama kutimiza mradi tu ili bora liende, lakini changamoto zinazowakabili zimewanyong'onyeza.



### BASHIR UHADI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

SERIKALI ina dhamira ya kweli katika jambo hili, ndio maana tumeshuhudia wanafunzi wa shule za msingi na wale wa kidato cha kwanza hadi cha nne wakisoma bure.

Kinachotakiwa kuboreshwa ni suala la nyenzo za kufanyia kazi, mishahara ya kutosha kwa walimu na kila mahitaji yote yanayohusu elimu, hayo yakifanyika ni lazima kiwango cha elimu kitapanda au kuinuka.

Vinginevyo itakuwa vigumu kufuta ada halafu mazingira ya walimu yakawa ni yale yale bila kuboreshwa, kwani haisaidii kitu kufuta ada halafu shule ina walimu watano na walimu 200, ambao hawafundishi kwa moyo.

Ndio maana nikasema inaweza kusaidia kidogo kwa upande mmoja tu wa kuondoa kero kwa wanafunzi, lakini kiuhalisia mambo yatakuwa ni yale yale iwapo hakutakuwa na juhudi za ziada ya kumaliza matatizo yote yanayoizunguka sekta ya elimu.

Hivyo hapa kuna mambo mawili ambayo yanaweza kutokea ikiwa ni pamoja na kusaidia wanafunzi wengi kuendelea na masomo na hasa wale ambao wameshindwa kwenda sekondari kwa kukosa ada na pia kulikuwa na wanafunzi mitaani wana akili lakini kutokana na wazazi wao kukosa uwezo wa kifedha wakawa wako mitaani, lakini sasa wanaweza kufaidika katika mazingira hayo ingawa suala la kuinua kiwango cha elimu linaweza kuwa kidogo.



### CHRISTINA GAMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

NIANZE kwa kuipongeza serikali kwa mpango huu kwani ni jambo jema kwa Watanzania na mimi ni mmojawapo wa walionufaika nao, kwani wengi wetu kama wazazi hatukuwa na uwezo wa kuwalipia ada watoto wetu.

Ila pamoja na hayo, serikali ijitahidi kuboresha mazingira mengine ambayo kwa namna moja au nyingine yamekuwa yakichangia kukwamisha maendeleo ya elimu kwa wanafunzi na hasa wa kike kikubwa zaidi kikiwa ni tatizo la mimba.

Hapa ninazungumzia ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari za kata ili ikiwezekana, wanafunzi wa kike wasipange mitaani au wasitembee umbali mrefu kufuata elimu.

Mazingira hayo yamekuwa ni kichocheo kikubwa cha kuwapo kwa mimba, kwani wanafunzi wanapopanga mitaani au kutembea umbali mrefu kwenda shuleni wanakutana na vishawishi vingi ambavyo mwishowe hujikuta wakipachikwa mimba na kukatisha masomo.

Ujenzi wa mabweni ufanywe na wananchi, kutokana na ukweli kwamba sekondari za kata ni mali yao.

Serikali imebeba mzigo mkubwa baada ya kuondoa ada, sasa kilichobaki ni sisi wazazi kusaidia kwenye ujenzi wa mabweni.

Hiyo ni njia mojawapo ya kupanda kwa kiwango cha elimu iwapo mpango wa ujenzi wa mabweni utafanikiwa badala ya kutegemea kuondolewa kwa ada tu.





## Wawekezaji kutumika kunoa vijana kujiajiri

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KAMPUNI binafsi zinazowekeza kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji mali nchini zinaweza kutumika kama vyuo vya kuwanoa vijana na kuwawezesha kujiajiri, hivyo kupunguza tatizo la ajira nchini.

Hayo yamebainika kupitia mradi wa kuwajengea uwezo vijana wa 'Youth Building' ambao unatekelezwa na Shirika la Catholic Relief Service (CRS) kwa kushirikiana na Shirika la Caritas Tanzania chini ya Kanisa Katoliki na kutekelezwa katika kata mbili za Jiji la Mbeya.

Meneja wa Mradi huo, Mary Chotah, alisema jana kuwa mradi huo uliwachukua vijana 60 kutoka katika kata za Mabatini na Sinde jijini Mbeya na kuwapeleka katika kampuni mbalimbali kwa ajili ya kujifunza kwa vitendo na baadhi yao wakafanya vizuri na kuajiriwa moja kwa moja na kampuni hizo.

Alisema baadhi ya vijana waliochukuliwa ni wale ambao walishindwa kuendelea na elimu ya juu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo sababu za kiuchumi na baada ya kuwachukua walikuwa wanawapeleka kwenye kampuni za uzalishaji kila mtu kulingana na anachopenda.

"Mradi wetu unalenga kuwasaidia vijana ambao waliachwa njiani kwenye elimu wakashindwa kuendelea. Lakini vijana hao walikuwa wale wanaopenda kujiendeleza kimaisha na wengi wao wamefanya vizuri sana," alisema Chotah.

Ofisa Mradi wa mradi huo, Nyanyonyi Neke, alisema wakati wa kutekeleza mradi huo maofisa wa mradi huo walikuwa wanatembelea kampuni zenye fursa mbalimbali na kisha kuwaelimisha vijana kuhusu shughuli hizo.

Alisema baada ya kuwaelimisha vijana hao kila mmoja anachagua kile ambacho anahisi kinaweza kikamsaidia na ndipo anapelekwa kwenye kampuni hizo kwa ajili ya kujifunza kwa vitendo.

"Hii ni fursa nzuri sana kwa vijana hasa wenye nia ya kuishi ndoto zao, wengi tuliowapeleka kwenye kampuni hizo wameajiriwa na wengine wamejiajiri wenyewe," alisema Nyanyonyi.

Akiwakabidhi vyeti vijana waliohitimu mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi (Mipango) wa Mkoa wa Mbeya, Conrad Milinga, aliyapongeza mashirika hayo kwa kubuni mradi huo kwa madai kuwa utasaidia kuwajengea uwezo vijana.

Alisema baadhi ya kampuni zinaajiri watu kutoka nje ya nchi kutokana na Watanzania kutokuwa na ujuzi unaohitajika na hivyo akawataka vijana waliopata mafunzo hayo kwenda kushindana kwenye soko la ajira.

Alisema ujuzi walioupata ni silaha tosha ya kupata ushindi kwenye vinyang'anyiro vya ajira kwa kuwaaminisha waajiri kuwa wana uwezo hata kuwazidi wageni wanaoaminiwa sasa.

# Jenerali Mwamunyange ageukia elimu

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

WATANZANIA wameshauriwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa kuchangia nguvu zao ili kuimarisha sekta hiyo na kuliwezesha taifa kuwa na maendeleo endelevu.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama mstaafu, Jenerali Devis Mwamunyange, alipokuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Kidzcare ambayo inaendeshwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Kidzcare.

Jenerali Mwamunyange alisema taifa haliwezi kuwa na maendeleo endelevu yakiwamo ya uchumi wa viwanda endapo halitawekeza ipasavyo kwenye elimu ambayo alidai ndiyo chimbuko la wataalamu.

Alisema serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuendeleza sekta ya elimu ikiwamo kuboresha miundombinu na kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shuleni wanaandikishwa.

"Serikali ya awamu ya tano chini Rais John Magufuli imejitahidi sana kuboresha sekta ya elimu. Sasa ni wajibu wetu na sisi wananchi na wadau wengine kushiriki katika kuboresha sekta hiyo ili tuweze kuliinua taifa letu," alisema Jenerali Mwamunyange.

Aidha, aliipongeza Kidzcare kwa kuanzisha shule hiyo kwa kuwa itasaidia kuimarisha sekta ya elimu wilayani Kyela na mkoa wa Mbeya kwa ujumla.

Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Kyela, Palemon Ndalugiliye, aliwataka wanafunzi wa shule zote wilayani humo kuwa na nidhamu na kusoma kwa bidii kwa madai kuwa hiyo ndiyo siri pekee ya kupata ufaulu mzuri kwenye mitihani yao.

Aliwataka kuachana na mambo ambayo hayawafai kulingana na umri wao ikiwamo mapenzi ili yasiwapotezee muda na pengine kuwapotezea dira ya maisha yao ya baadaye.

"Ukifanya mambo ambayo sio ya kinidhamu huwezi kufanya vizuri kwenye masomo, sasa nawashauri kokote mtakakoenda kuanzia sekondari mpaka vyuo vikuu cha msingi kuzingatia ni nidhamu vinginevyo hamtafaulu vizuri," alisema Ndalugiliye.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Mary Notman, alisema msingi mzuri wa elimu ni shule za msingi na hivyo akaiomba serikali kuongeza uwekezaji katika elimu ya msingi nchini.

Alisema ngazi hiyo ya elimu ndiyo muhimu zaidi katika kuwaandaa wanafunzi kwa maelezo kuwa mwanafunzi mzuri wa ngazi za juu za elimu ni yule aliyeandaliwa vema angali mdogo.

Alisisitiza kuwa elimu ndiyo mkombozi wa taifa, hivyo akasisitiza wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni na kuhakikisha wanawapatia mahitaji yote muhimu ili wasome katika mazingira mazuri na waipende shule.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei, akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana, kuhusu kukamatwa kwa madumu yaliyokuwa yanatumiwa na wauzaji haramu wa mafuta ya petroli na dizeli katika maeneo mbalimbali mkoani humo.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanaswa na lita 5,900 za petroli

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

OPERESHENI inayofanywa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya ya kudhibiti uuzwaji holela wa mafuta ya petroli na diseli, imeanza kuzaa matunda baada ya watu 16 kutiwa mbaroni wakiuza bidhaa hiyo bila kuwa na kibali.

Watuhumiwa hao walikamatwa na zaidi ya lita 5,900 za mafuta hayo wakiwa wanayauza katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya bila kuchukua tahadhari hali ambayo inadaiwa kuwa inahatarisha maisha yao.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Ulrich Matei, alisema jeshi hilo liliamua kuanzisha operesheni hiyo ili kudhibiti uuzwaji holela wa nishati hiyo.

Alisema operesheni hiyo ilifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwamo Chimala, Igurusi na Igawa wilayani Mbarali, Maghorofani, Uyole na Iteji kwa Jiji la Mbeya, Wilaya ya Rungwe na eneo la Ipinda wilayani Kyela na Chunya.

Matei alisema watuhumiwa hao walikutwa na madumu 79 na mapipa sita ambayo yanatumika kuhifadhia nishati hiyo pamoja na mipira ya kuhamishia mafuta hayo kutoka kwenye chombo kimoja kwenda kwenye chombo kingine.

"Tuliamua kufanya operesheni hii kutokana na kuongezeka kwa matukio ya moto katika maeneo yetu. Sasa hawa tuliowakamata walikuwa wanauza nishati hii bila kuwa na leseni na tutaendelea na msako katika maeneo mengine," alisema Kamanda Matei.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Majaliwa Edward (30) mkazi wa Mwambene, Edson Kalinga maarufu kwa jina la 'Mangi' (32) mkazi wa Iganzo, Hamis Anyimike (32) mkazi wa Mafiati, Issah Mwambelo (33) mkazi wa Sae, Kambela Mwaipopo (30) mkazi wa Makunguru na Daud Mwasalemba (40) mkazi wa Itezi wote jijini Mbeya.

Wengine ni Lugano Mwasalemba (18) mkazi wa Kibonde Nyasi, Sikudhani Anthony (35) mkazi wa Isyonje, Hashim Joseph (20) mkazi wa Mchangani na Justine Adam (21) mkazi wa Isyonje wilayani Rungwe.

Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni George Mwakalobo maarufu kwa jina la 'Mwadada' (40) mkazi wa Ipinda, Majuto Simon (37) mkazi wa Kapwili, Lwitiko Mwaipopo (38) mkazi wa Ipinda na Jakobo Mwakilema (47) mkazi wa Ipinda wilayani Kyela pamoja na Angalwisye Asubishi (35) mkazi wa Chimala na Mwangambo Uswege (40) mkazi wa Igurusi wilayani Mbarali.

Alisema watuhumiwa hao wapo mahabusu na Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi wa shauri hilo na kwamba utakapokamilika watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Kamanda Matei aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuepuka kufanya biashara hiyo bila kuwa na leseni wala kibali chochote kutoka kwenye mamlaka husika kwa madai kuwa nishati hiyo ni hatari kwa maisha ya watu.





# Wasomi watakiwa kuuinua ushirika

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

VIJANA wasomi wameshauriwa kujiunga na vyama vya ushirika na kuviongoza na kuachana na mitazamo hasi, kuwa vyama hivyo ni vya wazee.

Pia wameshauriwa kuwa wanachama wa ushirika kutawaongeza nguvu ya kitaalamu na kufanikisha jitihada ya kuimarisha ushirika nchini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Joyce Mbwambo, wakati walipotembelea baadhi ya vyama vya ushirika katika Wilaya ya Hai.

Mhadhiri huyo alikuwa ameongozana na wanafunzi 60 wa chuo hicho ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo.

Mbwambo alisema vyama vingi vya ushirika hususani vyama vya msingi, vimekuwa vikiongozwa na wazee, huku vijana wasomi wakiwa mitaani.

Alisema kuna haja sasa kwa vijana hao kuamka na kuona kuwa vyama hivyo ni moja ya fursa kwao katika kupeleka elimu waliyoipata vyuoni na kuvisaidia kujiendesha kibiashara na kujikwamua kiuchumi.

"Ipo fikra mbaya juu ya vyama hivi vya ushirika, vijana wasomi wanaona hawawezi kufanya kazi kwenye vyama hivi kwa madai kuwa hakuna hela, lakini baadhi ya wazee wanafikiria kuwa vijana watakuwa wezi kwenye vyama vyao. Haya ni mawazo hasi ambayo hayapaswi kuendelezwa katika harakati hizi za kuvifufua vyama vya ushirika nchini," alisema Joyce.

Husein Omary ambaye ni miongoni mwa wanafunzi waliokuwa kwenye ziara hiyo, alisema bado kunahitajika elimu ya kina juu ya namna ya uendeshaji wa vyama vya ushirika na kubuni miradi ambayo itaviwezesha kujiendesha kwa faida.

"Vyama vingi vya ushirika havina hali nzuri. Katika kipindi hiki ambacho serikali imedhamiria kufufua ushirika nchini, maofisa ushirika wanapaswa kutoka maofisini, kwenda kwenye vyama hivi na kutoa elimu. Ni kwa sababu vingi vinayumba kutokana na kukosekana kwa elimu na utaalamu wa kuviendesha," alisema Omary.

Akizungumza zaidi kuhusu taasisi hizo, Mashaka Laurent, alisema katika harakati za kuvifufua vyama vya ushirika, ipo haja kwa serikali, kuyatazama masoko ya mazao na usimamizi wa vyama hivyo, kwa kuwa vyama vingi vimekuwa vikiyumba, kutokana na usimamizi mbovu na kukosekana kwa masoko ya uhakika.

# Waomba wakalimani mahakamani, polisi

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

CHAMA cha watu wenye ulemavu wa kusikia (Chavita), mkoani Kilimanjaro, kimeiomba serikali kuajiri wakalimani katika vitengo nyeti kama polisi, magerezani na mahakamani ili kuwapa msaada wanaokosa kutokana na tatizo la mawasiliano.

Waliomba Wizara ya Mambo ya Ndani, kuangalia namna ya kuajiri wakalimani katika kila kitengo kutoa msaada wanapofika katika taasisi hizo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki katika kongamano la uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya alama kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama na Mratibu wa Chavita Wilaya ya Hai, Pulcaria Aloyce.

Alisema watu wenye ulemavu wa kusikia wanakabiliwa na changamoto wanapofikia katika taasisi hizo bila kuwapo kwa mkalimani wanakosa haki zao kwa kushindwa kujieleza na kupatikana kwa ushahidi sahihi.

"Tunaiomba serikali kuangalia namna ya kuajiri mkalimani wa lugha za alama katika vyombo vya ulinzi na usalama ili waweze kupata tafsiri mara wanapofika katika vituo hivyo," alisema Aloyce.

Aidha, alisema wakati wa utoaji wa ajira tunaomba wawakumbuke watu wenye ulemavu ili kupatikana mkalimani mmoja katika kila halmashauri ili kurahisisha mawasiliano," alisema Pulcaria.

Akifungua kongamano hilo Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliyewakilishwa na Ofisa Tarafa ya Kata ya Masama, Nsajigwa Ndagile, alisema watu wenye ulemavu ni binadamu kama walivyo wengine na wanahitajika kupewa huduma zote kama walivyo raia wengine wote wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa sasa tutaishauri serikali kuangalia namna ya kuweka ajira za wakalimani katika kila wilaya lakini kwa sasa tunawaomba mwendelee kutoa mafunzo ya alama ili watendaji wa idara mbali mbali wapate mafunzo ya alama kuwezesha kuwahudumia watu wenye ulemavu," alisema Ndagile.

Kwa upande wao baadhi ya washiriki Inspekta wa Jeshi la Polisi katika wilaya hiyo, Zacharia Shabo, alisema mafunzo hayo yataweza kuwasaidia baadhi ya askari kufahamu lugha za alama.

Ufahamu huo utasaidia kuwahudumia watu wenye ulemavu wanapofika katika kituo hicho.

"Ni kweli wapo baadhi ya walemavu ambao wakifika katika kituo cha polisi unaanza kubuni ili kuwapa huduma, lakini kwa baadhi ya askari wetu kupata mafunzo kunaweza kusaidia mawasiliano kuwa rahisi zaidi," alisema.

Naiman Akyoo ni Mkaguzi Msaidizi wa Magereza kutoka Gereza la Karanga, aliiambia Nipashe kuwa licha ya kazi yao kuwahifadhi na kuwarekebisha mienendo ya wahalifu, changamoto ya mawasiliano hiyo ipo na mafunzo hayo yataleta mabadiliko.

Aidha, Hakimu wa Mahakama ya Bomang'ombe, Regina Samwel, alisema watu wenye ulemavu wamekuwa wakifika kutoa ushahidi katika mahakama hiyo na kuwataka waandike hali ambayo imekuwa ngumu kwao.

"Ambacho tumebaini kuwa watu hawa hawapendi kuambiwa waandike. Kutokana na kukosekana kwa wakalimani tunateseka kuwaelewa na wakati mwingine tunatumia nguvu kubwa ili kubaini nini alichotamani kukisema lakini ikiwa tutapata mafunzo haya ya alama, yatatusaidia kufanya kazi kwa uhakika bila kubaki na mashaka," alisema hakimu Regina.



Baadhi ya askari wa kampuni binafsi za ulinzi Mkoa wa Dodoma, wakiwa kwenye gwaride la kufunga mafunzo yao ya miezi mitatu, yaliyolenga kuwajengea weledi zaidi wa kazi, katika Bwalo la Jeshi la Polisi mkoani humo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# K'njaro kuchanja watoto 224,000

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

TAKRIBANI watoto 223,772 walio na umri kati ya miezi tisa hadi chini ya miaka mitano wa maeneo yote ya mkoa wa Kilimanjaro, wanatarajiwa kupatiwa chanjo ya surua, rubella na polio.

Chanjo hiyo inatolewa ili kuwakinga na magonjwa hayo pamoja na kuzuia kupooza.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Kilimanjaro, Peter Kihamia, wakati akitoa elimu kwa waandishi wa habari mkoani hapa kuhusiana na kampeni ya chanjo hiyo.

Alisema kuwa, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeanzisha kampeni maalum ya kutoa chanjo hiyo kwa lengo likiwa ni kutokomeza magonjwa hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakiwashambulia watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Kihamia alisema kuwa, kampeni hiyo ya kutoa chanjo kwa mkoa wa Kilimanjaro inatarajiwa kuanza wiki hii Septemba 26 hadi 30 na kwamba vituo 312 vitatoa huduma hiyo, huku makadirio yakiwa ni kuwafikia watoto 223,772.


"Tunatambua yapo maeneo ambayo vituo vya afya vipo mbali hali ambayo inawalazimu wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma hii ya chanjo kwa sasa tumekuja na huduma ya mkoba ambayo wataalamu wetu watakuwa wakienda katika maeneo ambayo yapo mbali na kituo ili kutoa huduma ya chanjo," alisema Kihamia.

Aliwaambia wanahabari kuwa faida kubwa ya chanjo hii kwa watoto ni kuwakinga na magonjwa ya surua, rubella na ugonjwa wa kupooza jambo alilosema kuwa katika kipindi cha miaka mitano hakuna mtoto katika mkoa wa Kilimanjaro ambaye amethibitika kuwa na magonjwa hayo.

Kihamia alisema kuwa mtoto ambaye hatapata huduma hiyo ya chanjo madhara yake ni kuwa hatarini kupata maambukizi ya magonjwa hayo ambayo huleta vifo, endapo atacheleweshwa kupatiwa matibabu lakini pia anaweza kupooza baadhi ya viungo.

Kwa upande wake, Ofisa Afya Mkoa wa Kilimanjaro, Jonas Mcharo, alisema kuwa huduma hiyo ya chanjo hutolewa bila malipo na kuwataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka watoto kupatiwa chanjo kwani kinga ni bora kuliko tiba.

Aidha, aliwataka wazazi wanapoona mtoto amepata ulemavu wa viungo vya mwili ghafla kumwahisha hospitalini kufanyiwa uchunguzi.



# Atahadharisha mtikisiko visiwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema visiwa vya Zanzibar vinaweza kupata mtikisiko mkubwa wa uchafuzi wa mazingira, iwapo watu wataachiwa na kuendelea na uchimbaji holela wa mchanga na matumizi ya mawe na kokoto yasiyo na mpango.

Alisema kutokana na hali hiyo, serikali imeandaa utaratibu maalum wa upatikanaji wa rasilimali hizo muhimu katika harakati za ujenzi wa majengo na miundombinu mbalimbali.

Balozi Iddi alisema hayo alipofanya ziara fupi ya kukagua mradi wa ujenzi wa tangi kubwa la Kuhifadhia majisafi na salama katika kijiji cha Kitope Mbaleni baada ya ujenzi wake kusuasua kutokana na ukosefu wa mchanga, kokoto na mawe. Alisema nchi hivi sasa imeharibika kutokana na mashimo mengi yalichimbwa kwa ajili ya kupata mchanga wa ujenzi hali inayoashiria lazima zipatikane mbinu mbadala za kukabiliana na changamoto hiyo ya uchafuzi wa kimazingira inayoweza kuleta maafa baadaye.

Balozi Iddi alisema serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, wataalamu, taasisi za jumuiya za kiraia zinafanya jitihada za makusudi katika kuona ujenzi utakaobuniwa wa majengo ya taasisi za umma na binafsi yanazingatia mfumo wa kutumia mchanga kidogo.

Aliishukuru Taasisi ya kiraia ya Tanzania Youth Icon (TYI) pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (Zawa) kupitia wadau wa maendeleo kwa uamuzi wao wa kujenga tangi hilo litakalowanufaisha wananchi waliomo ndani ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja.

Alisema Kitope ni eneo lenye usumbufu wa huduma za majisafi na salama kwa muda mrefu tangu kuharibika kwa tangi la zamani na wananchi wanaozunguka eneo hilo wamekuwa wakipata changamoto ya huduma hiyo muhimu kwa ustawi wao. Naye Mhandisi Mkuu wa Mradi wa Ujenzi wa Tangi hilo, Jackson Maro, alisema tangi hilo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhifadhi zaidi ya lita 50,000.

Mhandisi Maro alisema kazi hiyo imeanza rasmi kwa hatua ya msingi karibu wiki tatu sasa, lakini imeshindwa kuendelea kama ilivyopangwa kutokana na ukosefu wa mchanga, kokoto na mawe.

Mwakilishi wa TYI, Abdullah Miraji Othman, alisema juhudi zimefanywa na taasisi yake kwa kushirikiana na Zawa za kuandika barua katika taasisi zinazosimamia rasilimali zisizorejesheka, lakini bado upatikanaji umekuwa mdogo.

Miraji alitahadharisha kwamba mradi wa ujenzi huo umepangwa kukamilika ifikapo Desemba 31, mwaka huu, vinginevyo wafadhili waliojitolea kuuwezesha wataondoa fedha walizozitenga.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akiwa na mwenyeji wake mmoja kati ya viongozi wa juu wa Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E), katika ukumbi wa watu mashuhuri katika Uwanja wa Ndege wa Dubai, baada ya kuwasili kwa ajili ya ziara ya siku saba U.A.E juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Waziri afafanua mgawo bendera kwa masheha

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Shamata Shaame, amesema masheha hawatakiwi kununua bendera za serikali ambazo hutolewa bure katika maeneo ya ofisi zao.

Shaame alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Tumbe, aliyelalamikia kitendo cha masheha kununua bendera ambayo hugharimu Sh. 80,000.

Alisema masheha ni wawakilishi wa serikali katika utawala wa chini ya shehia zao na wanatakiwa kupewa bendera kuonyesha hadhi yao.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, masheha wanapata mgawo wa bendera kwa mujibu wa mahitaji yao halisi na wanapatiwa bure.

"Masheha ndio watawala na watendaji wa shehia kwa hiyo wanawajibika kupewa bendera bure kwa ajili ya mahitaji ya ofisi zao," alisema.

Aidha, alisema serikali iko katika mchakato wa kujenga ofisi za kudumu kwa masheha ili watekeleze majukumu yao ya kazi kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, alisema kwa sasa masheha wanatumia nyumba zao binafsi kama ofisi za kufanyia kazi kwa mujibu wa mazingira yao. "Tunafikiria kuwapatia ofisi masheha katika maeneo yao, lakini kwa sasa wanatumia nyumba zao ziliopo katika eneo husika la kazi kama ofisi," alisema.

# Watolewa hofu upatikanaji maji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kazi za usambazaji wa maji safi na salama zinaendelea hadi vijijini ikiwa ni mikakati inayotokana na utekelezaji wa Ilani yya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020.

Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Haroun Ali Suleiman, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua lini wananchi wa Michamvi watafaidika na huduma ya majisafi na salama.

Suleiman alisema juhudi za kuwapatia majisafi na salama wananchi wa Michamvi zinaendelea ikiwamo uchimbaji wa visima.

Hata hivyo, alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, baadhi ya visima vinavyochimbwa hutoa maji yenye mchanganyiko wa chumvi ambayo si mazuri kwa matumizi ya binadamu kama vile kunywa.

Aliwataka wananchi hao kuwa wastahimilivu wakati utekelezaji wa usambazaji maji safi na salama ukiendelea ambao utafikia tamati mwaka 2020 kwa mujibu wa ilani ya CCM.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 katika sekta ya majisafi na salama. Tumepanga kufikisha maji katika kijiji cha Michamvi Mkoa wa Kusini Unguja," alisema.

Alizitaja juhudi zinazochukuliwa kwa sasa kuwa ni pamoja na kujenga matangi makubwa mawili ya kuhifadhi maji na usambazaji wake kwa mikoa ya Mjini Magharibi Unguja na Kusini Unguja.

Alisema kupitia miradi ya serikali na washirika wa maendeleo zikiwamo Japan na China, kuna matarajio makubwa ya kumaliza kwa tatizo la majisafi na salama Zanzibar ifikapo mwakani.

**"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 katika sekta ya majisafi na salama. Tumepanga kufikisha maji katika kijiji cha Michamvi Mkoa wa Kusini Unguja," alisema.**

# Mapato ya ndani yasaidia miradi

Na Halima Ikunji, KALIUA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, inaongoza kwa kutoa fedha kwa wananchi kupitia vyanzo vyake vya mapato ya ndani ili kuwaunga mkono katika kukamilisha miradi ya maendeleo.

Fedha hizo zimetumika kata ya Zugimlole kwa kujenga shule ya sekondari mpya iliogharimu zaidi ya Sh. milioni 156 hadi kukamilika kwake.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, John Pima, alisema kuwa fedha hizo zimewawezesha kujenga shule ili kukuza kiwango cha elimu katika kata na kuwapunguzia wanafunzi kutembea umbali mrefu.

Pima alisema halmashauri ilianza utekelezaji wake wa kuijenga shule hiyo tangu Aprili 2015 na kukamilisha mradi huo mwaka huu na mpaka sasa wanafunzi wapo madarasani wakiendelea na masomo.

Alibainisha kwamba halmashauri baada ya kutoa fedha kutoka mapato yake ya ndani, wananchi walichangia Sh. milioni 54, halmashauri Sh. milioni 62, Serikali Kuu milioni 29, Mfuko wa Jimbo shilingi milioni tano na wadau ni shilingi milioni tano.

Diwani wa kata hiyo, Balikeka Ramadhani, aliishukuru halmashauri kwa kusaidia kutoa fedha hizo pamoja na za kutoka Serikali Kuu pamoja na wananchi wake kuonyesha moyo, hivyo ni jambo muhimu kwa watoto wao ambao walikuwa ukitembea umbali mrefu kufuata elimu.

Balikeka alisema kuwa halmashauri inatekeleza majukumu yake vizuri kupitia ilani ya chama tawala.

Mmoja wa wananchi, Jumanne Halfani, alisema shule hiyo ni mpya imewasaidia watoto wao kupata elimu bora na wanategemea kwamba masomo wanayoyapata watafaulu vizuri kwa kuwa na shule yenye kiwango cha hali ya juu.

**Diwani wa kata hiyo, Balikeka Ramadhani, aliishukuru halmashauri kwa kusaidia kutoa fedha hizo pamoja na za kutoka Serikali Kuu pamoja na wananchi wake kuonyesha moyo, hivyo ni jambo muhimu kwa watoto wao ambao walikuwa ukitembea umbali mrefu kufuata elimu.**

# Waziri Mkuu kuanza ziara siku nne Iringa

Na Friday Simbaya, IRINGA

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, anatarajia kuanza ziara ya kikazi mkoani Iringa leo hadi Septemba 29.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ali Hapi, na kuwataka wananchi mkoani hapa kujitokeza kwa wingi kumlaki kiongozi huyo wa kitaifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Hapi alisema Majaliwa, atatembelea miradi mbalimbali ya maendeleo, kuongea na watumishi pamoja na kufanya mikutano ya hadhara na wananchi katika maeneo mbalimbali.

Hapi aliongeza kuwa Majaliwa atafanya ziara katika wilaya za Mufindi, Kilolo, Iringa DC na Iringa Manispaa, ambapo atazungumza na watumishi, wananchi na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya elimu, afya, maji na miundombinu.

"Waziri Mkuu anatarajia kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya wiki ya viziwi duniani yanayotarajia kufanyika kitaifa mkoani Iringa," alisema Hapi.

Pia atatembelea mradi ya maendeleo inayotekelezwa na sekta binafsi ikiwamo miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

Hapi wametaka wananchi mkoani kujitokeza kwa wingi kumlaki kiongozi huyo pamoja na kuonyesha ushirikiano kwake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alisema usalama utaimarishwa kuhakikisha hakuna vitendo vya uhalifu.

Bwire aliwataka pia wenye hoteli mbalimbali kuhakikisha wanaweka usalama katika maeneo yao kwa vile kutakuwa na ugeni mkubwa wa kitaifa. Chama cha Viziwi Tanzania (Chavita) kupitia tawi la Mkoa wa Iringa na asasi mbalimbali za viziwi zimepanga kuadhimisha Wiki ya Viziwi Duniani Septemba 28, mwaka huu, yatakayofanyika kitaifa mkoani hapa.

Chavita hujumuisha taasisi za shule za viziwi, wazazi viziwi, wasanii viziwi, shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania (Shivyawata), vyama vyenye watu wenye ulemavu na wadau wengine.

Akizungumza na wanahabari jana mjini Iringa, wakati wa kikao cha kwanza cha kamati ya maandalizi Katibu wa Chavita Iringa, Shaibu Juma Shaibu, akisaidiwa kutafsiri na mkalimani wake, Joshua Logan, amesema maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika Septemba 28, mwaka huu mkoani hapa.

Amesema lengo kubwa la maadhimisho hayo ni kujenga mwamko wa jamii kuhusu haki za viziwi hususani utambuzi rasmi wa lugha ya alama kama njia ya mawasiliano kwa viziwi na fursa ya watoto viziwi katika maendeleo ya kielimu, kukuza vipaji na kuweza kutimiza ndoto zao wakiwa kama sehemu ya nchi.

Shaibu aliongeza mgeni rasmi wa maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Majaliwa.

Hata hivyo alisema siku ya maadhimisho ya wiki ya viziwi ni moja ya kumbukumbu ya kufanyika kwa mkutano wa kwanza wa Shirikisho la Viziwi Duniani (WFD) uliofanyika Septemba 1951 mjini Rome, Italia.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, akitoa somo kwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Masasi jana, kuhusu uanzishwaji wa miradi ya kimaendeleo kwenye maeneo yao. Byakanwa aliwataka watumishi hao, kuwekeza wakiwa bado kazini, badala ya kusubiri kustaafu. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Siku 37 za waziri ujenzi vituo afya

Na Josephine Majura, KONDOA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ametoa siku 37 kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kuhakikisha ujenzi wa vituo vitatu vya afya.

Vituo hivyo ni vya Bereko, Thawi na Kalamba vinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi. Dk. Kijaji ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kondoa Vijijini, alitoa maagizo hayo alipofanya ziara ya kutembelea miradi ya ujenzi wa vituo vya afya vinavyojengwa kwa fedha za serikali katika vijiji mbalimbali wilayani Kondoa mkoani Dodoma, ambapo alibaini kuna uzembe katika umaliziaji wa ujenzi wa baadhi ya vituo hivyo kikiwamo Kituo cha Afya Kalamba.

Alielezea kutoridhika na utendajikazi wa uongozi wa halmashauri ya wilaya hiyo katika usimamizi wa miradi hiyo muhimu kwa wananchi, wakati serikali ilikwishatoa fedha zote za kukamilisha miradi hiyo na kuagiza hadi Oktoba 30, mwaka huu miradi hiyo iwe imekamilika.

"Dhamira njema ya serikali ya kuleta milioni 400 kwenye kituo hiki cha afya ni kupata huduma, lakini hatujaanza kutoa huduma hiyo kwa zaidi ya mwaka sasa," alisema Kijaji.

Aliiagiza Ofisi ya Mkoa na Wilaya kuhakikisha wanafuatilia vizuri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi inayofadhiliwa na serikali ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati kwa sababu serikali haianzishi mradi mpya bila kutoa fedha zote za miradi husika.

Serikali ilitoa fedha kwa nyakati tofauti kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vituo vya afya vitano wilayani Kondoa, kati ya vituo hivyo, vituo viwili vya Mauno na Busi vimekamilika, huku vituo vitatu vya afya vya Bereko, Thawi na Kalamba havijakamilika.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kondoa, Mashauri Vincent, alimwahidi Kijaji kutekeleza magizo yote aliyoyatoa hasa ya kulipwa kwa watumishi waliofanya kazi mbalimbali kwenye vituo hivyo vya afya ndani ya siku 14. Naye Mwanakijiji wa Mauno, Haji Selemani, aliishukuru serikali kwa juhudi mbalimbali inayofanya katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hasa huduma za jamii na kusifia huduma inayotolewa na Watumishi wa Kituo cha Afya Busi.

Mwanakijiji cha Bereko, Juma Saidi, alimpongeza Kijaji kwa kazi kubwa anayoifanya jimboni huko na kumwombea afya njema ili awe na nguvu ya kufanya kazi na zaidi.

HABARI KIMATAIFA

# Iran yataka vikosi vya kigeni kuondoka Ghuba

**TERHAN, Iran**

RAIS wa Iran amesema kuwa nchi yake ndiyo inastahili kuongoza usalama wa kikanda katika Ghuba ya Uajemi na kuonya kuhusu kuwapo kwa majeshi ya kigeni katika eneo hilo.

Hayo yanajiri wakati mkataba wa nyuklia wa nchi hiyo na nchi zenye nguvu duniani unasambaratika, Marekani ikitumia vikosi zaidi kwa ajili ya kuongeza usalama kwa washirika wake wa Kiarabu.

Akizungumza wakati wa gwaride la kijeshi, Rais Hassan Rouhani alisema kwamba uwapo wa majeshi ya kigeni katika Ghuba huenda ukasababisha matatizo kwa usalama wa nishati duniani.

Alisema Iran inaunyoosha mkono wa urafiki na udugu kwa mataifa mengine ya kanda hiyo kwa kusimamia usalama katika Ghuba ya Uajemi na njia ya bahari ya Hormuz ambapo asilimia 20 ya mafuta yanayouzwa nchi za nje yanapitia.

Marekani imesema Iran ndiyo iliyohusika na mashambulizi katika miundombinu muhimu ya mafuta ikiwamo mashambulizi yaliyofanywa kwa ndege zisizokuwa na rubani katika miundombinu ya uzalishaji mafuta huko Saudi Arabia.

**Baadae, Marekani ilitangaza nyongeza ya vikwazo kwa Iran kwa kuilenga Benki Kuu ya nchi hiyo.**

Hata hivyo, Iran imekanusha madai hayo na kusema mashambulizi yoyote ya kulipiza kisasi yatakayofanywa na Marekani yatasababisha kuanza kwa vita.

Kufuatia mashambulizi hayo, Rais wa Marekani Donald Trump alikuwa amezungumzia uwezekano wa kujibu kijeshi ambapo aliandika katika mtandao wa kijamii wa Twitter kwamba Marekani iko tayari.

Baadae, Marekani ilitangaza nyongeza ya vikwazo kwa Iran kwa kuilenga Benki Kuu ya nchi hiyo.

Mwishoni mwa wiki, Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper alitangaza kuwa Marekani inatuma nguvu mpya ya majeshi kwa Saudi Arabia baada ya ombi la nchi hiyo ya kifalme, akisema kuwa vikosi hivyo vya jeshi vitashughulika na masuala ya ulinzi na hasa ulinzi dhidi ya makombora ya angani.

**DW**

# Sababu kifo cha Mugabe yaelezwa

**HARARE, Zimbabwe**

SERIKALI ya Zimbabwe imesema kuwa rais wa zamani nchini humo, Robert Mugabe alifariki kutokana na kusumbuliwa na maradhi ya saratani.

Imesema kwamba matibabu ya chemotherapy anayepatiwa mgonjwa wa saratani kupunguza sumu mwilini yalisitishwa kwa Mugabe wakati ilipodhihirika kuwa hayatamsaidia tena.

Mugabe alifariki mapema mwezu huu nchini Singapore akiwa na umri wa miaka 95.

Anatarajiwa kuzikwa katika kaburi kwenye eneo la kitaifa la kuzikwa mashujaa ambalo linajengwa mjini Harare. Ni sehemu ambapo wapiganiaji uhuru wengi nchini humo walio maarufu wamezikwa.

Ikiwa ni mara ya kwanza kufichuliwa kwa chanzo cha kifo cha kiongozi huyo wa zamani, Rais wa Zimbabwe Emmerson Mnangagwa amenukuliwa na vyombo vya habari akiwaambia wafuasi wa chama tawala Zanu- PF mjini New York, ambako amekwenda kuhudhuria mkutano mkuu wa Umoja wa mataifa, kuwa Mugabe alikuwa na saratani, lakini hakufichua ni saratani ya aina gani.

"Matibabu yalisitishwa, madaktari walikatiza matibabu, chemotherapy, kwa sababu ya umri wake na pia kwa sababu saratani yake ilikuwa imesambaa na matibabu yalikuwa hayasaidii tena," alisea Rais Mnangagwa katika matamshi yaliochapishwa kwenye gazeti la The Herald.

Kwa kadri miaka yake ilivyozidi kuongezeka sambamba na matatizo ya kiafya yakizidi kuongezeka yalileta minong'ono ya nani wa kuichukua nafasi yake.

Lakini fitna ziliendelea kufanyika kwa wale walioonekana wanaweza kuchukua nafasi yake na hivyo kuthibitisha namna uongozi wa Zimbabwe unashikiliwa na Mugabe pekee.

Na hata Mugabe alionekana kuvunja nguvu ya utawala wowote uliokuwa kinyume nae.

Kufuatia uvumi wa mkewe Grace kutaka kutawala pale mume wake atakapofariki akiwa madarakani Mugabe alitangaza nia yake ya kugombea tena mwaka 2018 ambapo angekuwa na umri wa miaka 94.

Na katika kuondoa maswali yaliyokuwa yamebaki kati ya wale waliokuwa wakidhaniwa huenda wangekuwa warithi, Mugabe alitangaza rasmi kuwa ataendelea kuwa madarakani mpaka pale Mungu atakapomuita.

Kufuatia tukio hilo haikuwa tena Mungu ila ni umoja wa majeshi wa Zimbabwe ndiyo yaliyomuita Mugabe.

Mnamo Novemba, 2017 aliwekwa kizuizini kwa siku nne huku aliyekuwa makamo wake Emmerson Mnangagwa akichukua nafasi yake kama kiongozi wa Zanu-PF.

Novemba 21 Spika wa Bunge la Zimbabwe alitangaza rasmi kujiuzulu kwa Rais Mugabe baada ya muda mrefu kukataa kibabe kufanya uamuzi huo.

Mugabe alifikia makubaliano ya kupata ulinzi kwake na familia yake kutokana na hofu ya kuuawa na kuendeleza biashara yake. **BBC**



Rais wa Iran, Hassan Rouhani, akihutubia wananchi kuhusu uwapo wa vikosi vya kigeni katika ghuba ya Uajemi. **PICHA: ALLIANCE**

# Waarabu waapa kumng'oa Netanyahu

**YERUSALAMU, Israel**

WABUNGE Waarabu nchini Israel wamependekeza kuwa Mkuu wa Majeshi wa zamani nchini humo, Benny Gantz ndiye anayepaswa kuwa Waziri Mkuu.

Katika uchaguzi uliopita kiongozi wa Israel, Benjamin Netanyahu alikuwa bega kwa bega na Gantz, na wawili hao sasa wanawania kuunda serikali ya mseto.

Miongoni mwa vyama vilivyo katika orodha ya vile vitakavyounda serikali ya mseto ni pamoja na muungano wa vyama vya waarabu ambavyo vilishika nafasi ya tatu vinavyosema vinataka kumuondoa madarakani.

Hii ni mara ya kwanza tangu mwaka 1992 kwa kikundi cha wanasiasa wa kiarabu nchini Israel kumuidhinisha Waziri Mkuu Baada ya uchaguzi wa kwanza uliofanyika April, mazungumzo ya muungano yalivunjika na uchaguzi ukaitishwa.

Akikabiliwa na mkwamo wa kisiasa , Rais wa Israel, Reuven Rivlin alitendekeza kuwapo kwa serikali mpya itakayojumuisha muungano wa Blue unaongozwa na Gantz na ule mweupe pamoja na chama cha Waziri Mkuu, Netanyahu cha Likud.

Rivlin alieleza kuwa atafanya kila liwezekanalo kuepuka uchaguzi mkuu wa tatu kufanyika nchini humo kwa mwaka huu.

Kiongozi wa muungano, Aymen Odeh, alimweleza Rivlin kwamba kipaumbele cha muungano wao ni kumzuwia Netanyahu kuongoza kwa muhula mwingine. Muungano huo wa vyama vya kiarabu una viti 13 bungeni.

Gantz aliidhinishwa na wabunge wote 13 lakini bado atahitaji viti 61 vinavyohitajika kupata wingi wa viti katika bunge la Israel lenye viti 120.

Rais Rivlin anashauriana na viongozi wa chama kuhusu ni nani ambaye atamuomba kuongoza nchi baada ya matokeo ya uchaguzi wa wiki iliyopita ambao hayakutoa matokeo kamili.

Vyaka vya kiarabu vimeonyesha nguvu kwa kushika namba tatu kwa idadi ya viti vya bunge.

Hata hivyo, uungwaji mkono wao hautampa wingi wa viti Gantz na muungano wa bluu na nyeupe, lakini utamuinua katika mazungumzo kuhusu ni nani atapata nafasi ya kwanza ya kuunda serikali.

Akizungumza na wafuasi wakati wa kampeni za uchaguzi, Netanyahu alisema: "Sote tumepitia kampeni ngumu ya uchaguzi, bado tunasubiri matokeo yenyewe. Israel ipo katika kiwango cha historia, tumekabiliwa na changamoto nyingi na fursa nyingi."

Kwa upande wake Gantz alionekana kuwa na matumaini zaidi alipozungumza na wafuasi wake mapema kidogo, na kusema: "Bila shaka tutayasubiri matokeo halisi, lakini inavyoonekana ni kana kwamba tumelifikia lengo letu.Umoja na utangamano upo mbele yetu."

**BBC**

# Kamanda Moro aacha ujumbe mzito akiaga

**Na Idda Mushi, Morogoro**

ALIYEKUWA Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, amewataka wananchi wa Morogoro kushirikiana na Jeshi la Polisi kusaidia ujenzi wa makazi bora ya askari wa jeshi hilo.

Sambamba na hilo, Mutafungwa aliyehamishiwa makao makuu ya jeshi hilo, amesisitiza nidhamu kwa askari ili kufanikisha utendaji kazi.

Mutafungwa alisemsa hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuwaaga askari polisi wa vikosi mbalimbali vya Mkoa wa Morogoro na kutembelea nyumba 10 zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa katika kambi za polisi za wilayani Morogoro na Mvomero.

Hakusita kuonyesha hisisa zake kwa kumpongeza Rais John Magufuli na Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro kuwezesha ujenzi huo na kuamsha ari kwa wananchi kujitokeza kuchangia ukamilishaji wake.

Kamanda Mutafungwa alishukuru kwa ushirikiano ulioonyeshwa na wananchi katika shughuli mbalimbali za usalama wa raia na mali zao na kuwataka wasichoke kuchangia mahitaji mbalimbali ya jeshi hilo, hasa kwa kuhakikisha polisi na wafanyakazi raia wa jeshi hilo wanakuwa na makazi bora.

"Tunamshukuru pia Rais kwa uhamasishaji na uchangiaji wa ujenzi wa kituo cha polisi Kisaki ambacho kitasaidia pia kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mradi mkubwa wa umeme wa Julius Nyerere Rufiji. Naamini hata kamanda anayekuja ataendeleza kasi iliyoanzishwa na kuhakikisha kituo kile kinakamilika," alisema.

Askari akiishi kambini ni jambo jema sana kiusalama. Hata kukitokea changamoto zozote ni rahisi kuitwa na kukimbia kuwajibika kwa wakati kwani yuko jirani na yuko katika makazi salama ya kuishi," aliongeza.

Kuhusu Mvomero, alisema kuna eneo kubwa lililoanza kujengwa nyumba saba za askari na tano kati ya hizo zimekamilika na zimeanza kutumiwa na familia 10 za askari, huku zingine mbili zikiwa zimeanza kujengwa na wananchi wenyewe waliohamasika kushirikiana na polisi kuboresha makazi ya askari.

Kamanda Mutafungwa alisema eneo hilo pia kwa baadaye limeachwa katika mpango mkakati lijengwe shule ya awali na zahanati itakayotumiwa na askari na wananchi wa jirani. Pia litatumika kwa kantini ili askari wapate sehemu ya kupumzika na kuburudika na eneo hilo litajengwa pia kituo kikuu cha polisi cha wilaya ya Mvomero kwa kuwa eneo kilipo kwa sasa, Wami Dakawa, ni finyu.

Baadhi ya askari, walielezea kuridhishwa na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Kamanda Mutafungwa hasa kwa kuhakikisha utendaji kazi na nidhamu vinaimarishwa.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), akimkabidhi cheti Mkuu wa Taaluma wa Shule ya Tusiime, Maxon Binomtonzi, baada ya shule yake kufanya vizuri kitaaluma, katika hafla iliyoandaliwa na mkoa huo, wikiendi, kwa ajili ya kuwazawadia walimu na wanafunzi waliofanya vizuri kielimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wafanyabiashara wawekewa taratibu uwasilishaji kero

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Viwanda na Biashara, imetangaza utaratibu maalum wa kuwasilisha changamoto, vikwazo na kero zote zisizo za kikodi za maeneo ya mipakani ambazo wafanyabiashara wanakutana nazo.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alitangaza utaratibu huo mpya jana kwa wanahabari na kusema, lengo ni kuwezesha wafanyabiashara kupata huduma haraka kupitia wizara na taasisi mbalimbali za Serikali zinazotoa huduma mipakani.

Alisema kwa kuanzia wizara imetoa anuani maalumu za barua pepe na namba za simu za watendaji ambazo kila mfanyabiashara anayepata vikwazo aweze kutoa taarifa kupitia namba hizo.

"Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa biashara za mipakani zinaimarishwa na kufanyika kwa ufanisi zaidi kwa kuondoa vikwazo vyote vya kikodi na visivyokuwa vya kikodi na kuwezesha wananchi na taifa kwa ujumla kunufaika na kukuza biashara," Manyanya alisema.

Aidha, aliwataka wakuu wa taasisi hizo walioko kwenye vituo vya mipakani kubandika orodha hiyo kwenye mbao za matangazo ili kurahisha mawasiliano.

Alitaja vikwazo vinavyotakiwa kuripotiwa ambavyo siyo vya kikodi ni pamoja na rushwa ya kifedha na isiyo ya kifedha, urasimu na kutotoa miongozo ya taratibu zinazohitajika, kukosa taarifa muhimu na kutojua fursa zilizopo.

Manyanya alizitaja wizara na taasisi zinazotoa huduma mipakani ni pamoja Mamlaka ya Mapato (TRA); Idara ya Uhamiaji; Wakala wa Vipimo (TBS); Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA); Mkemia Mkuu wa Serikali; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) na Kitengo ya Huduma za Afya ya Mimea.

Nyingine ni Idara za Maliasili na Utalii, Idara za Mifugo na Uvuvi Halmashauri za Wilaya na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade).

# Waziri apigia debe matumizi fursa za bahari

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WANANCHI na wadau mbalimbali wamehimizwa kutumia fursa kuwekeza katika bahari, mito na maziwa ili kufanya sekta ya usafiri wa maji kuwa nguzo ya uchumi nchini na duniani kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Siku ya Usafiri wa Maji Duniani, ambayo huadhimishwa Alhamisi ya mwisho wa Septemba kila mwaka, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema asilimia 90 ya usafirishaji mizigo duniani unatumia njia ya maji, hivyo ni fursa kwa wananchi kuwekeza katika sekta hiyo.

Maadhimisho hayo kitaifa yanafanyika mkoani Mwanza na kilele ni keshokutwa.

Kwandikwa alisema lengo la maadhimisho hayo ni kudumisha, kuimarisha, kuenzi na kukumbushana juu ya umuhimu wa usafiri kwa njia ya maji katika kuboresha biashara za kimataifa na kitaifa ili huduma hiyo kuwa bora.

Wakati akihimiza matumizi hayo, Kwandikwa alisema serikali imedhamiria kuondoa vikwazo vya kibiashara katika sekta hiyo vitakavyosaidia kufikia malengo endelevu ya taifa.

Alisema serikali inashirikiana na Chama cha Wanawake wanaofanya kazi katika sekta ya bahari (maji) Afrika Mashariki na Kusini (Womesa) Tanzania, kuhakikisha wanawake wanapata fursa, haki na uhuru wa kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazohusu na sekta hiyo ili kukuza uchumi na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

"Kaulimbiu ya kitaifa ya mwaka huu ya maadhimisho haya inasema 'Kuwazesha Wanawake katika Sekta ya Usafiri kwa njia ya maji' ambayo inatukumbusha kuzingatia usawa wa kijinsia katika utoaji wa fursa za mwanamke katika masuala mbalimbali ya sekta hiyo kwani wanawake ni nguzo muhimu kwenye maendeleo," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (Tasac), Emmanuel Ndomba, alisema shirika hilo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Na. 14 ya mwaka 2017 na kuanza kutekeleza majukumu yake mwaka jana kwa lengo la kudhibiti sekta ya usafiri wa majini.

"Shirika letu linasimamia pia utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya Shirika la Bahari Duniani (IMO) iliyoridhiwa na Tanzania. Maadhimisho hayo yalianza baada ya shirika hilo la bahari kutimiza miaka 20 na kuridhia yawe endelevu kwa kila mwaka ambayo yanaendana na maadhimisho ya miaka 70 ya IMO," alisema Ndomba.

Naye Mwenyekiti wa Womesa, Mhandisi Fortunata Kakwaya, aliwataka wazazi kuhamasisha watoto wa kike kujiunga na sekta ya bahari (maji), licha ya kuwapo kwa changamoto ambazo zinaweza kuwa fursa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI



**Joyce Frank Kallaghe** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0233-0543** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari **St. Mary's Mazinde Juu.**

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/KIJ/RB/315636/2019

### KUPOTEA KWA CHETI



**Jane L. Maiga anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3535/0031 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Shule ya Sekondari Debrabant .**

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: DAR/MBA/RB/318279/2019**

215429702

### KUPOTEA KWA CHETI



**Lissa Daniel Kalokola** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0248-0528 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya Sekondari Marian Girls.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Report Namba:**
**991089954783**

115429302

### PRIMARY COURT (ADMISTRATION OF ESTATES)

Citation
Katika Mahakama ya Mwanzo MABIRA
Usimamizi wa Mirathi No: 12/2019

Ombi la SAIMON HENERIKO kuteuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi ya Marehemu HENERIKO BITAMANYIRWE
Kwa watu wote Wanaohusika

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo mnaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka, mnamo tarehe 30.09.2019 kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 9.9.2019

MAHAKAMA YA MWANZO MABIRA - KARAGWE

SAHIHI YA HAKIMU

215429902

### IN THE RESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA
RM.CIVIL CASE NO: 11/2019

MUSSA OMARY ....................PLAINTIFF
VERSUS
ALLY MOHAMED ................. 1ST DEFENDANT
JAMES GAIDON ....................2ND DEFENDANT
LASAR LOGISTICS CO, LTD......3RD DEFENDANT

**NOTICE OF MENTION**

TO: ALLY MOHAMED
P.O.BOX DAR-ES-SALAAM.

TAKE NOTICE that the mentioned case has been set down for MENTION on the 15RD day of OCTOBER, 2019 at 8:30 O'clock in the forenoon, Before Hon. J.D LUAMBANO -RM. Your presence is therefore requires on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 23th day of SEPTEMBER,2019.

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

215430002


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII


### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

22/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMANNE tarehe **24/09/2019** kampuni ya **LOGISTICS FOR SUB SAHARA,** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MTUKULA** kuelekea **TUNDUMA** kupitia **MIKUMI**. Magari yenye namba za usajili
2. Gari hilo lenye namba ya usajili zenye vipimo vyake:

   **TRUCK NO. 280 SSC FS/HL 04 SF GP**

   | | | | |
   |---|---|---|---|
   | Urefu | - | mita | 22 |
   | Upana | - | mita | 4.0 |
   | Kimo | - | mita | 4.75 |

3. Njia itakayotumika: **MTUKULA** kuelekea **TUNDUMA** kupitia **MIKUMI.**
   Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115428902

### IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR MARA AT MUSOMA

APPLICATION NO. 41 OF 2019

TWAHA ABUDUL ..............................APPLICANT
VERSUS
1. CHARLES CORDINIUS
2. SAMWEL KANILA................RESPONDENTS

**SUMMOUNS/NOTICE**

TO,
SAMWEL KANILA

The above mentioned applicant has instituted a suit in this Tribunal, against you, particulars of which are mentioned in a copy of the Application which is obtainable from the registry of this Tribunal, YOU ARE HEREBY SUMMONED TO APPEAR IN THIS TRIBUNAL in person (s) or by recognized agent(s) for mention on 02nd October, 2019 at 08:00am in the fore noon.

TAKE NOTICE THAT;
In default of your appearance on he said day, the above mentioned Suit shall be mentioned and determined in your absence.
Given under my hand and seal of this Tribunal this.................................. day of ........................ 2019.

Scanned with CamScanner

215430002


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# BENZEMA

## AMSHUSHA PRESHA ZIDANE MADRID

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane amebainisha kwamba ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sevilla juzi Jumapili umemfanya kuwa ameridhika na matokeo hayo.

Kocha huyo alikuwa akikabiliwa na wakati mgumu baada ya Madrid kuchapwa mabao 3-0 na PSG kwenye mechi ya ufunguzi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini bao la Karim Benzema la kichwa la kipindi cha pili dhidi ya Sevilla lilibadilisha mambo kwa miamba hao wa La Liga.

Sevilla ilishinda mechi zake nne zilizopita kati ya miamba hao, lakini walishindwa kupenya ngome ya Madrid iliyokuwa inaongozwa na nahodha wake, Sergio Ramos.

Alipoulizwa na televisheni ya Movistar kama matokeo hayo yamebadilisha chochote kwa upande wake, Zidane alijibu: “Ndio, ni mchezo ulionichacha mimi nimetosha na matokeo tangu nimerudi tena hapa.

“Walisaidiana mno dimbani. Tulikuwa na wakati wa aina yake, lakini walicheza kwa kujituma na kwa bidii kubwa na tukaweza kupata matokeo. Kwa uhakika nimeridhishwa na matokeo.”

Wakali Eden Hazard, James Rodriguez na Gareth Bale wote walishindwa kuonyesha viwango vyao kwenye safu ya ushambuliaji, ingawa Zidane aliwatetea.

“Tunajua kwamba wanaweza kutengeneza hatari, lakini safu ya ulinzi ya kila mmoja ilikuwa muhimu zaidi kwa ushindi wetu,” aliongeza Zidane.

## SOLSKJAER: UMALIZIAJI TATIZO MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

BAADA ya kupokea kisago cha mabao 2-0 kutoka kwa ‘Wagonga Nyundo’ wa jijini London, West Ham United juzi Jumapili, Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema ameumizwa na matokeo hayo na wala hakutegemea, lakini pia akilia na safu ya ushambuliaji.

Man United ilikubali kichapo hicho, ikiwa ugenini jijini London kwa mabao yaliyofungwa na Andriy Yarmolenko na Aaron Cresswell, dakika ya 44 na 84.

Solskjaer amesema matokeo hayo ni mabaya na hayakubaliki kwa ustawi wa klabu hiyo ya Old Trafford.

“Nimesikitishwa na matokeo haya. Siku zote mtu anaumizwa anapofungwa, ulikuwa mchezo ambao tulipaswa kushinda lakini matokeo yamekuwa tofauti,”alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa timu hiyo.

Kocha huyo kutoka nchini Norway, aliongeza kuwa, kikosi chake kina matatizo katika umaliziaji



kwa kuwa kimekuwa kikitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini washambuliaji wanakosa umakini.

Kuumia kwa mshambuliaji wake tegemeo Marcus Rashford katika mchezo wa juzi, kulionekana kuigharimu timu hiyo kwani ilishindwa kufunga licha ya kupata nafasi.

Solskjaer alisema hana budi kukubaliana na kilichotokea juzi jijini London, na sasa anajipanga ili kufanikisha lengo la kufanya vema katika michezo inayofuata.

Hata hivyo, amesisitiza kupokea matokeo hayo kwa mtazamo chanya na anajipanga kukabiliana na changamoto zinazoikabili Man United.

Jumatatu Septemba 30, Man Utd itakuwa nyumbani Old Trafford wakiikaribisha Arsenal, katika mchezo wa Ligi Kuu England.

## EMERY AANZA NYODO ARSENAL

**LONDON, England**

BAADA ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Aston Villa juzi, Kocha wa Arsenal, Unai Emery amesema kikosi chake kitaendelea kucheza mpira kwa kuanzia nyuma kwa sababu hiyo ndiyo staili anayotaka timu yake icheze msimu huu.

Arsenal ilitoka nyuma kwa mabao mawili na kupata ushindi huo wa 3-0 dhidi ya Aston Villa kwenye Ligi Kuu England.

Kabla ya mchezo huo wa juzi, kocha huyo alijikuta kwenye lawama kubwa baada ya kutaka timu yake ianze mpira kwa kupiga pasi kuanzia kwenye benchi, kitu kilichowagharimu katika mechi dhidi ya Watford na kupoteza uongozi wao wa mabao mawili na kabla ya kupata sare ya 2-2, huku wakikoswa mara kadhaa na kunusurika kufungwa.

Wachambuzi wa mambo ya soka wamemkosoa Emery na kumwambia Arsenal haina wachezaji kama wa Manchester City wanaoruhusu mpira uanzie nyuma, hivyo kuendelea kung’ang’ania staili hiyo itamgharimu tu hapo Emirates.

Lakini, kocha Emery amepata jeuri ya kuendelea na staili yake hiyo baada ya Alhamisi iliyopita kupata ushindi wa 3-0 ugenini kwa Eintracht Frankfurt kwenye Europa League.

Kocha huyo Mhispania alisema anataka staili hiyo ndiyo iwe utambulisho wa Arsenal.

“Mechi ile ya Watford pengine ilikuwa ni makosa tu yamejitokeza, lakini tutaendelea kutumia staili yetu hiyo ya uchezaji,” alisema Emery.

“Kuanzia mpira kutoka kwa kipa, kisha mabeki wa kati, ndipo ufike kwenye kiungo na hatimaye kwa washambuliaji, huo ndio utakuwa utambulisho wetu, licha ya kwamba wakati mwingine tutacheza mipira mirefu.”



## HABARI MICHEZO




# ICARDI:

## NIMETUA PSG KUSHINDA MATAJI

**PARIS, Ufaransa**

MAURO Icardi amesema aliondoka Inter kwenda kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain ili kushinda mataji.

Icardi alihamia PSG kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu, huku miamba hao wa Ufaransa wakiripotiwa kwamba wana kipengele cha kumnunua mshambuliaji huyo kwa euro milioni 70.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye alitua hapo Inter kutoka Sampdoria mwaka 2013, alifunga mabao 111 kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na mabao 124 katika mashindano yote na kuwa nafasi ya nane kwa wachezaji wote wanaaongoza kwa kuzifumania nyavu hapo Nerazzurri.

Icardi alinyang'anywa unahodha hapo Inter msimu uliopita na kuachana na kocha, Antonio Conte na amesema muda ulikuwa muafaka kwake kuondoka pale San Siro.

"Nimekuja kucheza," amesema Icardi akiiambia Canal+.

"Kama umekuja hapana kuna kipendele cha kununuliwa, unajua mchezaji anajitoa kwa ubora wake wote kwa ajili ya kuhakikisha kwamba klabu inafanya maamuzi mazuri kwake. Tutaona nini kitatokea kipindi kijacho cha majira ya joto.

"Ulikuwa ni mwaka wangu wa saba pale Inter na ndoto yangu ilikuwa ni kucheza ligi ya mabingwa nikiwa na Inter, kitu ambacho nilikifanya msimu uliopita."

## Klopp asema Man City wanarahisisha ushindi

**LONDON, England**

KOCHA Jurgen Klopp amekubali kwamba, Manchester City inafanya ushindi uonekane rahisi baada ya Liverpool kushinda 2-1 dhidi ya Chelsea, wakishinda baada ya mabingwa hao kuwashindilia Watford mabao 8-0.

Wekundu hao walifurahia ushindi wao pale kwenye dimba la Stamford Bridge, kwa mabao ya Trent Alexander-Arnold na Roberto Firmino.

Chelsea walijaribu kujibu mashambulizi kupitia kwa N'Golo Kante aliyefunga bao la kufutia machozi, lakini wakashindwa kusawazisha hadi mwisho wa mchezo.

Alipoulizwa kama kikosi chake kipo kwenye kiwango kizuri zaidi msimu huu, Klopp aliiambia Sky Sports: "Ni aina yake, lakini tunatakiwa kuendelea kwenda mbele, hatufikirii sana kuhusu hilo.

"Hatutakiwi kufanya jambo liwe jepesi. Tunaigana katika kila mchezo na kutafuta mpira na hatimaye kupata ushindi.

"Unaendelea kupambana na nina uhakika tutaweza kumaliza ligi tukiwa kwenye nafasi nzuri zaidi.

"Kwa uhakika inaonekana ni kawaida, lakini presha kwa upande wetu ipo juu zaidi, na nina uhakika Man City watazidi kutupa presha kubwa zaidi."



## Mourinho: Siipendi Utd ya msimu huu



**LONDON, England**

JOSE Mourinho amebwatukia kiwango cha kikosi cha Manchester United kilichofungwa mabao 2-0 na West Ham na kusema kwamba haoni kama kuna kuimarika kwa timu hiyo ya kocha Ole Gunnar Solskjaer.

Mabao ya Andriy Yarmolenko na Aaron Cresswell yaliiadhibu United na kuwa kipigo chake cha pili kwenye Ligi Kuu katika mechi sita na Mourinho anaona kwamba, timu hiyo kamwe haitaimarika.

Alipoulizwa na Sky Sports kama anaona kuna mabadiliko chanya kwa kikosi cha United, Mourinho alisema: "Hapana... sioni chochote.

"Tulikuwa wabaya msimu uliopita, lakini sioni kuimarika kokote, hata kwa wachezaji hawa wapya watatu na sioni wachezaji watakuwa na mchango wowote.

"Lakini kama timu, sioni, siipendi inavyocheza. Nilishangazwa na matokeo wanayoyapata kwa sasa na sidhani kama Ole anaweza kuipeleka timu hii popote."

Kiungo wa zamani wa United, Roy Keane naye amebainisha wazi kwamba, Man United ya sasa ina kosa kitu fulani muhimu na wanatakiwa kutatua matatizo hayo mapema.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD PIGO UNITED, ANUKIA KUIKOSA ARSENAL

Lukaku, Sanchez sasa wakumbukwa, Solskjaer ategemea majaliwa ya majeruhi Mason na Martial kurejea mapema ili...

**Manchester, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford anaweza kuwa "nje kwa muda" kutokana na majeraha ya nyonga aliyoyapata wakati wa wakichezea kipigo dhidi ya West Ham, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Ole Gunnar Solskjaer.

Nyota huyo wa kimataifa wa England, Rashford alikumbwa na balaa hilo katika dakika ya 61 wakati United ikichezea kichapo cha mabao 2-0, na Solskjaer kulazimisha kumchezesha kiungo Jesse Lingard kama mshambuliaji wa kati kufuatia kutokuwapo kwa Anthony Martial anayeuguza majeraha ya paja na Mason Greenwood anayesumbuliwa na mafundofundo.

Solskjaer alithibitisha Rashford atafanyiwa vipimo zaidi jana na atakuwa akitumai kupata taarifa nzuri kufuatia kutokuwa na hazina katika safu yake ya ushambuliaji kutokana na kuondoka kwa Romelu Lukaku na Alexis Sanchez waliojiunga na Inter Milan ya Italia majira haya ya joto.

"Alihisi maumivu," Solskjaer aliiambia MUTV.

"Tutafanya vipimo kesho [jana] kuona ukubwa wa majeraha. Sijui atakuwa nje kwa muda mrefu kiasi gani, mimi si daktari. Lakini pengine anaweza kuwa nje kwa muda kidogo."

Jumatano United itaivaa Rochdale kwenye mechi ya Kombe la Ligi (EFL Cup) kisha itakuwa na mechi tatu ndani ya siku saba dhidi ya Arsenal, AZ na Newcastle United.

Solskjaer aliongeza: "Natumai Mason na Anthony watarejea katika mechi dhidi ya Arsenal na angalau mmoja kati yao dhidi ya Rochdale."

Kipigo hicho dhidi ya West Ham kinakifanya kikosi hicho cha Solskjaer kubaki na pointi nane tu kutokana na mechi sita za Ligi Kuu England ilizocheza hadi sasa.

## KWA UFUPI

**XAVI AWAZA KUMNOA MESSI**

KIUNGO wa zamani wa Barcelona, Xavi, ambaye anainoa Al-Sadd ya Qatari, amesema haitakuwa tatizo kwake kuwanoa wachezaji wenza wa zamani kama vile Lionel Messi, Luis Suarez na Sergio Busquets katika dimba la Nou Camp. ***(Ara - in Spanish)***

**MOURINHO AIPONDA UNITED**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho alisema timu hiyo ni "mbovu zaidi" kwa sasa kuliko wakati anatimuliwa Desemba mwaka jana. ***(Times)***

**SPURS WAMFUATA RICCARDO**

Tottenham imetuma mashushu kumtazama winga kinda wa Fiorentina na Italia U-21, Riccardo Sottil wakati huu wakipiga hatua ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Express)***

**CHELSEA KUMKOSA HYSAJ**

NAFASI ya Chelsea kuinasa saini ya beki wa kulia wa Napoli, Elseid Hysaj, 25, majira ya joto yajayo yamepunguzwa na klabu hiyo ya Serie A kufuatia kuwa tayari kumpa ofa ya mkataba mpya nyota huyo wa kimataifa wa Albanian. ***(Express)***

**EVERTON YAMTAKA POULSEN**

KOCHA wa Everton, Marco Silva amewaambia wasaka vipaji wake kuendelea kumtazama straika wa RB Leipzig, Mdenmark Yussuf Poulsen, 25. ***(Express)***

**KEANE AISIKITIKIA UNITED**

KIUNGO wa zamani wa Man United, Roy Keane "alishtushwa na kusikitishwa" na kwa namna ilivyokuwa mbaya wakati timu yake hiyo ya zamani ikichezea kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya West Ham Jumapili. ***(Sky Sports, via Evening Standard)***

**LUKAKU AMFAGILIA CONTE**

STRAIKA wa Inter Milan, Romelu Lukaku, 26, amabaye amejiunga na miamba hiyo ya Italia majira haya ya joto akitokea Manchester United, amesema kocha wa klabu hiyo, Antonio Conte ni mtu ambaye "ananisaidia kila siku na kunihamasisha". ***(Metro)***

**HODDLE AFUNGUKA KUUGUA**

KOCHA wa zamani wa England, Glenn Hoddle amesema anaishi katika "muda wa nyongeza" baada ya maisha yake kuokolewa kufuatia tatizo la moyo mwaka jana. ***(Mirror)***

**BALOTELLI KUANZA NA JUVE**

MSHAMBULIAJI wa Italia, Mario Balotelli, ambaye ataichezea Brescia kwa mara ya kwanza kwenye mechi dhidi ya Juventus kesho, amesema "alifanya kazi kwa bidii katika mwezi uliopita na nusu" kuliko "kipindi cha muongo mmoja kwenye kazi yake hiyo", wakati huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 akiwinda nafasi ya kuitwa katika kikosi cha timu ya taifa kitakachoshiriki michuano ya Euro 2020. ***(Football Italia)***

**PALACE YAMTEGA MCAMERON**

Crystal Palace, Leicester City na Middlesbrough ni kati ya klabu zinazovutiwa na beki wa kati wa Wolves, Mcameron John, 20, ambaye anaichezea kwa mkopo Doncaster Rovers. ***(Mail)***

**JUVE, CITY KWA HAALAND**

Juventus imeripotiwa kujiunga katika mbio za kuinasa saini ya straika wa Red Bull Salzburg, Erling Braut Haaland, 19. Manchester United na Manchester City pia zinavutiwa na huduma ya mshambuliaji huyo, ambaye alifunga hat-trick wakati timu yake ikiichaka KRC Genk mabao 6-2 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema wiki iliyopita. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# MALINDI YAPATA KIGUGUMIZI CHA KUIFUATA AL MASRY MISRI

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UONGOZI wa Malindi FC ya Visiwani hapa umesema haufahamu ni lini timu yao itaondoka nchini kuelekea Misri ili kucheza mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Masry.

Al Masry ambao katika mchezo wa kwanza uliopigwa wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Amaan walipata ushindi wa mabao 4-1, wanatarajia kuwakaribisha Malindi Jumamosi jijini Cairo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Malindi, Mohammed Masoud, alisema ndiyo kwanza uongozi wa klabu hiyo uko katika hatua za mwisho za kukamilisha hati za kusafiria na visa za wachezaji wao.

Masoud alisema mchakato huo umechelewa kukamilika mapema kutokana na idadi kubwa ya wachezaji kutokuwa na vitambulisho vya Taifa na kusababisha nyota hao kuanza kupoteza hamasa ya mchezo huo wa marudiano.

Alisema baada ya kukamilika kwa mchakato huo, watatangaza rasmi siku ya kuondoka pamoja na idadi ya wachezaji watakaosafiri. "Muda wowote tutakapokamilisha zoezi hili, timu itasafiri kuelekea Misri kwa ajili ya kukabiliana na Al-Masry, baadhi ya wachezaji ambao hawatapata hati za kusafiria au zitachelewa kutoka, hawatasafiri na badala yake wataondoka na wachezaji watakaofanikiwa kukamilisha mchakato huo," alisema Masoud.

Aliongeza kuwa licha ya kupoteza mchezo wa kwanza, bado kikosi hicho kinaamini kwamba lolote linaweza kutokea katika mchezo huo wa marudiano.

Malindi FC ilisonge mbele katika mashindano hayo kwa kuiondoa Mogadishu City ya Somalia kwa kupata ushindi wa ugenini wa bao 1-0, baada ya sare ya bila kufungana katika mechi ya kwanza.



Mshambuliaji wa Tanzania U-20, Andrew Simchimba akishangilia na wenzake kwa kuonyesha dole gumba baada ya kukamilisha hat-trick yake dhidi ya Ethiopia wakati wakishinda 4-0 kwenye mechi ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge U-20) iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Jinja nchini Uganda. Bao la kwanza lilifungwa na Kelvin John (Jezi Na. 10). **MPIGAPICHA WETU**

## Kipanga yatamba kufanya vema Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Kipanga inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Rashid Lato, amesema hana wasiwasi na kikosi chake na anaamini msimu huu kimejiandaa kufanya vizuri, tofauti na ilivyokuwa katika misimu iliyopita.

Lato alisema maneno hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Malindi FC, katika mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar uliochezwa juzi jioni.

Kocha huyo alisema msimu huu kikosi chake kiko imara na amewataka wadau na mashabiki wake wasahau dhana ya kwamba timu hiyo ni ya kupanda na kushuka daraja.

"Nina uhakika na timu yangu msimu huu, tumejiandaa kufanya vizuri ili kuondosha ile dhana ya timu hii hucheza Ligi Kuu msimu mmoja huku msimu mwingine ikishuka daraja," alisema Lato.

Aliongeza kuwa kikosi chake kimejipanga kuendeleza "ubabe" katika ligi hiyo kwa sababu wana malengo ya kutwaa ubingwa na kukata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa hapo mwakani.

"Tumeanza vizuri na wachezaji wanajituma sana wanapokuwa uwanjani, hakika katika mchezo huu siwezi kutoa makosa kwani wachezaji wote walijituma na walizitumia nafasi zote walizopata hadi tukatoka na ushindi," kocha huyo alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Malindi, Waziri Seif, alisema "kichapo" walichokipata kimetokana na wachezaji kutocheza vizuri hali iliyosababisha kupoteza nafasi chache za kufunga walizozitengeneza. Seif alisema kuwa Kipanga ilicheza vizuri na walistahili kushinda mchezo huo kutokana na wachezaji wake kuelewana vema na kufanikiwa kuondoka na pointi tatu muhimu.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena Ijumaa kwa "Maafande" hao wa Kipanga kuwakaribisha "Mabaharia" wa KMKM kwenye Uwanja wa Amaan.

# Tanzania, Kenya hapatoshi Cecafa

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 ya Tanzania Bara, inatarajia kuwakabili yosso wenzao kutoka Kenya katika mechi ya pili ya Kundi B katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jinja, Uganda.

Yosso hao wa Tanzania Bara watashuka uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Ethiopia wakati wenzao wa Kenya waliwapa kichapo cha mabao 5-0 Zanzibar (Karume Boys).

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila, alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa na ushindani, kwa sababu Kenya inaundwa na wachezaji wenye vipaji na wanaonekana kuwa na uzoefu wa mashindano ya kimataifa.

Katwila alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza kwa utulivu ili wapate ushindi na kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Kwanza kabisa napenda kuwapongeza wachezaji wangu kwa kupambana kupata ushindi katika mechi ya kwanza, haikuwa mechi rahisi, licha ya kuwa tulipata ushindi mkubwa, mechi inayofuata itakuwa ni dhidi ya Kenya, nayo tunatarajia itakuwa na ushindani, kama mlivyoona nao pia wameshinda, tofauti yetu, wao wana bao moja zaidi," alisema Katwila.

Aliongeza kuwa wachezaji wake wako katika hali nzuri, hana majeruhi na wako tayari kwa ajili ya mchezo huo wa leo, utakaochezwa kuanzia saa 7:00 mchana.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Zanzibar, dhidi ya Ethiopia.

Timu nane zitakazofanya vizuri katika hatua hiyo ya makundi, zitasonga mbele kucheza hatua ya robo fainali wakati fainali ya michuano hiyo itachezwa Oktoba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Gulu.

## MAKAMBA AENDA MAJARIBIO ISRAEL

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amemtakia mafanikio mchezaji chipukizi, Issa Makamba, ambaye anatarajia kuondoka nchini kwenda kufanya majaribio katika klabu ya Kiryat Shmona FC inayoshiriki Ligi Kuu Israel.

Makamba anakuwa mchezaji wa pili wa hapa nchini kwenda katika klabu hiyo, chini ya wakala Mnigeria, James Adeniyi.

Akizungumza jijini hapa jana, Mavunde, alisema kuwa anaamini Makamba ataitumia vema nafasi hiyo ili kukuza kipaji chake na pia kufungua milango kwa wachezaji wengine chipukizi kwenda kucheza soka la kulipwa.

Mavunde alisema wakala wa Makamba ameahidi kufungua akademi jijini Dodoma endapo nyota huyo atafuzu majaribio hayo aliyokwenda kufanya.

"Napenda kuishukuru Kampuni ya SG Sports kwa kumpatia Issa Makamba vifaa muhimu vya michezo wakati akijiandaa na safari hiyo, nawashukuru wote mlionisaidia kufika hapa, shukrani za pekee ziwaendee wabunge Anthony Mavunde na Mariam Ditopile, ahadi yangu kwa vijana ni kwamba sitawaangusha na nitajituma zaidi ili kuiwakilisha vema Tanzania," alisema Makamba.

Nahodha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), anatarajia kuondoka nchini mwishoni mwa wiki hii kuelekea Israel kuanza majukumu yake hayo mapya.

# Michezo

Jumanne Septemba 24, 2019

Nipashe





HABARI UK 30

## Rashford pigo United, anukia kuikosa Arsenal

**BINJUKA...**




Mshambuliaji wa Arsenal, Nicolas Pepe, akibinjuka mithili ya baiskeli miguu juu hewani, akijaribu kufunga wakati wakishinda mabao 3-2 dhidi ya Aston Villa kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. **PICHA: MTANDAO**

# DANTE AITWA YANGA KUONGEZA NGUVU CAF

●●● Mwakalebela asema hakuna namna, atangulia Zambia timu ikifuata leo, silaha zinazoifuata Zesco hizi hapa...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wawakilishi pekee wa nchi waliobaki katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga, wakiondoka nchini leo kuelekea Zambia kuwakabili Zesco FC, uongozi wa klabu hiyo umemtaka beki wake, Andrew Vicent 'Dante' kurejea kwenye kikosi hicho ili kuongeza nguvu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kuwa wanaamini uwapo wa beki huyo katika kikosi chao, unaimarisha safu ya ulinzi na wako tayari kumpokea, endapo atakubali kukutana na uongozi wa klabu hiyo.

Mwakalebela alisema wanaamini Yanga itasonga mbele katika mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika na hivyo wanahitaji mchango wa Dante kwenye michuano hiyo na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema kuwa wachezaji wote ni wazima na wamekuwa wakifanya vema kwenye mazoezi yanayoongozwa na Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera ambaye anashirikiana na Mzambia Noel Mwandila.

"Mimi na kiongozi mwingine tunaondoka leo (jana), lakini msafara kamili wa timu utaondoka kesho (leo), ila tunapenda kuweka wazi kwamba vijana wetu wako vizuri, tumewaandaa kimwili na kuwatayarisha kisaikolojia kwenda kupambana, tungependa kila mmoja ajitoe kwa ajili ya kusaka ushindi, hata Dante milango iko wazi kurejea kundini," alisema Mwakalebela.

Kuhusu fedha anazodai Dante, Mwakalebela alisema kuwa beki huyo anatakiwa kukubaliana na uamuzi wa kulipwa kwa awamu, kama ambavyo wachezaji wengine wanavyolipwa.

"Timu inamhitaji, kuhusu deni lake, nadhani angekuwa kikosini, muda huu lingekuwa linaelekea kumalizika, kwa sababu tulikubali kumlipa kwa awamu, mchango wake ni muhimu na timu inamhitaji," Mwakalebela alisema.

Aliwataja wachezaji watakaosafiri leo ni Metacha Mnata, Farouk Shikalo, Mapinduzi Balama, Raphael Daudi, Ali Mtoni, Lamine Moro, Kelvin Yondani, Ali Ali, Juma Abdul, Muharami Issa, Papy Tshishimbi na Feisal Salum "Fei Toto".

Wengine ni Mohammed Issa, Abdul-Aziz Makame, Sadney Khoetage, Juma Balinya, Patrick Sibomana, Mrisho Ngasa, Mybin Kalengo, Deus Kaseke na Jafari Mohammed.

Wachezaji watakaobaki kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kwa kukosekana vibali vya kimataifa (ITC) ni pamoja na Paul Godfrey 'Boxer', Issa Bigirimana 'Walcott' , David Molinga 'Falcao' na Selemani Moustafa.

Zesco inatarajia kuikaribisha Yanga katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko mjini Ndola.

# Mexime ampasua kichwa Aussems

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akiendelea kumkosa nahodha wake, John Bocco, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa kikosi chake kinakwenda Bukoba kuwakabili vijana wa Mecky Mexime, Kagera Sugar kwa "nguvu za ziada" ili kuweza kupata ushindi katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini humo.

Simba, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, walifungwa mechi zote mbili za msimu uliomalizika na timu hiyo ambayo iliponea chupuchupu kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema wamejipanga kucheza katika kiwango cha juu katika mechi zote za ligi hiyo kwa sababu wanataka kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Aussems alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na hawataudharau mchezo wowote wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mbelgiji huyo aliongeza kuwa anafurahi kuona wachezaji wake wanaonyesha ushindani katika mazoezi na hali hiyo inasaidia kuimarisha kikosi chake.

"Tunajua tunaenda kucheza na moja ya timu ngumu kwenye ligi, pia tulipoteza mechi zote mbili tulipokutana msimu uliopita, hatutaki kuona inajirudia, tunataka kufungua ukurasa mpya kwa kupata matokeo mazuri, tunaamini tutapata ushindi dhidi ya Kagera Sugar na Biashara United," alisema Aussems.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi cha mabingwa hao wa Bara kinatarajia kuondoka jijini Dar es Salaam kesho kuwafuata mabingwa hao wa Kombe la Tusker mwaka 2008.

"Tutaondoka Jumatano, ila nani ataenda na nani atabaki, bado tunafanyia kazi, hasa ukizingatia tutakuwa na mechi mbili huko, nadhani kesho (leo), tutakuwa na wakati mzuri wa kueleza kuhusu safari yetu, ila Bocco bado ni mgonjwa na hayuko katika mipango ya mwalimu," Rweyemamu alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >